# MASUALA YANAYOATHIRI UFUNZAJI NA UJIFUNZAJI WA SOMO LA UFAHAMU KATIKA SHULE ZA UPILI KATIKA KAUNTI YA KISUMU NCHINI KENYA

**Oloo Mary Aluoch**

**Tasnifu iliyowasilishwa kwa Mintarafu ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Taaluma ya Elimu ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.**

**NOVEMBA- 2018**

## UNGAMO NA IDHINISHO

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa popote na yeyote kwa minajili ya shahada yoyote au jambo jingine lolote lile. Hairuhusiwi kutolesha tasnifu nzima au sehemu yake bila kibali cha mtafiti au Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

Sahihi…………………………… Tarehe…………………………………

**OLOO MARY ALUOCH**

**EDK/G/01/2015**

Tasnifu hii imeidhinishwa kwa kibali chetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

Sahihi……………………… Tarehe…………………………

**DKT. SUSAN C. CHOGE**

Mhadhiri Mwandamizi

Idara ya Elimu ya Lugha na Fasihi

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro

Sahihi……………………… Tarehe…………………………

**DKT. FRED WANJALA SIMIYU**

Mhadhiri Mwandamizi

Idara ya Kiswahili na Lugha Zingine za Kiafrika

Chuo Kikuu cha Kibabi

## HAKI MILIKI

Tasnifu hii ni hakimiliki kwa mujibu wa mkataba wa BERNE, kifungu cha sheria cha haki miliki cha mwaka wa 1999, kulingana na sheria na hataza za kitaifa na kimataifa. Hakuna kibali kutolesha au kuchapisha tasnifu hii au sehemu yake kwa namna yoyote bila idhini ya mwandishi au Mkuu wa Kitivo cha Taaluma ya juu kwa niaba ya chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

## TABARUKU

Kwa Babangu Askofu Richard Oloo, Mamangu Mchungaji Mable Atia Oloo na Mume wangu Mchungaji John Wekesa Wanjala kwa kunifadhili na kunitia shime ya kuendelea na masomo yangu. Pia namtabarukia kakangu Caleb Ochieng Oloo pamoja na wanangu Hannah na Mercy kwa utulivu wao nilipokosa kuwashughulikia ipasavyo wakati nilipokuwa nikiishughulikia kazi hii.

## SHUKRANI

Kwanza, namshukuru Mwenyezi Mungu  kwa kunipa siha njema na fursa hii adimu ya kuendeleza masomo yangu.Nashukuru Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro kwa kunisajili kuendelea na masomo yangu. Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt Susan Choge na Dkt Fred Wanjala Simiyu kwa kufanikisha kazi hii.Vilevile nawapa shukrani Dkt Elizabeth Khalili Ombito, Bwana Shadrach Opunde, Bwana Erick Walela, Bwana Manase Luganda, Bi Rukia Salim, na Bwana Joseph Marani ambao walijitolea kwa hali na mali katika kuifanikisha kazi hii. Shukrani pia nazitoa kwa Dkt Joyce Kagendo kwa kunihimiza kuendelea na masomo yangu ya uzamili.

Pongezi kwenu wazamili wenzangu Bi Sussy Lichuma, Truphena Okello,  Alice Khayali Mukoko  na Catherine Ingosi wa shule ya Daisy  kwa  kunitia shime nilipokuwa nikiufanya utafiti huu.

## IKISIRI

Ufahamu ni mojawapo ya vitengo katika somo la Kiswahili. Ili mwanafunzi afaulu katika mtihani wa Kiswahili, hana budi kufanya vyema katika kitengo hiki muhimu. Kutokana na matokeo duni ya mtihani katika sehemu hii, mtafiti alilenga kuchunguza masuala yanayoathiri ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu katika kidato cha tatu katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi. Utafiti huu ulifanyika katika shule za upili katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi nchini Kenya. Utafiti uliongozwa na madhumuni muhimu yafuatayo: Kuchunguza mbinu za kufundishia anazozitumia mwalimu katika kufundisha somo la ufahamu katika kidato cha tatu; kutathmini matumizi ya nyenzo katika ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu; kuchunguza maandalizi ya mwalimu kuhusu ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu na kutathmini maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya utabia iliyoasisiwa na mwanasaikolojia Hull (1943) na kuimarishwa na Skinner (1957), (Deodutus 2015) Nadharia hii inasisitiza upataji na mabadiliko ya uwezo wa tabia inayotokana na michakato ya ujifunzaji na mazoea ya taaluma fulani katika mazingira mahsusi. Mabadiliko haya hutokea kutokana na mazoezi yanayoimarishwa. Nadharia hii ilitufaa katika utafiti wetu kuchunguza mbinu zinazotumiwa na walimu kufundishia ufahamu darasani pamoja na maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu ufahamu ambayo huweza kuathiri ufunzaji na ujifunzaji wa somo hili. Katika utafiti huu data ilikusanywa kwa kutumia hojaji na mwongozo wa usaili. Muundo wa usoroveya elezi ulitumika katika utafiti huu. Idadi lengwa ya utafiti huu ilikuwa walimu wote wa Kiswahili pamoja na wanafunzi wa kidato cha tatu wanaojifunza somo la Kiswahili katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi. Utafiti ulifanywa miongoni mwa shule 11 za upili.Walimu 18 waliokuwa wakifundisha somo la Kiswahili walihusishwa kwenye utafiti,huku wanafunzi 180 wanaojifunza somo la Kiswahili pia kuhusishwa. Sampuli ya kutumiwa ilikuwa theluthi moja ya idadi lengwa. Walimu waliojaza hojaji waliteuliwa kimakusudi kwa kuwa wote walikuwa wakifunza ufahamu wa kusoma katika kidato cha tatu. Utafiti huu ulitumia tarakimu elezi dafaa, majedwali na asilimia wakati wa uchanganuzi wa data. Aidha kila sehemu ilifanyiwa uchanganuzi kwa kutumia maelezo kutokana na data iliyotokana na utafiti. Mjadala wa matokeo ya utafiti ulielekezwa na malengo ya utafiti. Utafiti huu ulibainisha kwamba walimu hawazingatii matumizi ya nyenzo na mbinu mwafaka za kufundishia. Uchanganuzi wa data ulithibitisha kuwa, ufunzaji na ujifunzaji wa ufahamu ulikumbwa na changamoto kama vile maandalizi mabovu ya walimu nyanjani na hata wanapoenda darasani kufunza somo la ufahamu pamoja na walimu na wanafunzi kuwa na mielekeo hasi kuhusu somo la ufahamu. Matokeo ya Utafiti huu yatakuwa msingi bora wa kutoa maelekezo kuhusu jinsi ya kuimarisha ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu katika eneo la utafiti. Mapendekezo hayo aidha yataweza kutumiwa na washikadau katika maeneo mengine nchini ili kutatua matatizo yanayotinga ufanisi wa somo la ufahamu wa kusoma katika shule za Sekondari nchini. Utafiti huu vilevile utawaimarisha walimu kuhusu mbinu za kufundishia somo la ufahamu. Walimu wataweza kuelewa na kutumia mbinu bora za kufunzia somo la ufahamu. Wanafunzi nao watapata msingi bora wa kusoma na kuyajibu maswali ya ufahamu.

## ABSTRACT

Comprehension is one of the several compulsory sections in Kiswahili subject syllabus. For a student to perform well in Kiswahili exams, he or she has to do well in this section. Unfortunately, this is one of the most poorly performed section in Kiswahili. This study therefore sought to investigate the factors that affect the teaching and learning of Kiswahili reading comprehension in Secondary schools in Kisumu West sub county in Kenya. The objectives of this study were: To investigate the teaching strategies that the Kiswahili comprehension teachers use to teach Kiswahili reading comprehension; To assess the availability and use of learning and teaching aids by teachers in teaching Kiswahili reading comprehension;To find out whether Kiswahili teachers adequately prepared before going to teach Kiswahili reading comprehension lessons and, To investigate about teachers and learners'opinions towards the teaching and learning of Kiswahili reading comprehension.This study was guided by the behaviourism theory by Hull (1943) which was reinforced by Skinner (1957), (Deodutus 2015) This theory states that learning reflects the development of an S-R (stimulus-response) association. The research used descriptive survey design. The target population included all form three teachers of Kiswahili reading comprehension together with their Kiswahili students. Stratified sampling was used to select a representative sample of schools while simple random sampling was used to select teachers of Kiswahili and students.The research was carried out in 11 secondary schools, among 18 form three teachers of Kiswahili and 180 students which represented 30% of the total population. Data was analyzed using descriptive statistics. Data was presented using, tables, graphs and charts. Discussion of the findings of the research was guided by research questions. The findings of the data analysis showed that there were challenges in the teaching and learning of Kiswahili reading comprehension. The findings indicated that poor preparation by teachers in their teaching content, inappropriate teaching methodologies used by Kiwahili teachers, neglect of the use of relevant teaching materials and teaching aids and negative attitudes by teachers and students towards Kiswahili reading comprehension are the factors affecting the teaching and learning of comprehension. Based on the finding, it is recommended that the Kenya Institute of Curricullum Development should organize seminars and workshops for teachers of Kiswahili on the relevant topics and methods of teaching Kiswahili comprehension. The importance of this research is that, the findings are useful in teaching and learning of Kiswahili comprehension in Secondary schools not only in Kisumu West Sub-County, but also in other pats of Kenya and other places where Kiswahili comprehension is taught. The teachers will be able to understand the best instructional strategies for teaching reading comprehension. The learners will also get the required skills to read and answer comprehension questions correctly.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINISHO** ............ ii
**HAKI MILIKI** ............ iii
**TABARUKU** ............ iv
**SHUKRANI** ............ v
**IKISIRI** ............ vi
**ABSTRACT** ............ vii
**YALIYOMO** ............ viii
**VIELELEZO** ............ xii
**ORODHA YA MAJEDWALI.** ............ xiii
**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** ............ 1
1.1 Usuli wa Utafiti ............ 1
1.2 Suala la Utafiti ............ 8
1.3 Malengo ya Utafiti ............ 9
1.4 Maswali ya Utafiti ............ 9
1.5 Misingi ya Uteuzi wa Mada ya Utafiti ............ 10
1.6 Umuhimu wa Utafiti ............ 10
1.7 Nadharia ya Utafiti ............ 11
1.8 Upeo na Mipaka ya Utafiti ............ 18
1.9. Hitimisho ............ 18
1.10 Maelezo ya Istilahi ............ 19
1.11 Maelezo ya Vifupisho ............ 20
**SURA YA PILI: UHAKIKI WA MAANDISHI** ............ 21
2.1 Utangulizi ............ 21
2.2 Dhana ya Ufahamu ............ 21
2.3 Masuala Yanayoathiri Ufunzaji na Ujifunzaji wa Somo la Ufahamu ............ 22
2.3.1 Mbinu za Kufundishia ............ 22

2.3.2 Nyenzo za Kufundishia Somo la Ufahamu ........ 29

2.3.3 Maandalizi ya Mwalimu Nyanjani na Darasani ........ 34

2.3.4 Maoni ya Wanafunzi Kuhusu Somo la Ufahamu wa Kusoma ........ 37

2.4 Hitimisho ........ 40

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........ 41**

3.1 Utangulizi ........ 41

3.2 Muundo wa Utafiti ........ 41

3.3 Eneo la Utafiti ........ 41

3.4 Idadi Lengwa ........ 42

3.5 Uteuzi wa Sampuli ........ 43

3.6 Vifaa vya Utafiti ........ 44

3.6.1 Hojaji ........ 45

3.6.1.1 Hojaji ya Walimu. ........ 45

3.6.1.2 Hojaji ya Wanafunzi ........ 46

3.7 Mwongozo wa Maswali ya Usaili ........ 46

3.8 Uaminifu wa Vifaa vya Utafiti ........ 47

3.9 Uthabiti wa Vifaa vya Utafiti ........ 47

3.10 Majaribio ya Vifaa vya Kukusanyia Data ........ 48

3.11 Mchakato wa Ukusanyaji Data ........ 48

3.12 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data ........ 49

3.13 Changamoto Nyanjani ........ 49

3.14 Hitimisho ........ 50

**SURA YA NNE: UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO .. 51**

4.0 Utangulizi ........ 51

4.1 Mbinu za Kufundishia Ufahamu ........ 51

4.1.1 Matumizi ya Mbinu za Kufundishia ........ 51
4.1.2 Mara-idadi ya Matumizi ya Mbinu za Kufundishia ........ 53
4.1.3 Stahabu za Wanafunzi Kuhusu Njia za Ufundishaji wa Ufahamu ........ 55
4.1.4 Vigezo Vinavyotinga Uteuzi na Matumizi ya Mbinu ........ 57
4.1.5 Athari za Matumizi ya Mbinu Zisizo Mwafaka Kufundishia ........ 58
4.2 Nyenzo za Kufundishia ........ 59
4.2.1 Uwepo wa Nyenzo za Kufundishia ........ 60
4.2.2 Idadi ya Vitabu vya Kiada Shuleni Ikilinganishwa na Idadi ya Wanafunzi ........ 63
4.2.3 Utoshelevu wa Vitabu vya Kiada ........ 64
4.2.4 Matumizi ya Nyenzo ........ 65
4.2.5 Changamoto Zinazotinga Matumizi ya Nyenzo ........ 68
4.3 Maandalizi Ufundishaji wa Ufahamu wa Kiswahili ........ 69
4.3.1 Maandalizi ya Walimu Nyanjani ........ 70
4.3.2 Mchango wa Maafisa Wadhibiti Ubora na Viwango wa Elimu. ........ 72
4.3.3 Maandalizi ya Walimu Darasani ........ 73
4.4 Maoni ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Somo la Ufahamu ........ 75
4.4.1 Manufaa ya Somo la Ufahamu ........ 75
4.4.2 Kupenda Somo la Ufahamu ........ 77
4.4.3 Changamoto Zinazokabili Ufunzaji na Ujifunzaji wa Ufahamu ........ 83
4.4.4 Mapendekezo ya Suluhisho ........ 85
4.5 Hitimisho ........ 87
**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 88**
5.1 Utangulizi ........ 88
5.2 Muhtasari wa Matokeo ........ 88
5.2.1 Mbinu za Kufundishia Ufahamu ........ 89

5.2.2 Nyenzo za Kufundishia Ufahamu ........ 91

5.2.3 Maandalizi ya Walimu Kuhusu Ufundishaji wa Ufahamu ........ 93

5.2.4 Maoni ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Somo la Ufahamu ........ 95

5.3 Hitimisho ........ 97

5.4 Mapendekezo ........ 98

5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi ........ 99

**MAREJELEO ........ 101**

**VIAMBATISHO ........ 112**

**KIAMBATISHO A**: HOJAJI YA MWALIMU ........ 112

**KIAMBATISHO B**: HOJAJI YA MWANAFUNZI ........ 122

**KIAMBATISHO C**: MWONGOZO WA USAILI ........ 126

**KIAMBATISHO D**: ORODHA YA SHULE ZILIZOTAFITIWA ........ 127

**KIAMBATISHO E**: RAMANI YA KAUNTI NDOGO YA KISUMU ........ 129

**KIAMBATISHO F**: RAMANI YA KAUNTI NDOGO YA KISUMU MAGHARIBI ........ 130

**KIAMBATISHO G:** KIBALI CHA UTAFITI CHA NACOSTI ........ 131

**KIAMBATISHO H**: KIBALI CHA UTAFITI CHA NACOSTI ........ 132

**KIAMBATISHO I:** KIBALI CHA UTAFITI KUTOKA WIZARA YA ELIMU ........ 133

**KIAMBATISHO J**: KIBALI CHAUTAFITI KUTOKA KWA KAMISHONA WA KAUNTI YA KISUMU ........ 134

**KIAMBATISHO K:** KIBALI CHA UTAFITI KUTOKA KWA IDARA YA ELIMU YA KISUMU MAGHARIBI ........ 135

**KIAMBATISHO L:** HOJAJI YA MWALIMU ILIYOJAZWA ........ 136

**KIAMBATISHO M:** HOJAJI YA MWANAFUNZI ILIYOJAZWA ........ 148

**KIAMBATISHO N:** MATOKEO YA MTIHANI WA KITAIFA WA KISWAHILI – KAUNTI NDOGO YA KISUMU MAGHARIBI 2014 - 2015 ........ 152

**KIAMBATISHO O:** MTIHANI WA UFAHAMU ULIOFANYWA NA WANAFUNZI WA KIDATO CHA TATU ........ 154

## VIELELEZO

**Kielelezo 4.1:** Stahabu za wanafunzi kuhusu njia za ufundishaji wa ufahamu ............................ 56

**Kielelezo 4.2:** Vigezo vinavyotinga uteuzi na matumizi ya mbinu darasani................................ 58

**Kielelezo 4.3:** Athari za matumizi ya mbinu zisizo mwafaka ..................................................... 59

**Kielelezo 4.4:** Vigezo vinavyotinga uteuzi na matumizi ya nyenzo darasani .............................. 68

**Kielelezo 4.5:** Mahudhurio ya warsha na semina ......................................................................... 72

**Kielelezo 4.6:** Mapendekezo ya Walimu ..................................................................................... 86

**Kielelezo 4.7:** Mapendekezo ya Wanafunzi ................................................................................. 87

## ORODHA YA MAJEDWALI.

**Jedwali 1.1:** Ripoti ya Utendaji wa Wanafunzi katika somo la Kiswahili, Mtihani wa KCSE wa 2015-2014 unaosahihishwa juu ya alama 100 .......... 6

**Jedwali 4.1:** Matumizi ya Mbinu za Kufundishia (mwitiko wa walimu) .......... 52

**Jedwali 4.2:** Mara-idadi ya Matumizi ya Mbinu za Kufundishia (mwitiko wa walimu) .......... 54

**Jedwali 4.3:** Mara-idadi ya Matumizi ya Mbinu za Kufundishia (mwitiko wa wanafunzi) .......... 55

**Jedwali 4.4:** Uwepo wa nyenzo za kufundishia .......... 62

**Jedwali 4.5:** Idadi ya vitabu kwa idadi ya wanafunzi .......... 64

**Jedwali 4.6:** Utoshelevu wa vitabu vya kiada .......... 65

**Jedwali 4.7:** Mara-idadi ya matumizi ya nyenzo .......... 67

**Jedwali 4.8:** Makadirio ya Ushauri wa Maafisa Wadhibiti Ubora na Viwango wa Elimu. .......... 73

**Jedwali 4.9:** Matumizi ya stakabadhi za kujifunza na kufundishia .......... 74

**Jedwali 4.10:** Maoni ya Walimu .......... 76

**Jedwali 4.11:** Maoni ya Wanafunzi .......... 77

**Jedwali 4.12:** Maoni ya Walimu .......... 77

**Jedwali 4.13:** Maoni ya Wanafunzi .......... 79

**Jedwali 4.14:** Maoni Kuhusu Ufahamu kwa Jumla .......... 81

**Jedwali 4.15:** Maoni ya Walimu .......... 84

**Jedwali 4.16:** Maoni ya Wanafunzi .......... 85

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Utafiti

Kembo-Sure (1996) anasema kuwa, kulikuwa na mabadiliko makuu katika sekta ya elimu ya Kenya, Kiswahili kilipopewa hadhi kwa kuteuliwa kuwa somo la lazima darasani na hata katika mitihani na Tume ya Mackay (1981). Hii inatokana na Kiswahili kutambuliwa kuwa na uzito sawa kama Kiingereza katika kuendesha masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Katiba mpya ya Kenya iliyozinduliwa mwaka 2010 iliikweza nafasi ya lugha ya Kiswahili zaidi kwa kuitambua kama lugha rasmi. Kiswahili sasa ni lugha ya taifa la Kenya na lugha rasmi ambayo inatumika pamoja na Kiingereza katika mawasiliano ya kibiashara, kiutawala na katika hali ya kisiasa. Hii inaonyesha umuhimu wa Kiswahili katika taifa letu la Kenya. Kwa hivyo, Kiswahili ni chombo muhimu katika mawasiliano miongoni mwa jamii. Mathalani, asilimia themanini ya watu nchini Kenya huitumia lugha hii katika mawasiliano yao ya kila siku. Uwiano huu umetambuliwa na shirika la Kimataifa (Momanyi, 2007).

Kiswahili kinapiku lugha ya Kiingereza na lugha nyingine za kienyeji katika kutimiza malengo ya kitaifa kiuchumi, kisiasa na kijamii (Shitemi & Mwanakombo, 2001). Sababu ni kuwa kimatumizi, Kiswahili hukiuka mipaka ya kikabila, na matabaka kiuchumi na kielimu. Kiswahili huwawezesha Wakenya wengi kushiriki katika masuala ya maendeleo katika jamii. Ni kwa mintarafu hii, ndipo Kiswahili kimepewa umbele kama somo katika shule za msingi, upili na vyuo. Shuleni, Kiswahili ni somo la lazima. Kinafundishwa na kutahiniwa katika shule za upili nchini Kenya sambamba na masomo mengine ya lazima ambayo ni Kiingereza na Hisabati. Umuhimu wa somo hili unashadidiwa na mahitaji kuwa ili mwanafunzi aweze kujiunga katika

masomo ya chuo kikuu, lazima awe amepata alama ya C+ katika Kiswahili. Maswali ya ufahamu yamekuwako tangu somo la Kiswahili lilipofanywa kuwa somo la lazima katika shule za Sekondari na hata za msingi. Hivyo basi, matokeo duni katika somo la ufahamu huathiri gredi ya Kiswahili na hatimaye, gredi ya jumla katika mitihani.

Ufahamu ni dhana inayorejelea kujua na kulielewa jambo kwa usahihi na kuweza kulieleza upya kwa usahihi bila kupoteza maana yake ya msingi (Wamitila, 2004). Ufahamu wa watu huweza kupimwa katika kusikiliza jambo au katika kusoma jambo. Kuna aina mbili za ufahamu ambazo ni ufahamu wa kusikiliza na ufahamu wa kusoma. Utafiti wetu ulishughulikia ufahamu wa kusoma katika kidato cha tatu kwenye shule za upili za Kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi.Aina ya ufahamu unaotumika katika shule za upili ni ule wa kusoma kwa makini. Huu ni usomaji wa kimya au kwa sauti ambapo msomaji huvuta fikra zake zote kwa kile anachokisoma.

Katika njia hii msomaji huzingatia maana ya kila neno, sentensi na aya kwa makini. Lengo la usomaji wa njia hii ni kupata uelewaji kamili na wa ndani. Kulingana na Silabasi ya Shule za Sekondari ya K.I.E (2006), ufahamu wa kusoma ni zaidi ya kusikiliza tu kile kilichosemwa, badala yake ni uwezo wa mtu kuelewa maana ya maneno anayoyasoma na kuweza kuhusiana nayo kwa namna fulani. Kwa mfano mwanafunzi anaposikiliza hadithi, ufahamu mzuri humsaidia kuielewa hadithi hiyo, kuikumbuka, kujadili na hata kusimulia tena kwa maneno yake mwenyewe.

Gekombe (2015) anadokeza kuwa, somo la ufahamu lina umuhimu katika kustawisha msamiati na kukuza uelewa wa mambo mbalimbali, kuimarisha usomaji wa kasi kwa kuzingatia kaida zifaazo za usomaji kwa mfano kutoelekeza kidole katika maandishi, kutopanuapanua midomo, kutotikisa kichwa wakati wa kusoma, kuboresha sarufi na uwezo wa kujenga hoja, kuchochea ari za wanafunzi, kujisomea na kuwaburudisha

wanaposoma ufahamu, kuchuja ujumbe na kufahamu maana ya maneno kupitia muktadha badala ya kutumia kamusi na kuwasaidia wanafunzi kujibu maswali, hali ambayo huwasaidia wanapokabiliana na maisha ya kila siku, huwasaidia wanafunzi kujifunza uakifishaji.

K.I.E. (2006) inasema kuwa usomaji wa ufahamu hufunzwa shuleni ili kuafikia shabaha kadha. Kwanza ni kuwapa wanafunzi uwezo wa kusoma taarifa kimya na kuyabainisha mawazo muhimu. Pili, kuwawezesha wanafunzi kujibu maswali kwa usahihi. Shabaha hizi huwapa wanafunzi uwezo wa kufanya vizuri katika ufahamu na kwenye vipengele vingine vya lugha kama vile sarufi na fasihi. Uwezo huu hurahisisha mawasiliano kwenye mahala pa kazi. Isitoshe, mbali na kutoa burudani kwa wanafunzi, ufahamu hubeba maudhui ya masuala ibuka yanayoathiri jamii ya kisasa na hivyo humpa mwanafunzi fursa ya kuyafahamu na kutambua njia za kukabiliana nayo katika maisha halisi ya jamii.

Masuala haya ni kama vile mazingira, magonjwa sugu, ubaguzi, imani mpya, ugaidi, mihadarati miongoni mwa mengine (Wasike, 2015). Masuala kadhaa huweza kuathiri ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu wa kusoma. Njogu (2011) anasema kuwa, kuna vipengele viwili vinavyounda mchakato wa ufahamu wa kusoma, uelewa wa msamiati na uelewa wa matini. Ili kuelewa habari ni lazima msomaji awe na uwezo wa kuelewa msamiati uliotumika katika matini hiyo. Endapo maneno yaliyotumika hayataeleweka vilevile matini yote hayataeleweka.

Mazingira pia huathiri mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa Ufahamu. Silabasi ya Shule za Sekondari K.I.E. (2002) inashauri kuwa, ufunzaji wa Kiswahili ufanywe katika mazingira yatakayomwezesha mwanafunzi kupitisha na kupokea ujumbe anapotagusana na wenzake. Kwa hivyo, mwanafunzi anapaswa kutumia lugha

anayojifunza kueleza, hisia, maoni, matamanio na tajriba yake. Usomaji huhitaji muda na utulivu katika mawazo na mazingira yanayomzunguka mwanafunzi. Kwa mfano, mwanafunzi akipewa kazi ya kujibu maswali, atalazimika kusoma kimya kimya kwa makini kurasa hadi kurasa. Atachunguza yaliyomo katika sentensi hadi sentensi akichagua yale ya msingi anayohitaji. Wakati mwingine atachunguza pia maneno na jinsi yalivyotumika katika habari hiyo.

Mbinu, mikakati na nyenzo zinazotumiwa kufundisha ufahamu zinafaa kumwezesha mwanafunzi kutimiza malengo kadhaa (Musau & Chacha, 2001). Haya ni kama vile kusoma maneno kutoka kushoto hadi kulia, kuelewa maana ya juu juu na ya ndani ya matini, kuimarisha kusoma kwa kasi, kuelewa maana ya mada bila kujaribu kuelewa kila neno, kuelewa neno kimuktadha, kuelewa vizuri miundo ya kimsingi ya kisarufi na matumizi yake katika sentensi, kuelewa mtindo na mshikamano wa makala inavyofululiza kutoka mwanzo hadi mwisho, kuelewa na kutathmini yaliyosomwa kwa kutoa maoni yanayofungamana na tajriba.

Baadhi ya tafiti ambazo zimewahi kufanywa kuhusu kitengo cha ufundishaji na ufunzaji wa Kiswahili kwa jumla zimeonyesha kuwa walimu wamekuwa wakiwafundisha wanafunzi kwa mbinu, mikakati na nyenzo za kuwatayarisha ili kuweza kupita mtihani wa kitaifa wa Kiswahili. Githinji (2017) anasema kuwa, walimu wanazingatia zaidi vitabu vya kiada, ubao na mbinu zisizowashirikisha wanafunzi katika ujifunzaji kama vile ya mhadhara. Changamoto au mambo mengine yanayoathiri ufundishaji na ufunzaji wa Kiswahili ni kama vile uhaba wa vifaa, maandalizi mabaya ya walimu, uhaba wa walimu, mielekeo hasi ya walimu na wanafunzi kuhusu vipengee fulani katika somo la Kiswahili. Matokeo haya yanaonyesha kuwa somo la Kiswahili katika shule za upili nchini Kenya umekuwa

haupewi uzito unaostahili. Hali hiyo huweza kujenga mazingira hasi katika ufunzaji na ujifunzaji wa ufahamu.

Kwa miaka kadhaa (2012-2015), matokeo ya Kiswahili katika mitihani ya KCSE ,miigo, mwisho wa mihula yamekuwa yakidorora. Hii ni kinyume na matarajio ya silabasi ya Kiswahili kwa shule za msingi na upili ambapo kufikia mwisho wa mafunzo, kila mwanafunzi hutarajiwa kuwa na umilisi wa kusikiliza na kuelewa; kujieleza vizuri na kwa mantiki katika maandishi na mazungumzo; kusoma na kuelewa kuwasiliana vyema (Musau na Chacha, 2001.)

**Jedwali 1.1: Ripoti ya Utendaji wa Wanafunzi katika Somo la Kiswahili, Mtihani wa KCSE wa 2015-2014 Unaosahihishwa juu ya Alama 100**

| **Shule** | **2015** | **2014** | |
|---|---|---|---|
| Shule ya Upili ya A1 | 11.263 | 10.826 | B+ |
| Shule ya Upili ya B2 | 9.1043 | 8.177 | B |
| Shule ya Upili ya C3 | 7.0714 | 8.1279 | B- |
| Shule ya Upili ya D4 | 7.7857 | 7.5566 | B- |
| Shule ya Upili ya E5 | 5.57 | 7.5 | C+ |
| Shule ya Upili ya F6 | 8 | 7.3424 | B- |
| Shule ya Upili ya G7 | 6.91 | | C+ |
| Shule ya Upil ya H8 | 6.7 | 6.9 | C |
| Shule ya Upili ya I 9 | 4.3421 | 4.4375 | C |
| Shule ya Upili ya J10 | 6.566 | 6.413 | C |
| Shule ya Upili ya K11 | 4.54 | 6.1098 | C |
| Shule ya Upili ya L12 | 5.162 | 6.032 | C |
| Shule ya Upili ya M13 | 5.3 | 5.82 | C |
| Shule ya Upili ya N14 | 6.3471 | 5.071 | C |
| Shule ya Upili ya O15 | 5.0384 | 4.3889 | C |
| Shule ya Upili ya P16 | 5.2857 | 5.421 | C- |
| Shule ya Upili ya Q17 | 4.389 | 5.143 | C- |
| Shule ya Upili ya R 18 | 3.56 | | D+ |
| Shule ya Upili ya S19 | 4.03 | 4.53 | C- |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Shule ya Upili ya T20 | 4.648 | 4.395 | C- |
| Shule ya Upili ya U21 | 4.295 | 5 | C- |
| Shule ya Upili ya V22 | 3.8696 | 3.58 | D+ |
| Shule ya Upili ya W23 | 5.44 | 2.76 | C- |
| Shule ya Upili ya X24 | 3.954 | 3.967 | D+ |
| Shule ya Upili ya Y25 | 3.8696 | 3.875 | D+ |
| Shule ya Upili ya Z26 | 3.04 | 2.76 | D+ |
| Shule ya Upili ya Z27 | 6.23 | 3.967 | D+ |
| Shule ya Upili ya Z28 | 4.8125 | 3.875 | D+ |
| Shule ya Upili ya A29 | 5.894 | 2.92 | D+ |
| Shule ya Upili ya B30 | 3.5667 | 3.52 | D+ |
| Shule ya Upili ya C31 | 2.357 | 3.4 | D |
| Shule ya Upili ya D32 | 2.916 | 2.1905 | D |
| Shule ya Upili ya E33 | 4.0545 | | |
| Shule ya Upili ya F34 | 4.176 | | |
| Shule ya Upili ya G35 | 3.2 | | |

**Chanzo: (Ripoti ya KNEC 2015-2014: Mtihani wa KCSE )**

Kutokana na matokeo katika jedwali 1.2, mtafiti anahusisha matokeo duni katika Kiswahili kwenye mtihani wa KCSE na Matokeo duni katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi ambayo yamekuwa ya kiwango cha chini kwa muda mrefu.

Ripoti ya KNEC (2015) inashauri kuwa walimu wanafaa kutafuta suluhisho la kudumu kuhusu matokeo duni ya Kiswahili, hususan sehemu ya Ufahamu. Ni kwa

mizani hii ndipo mtafiti aliazimia kutafiti kuhusu mambo ambayo yanachangia matokeo duni kwenye ufahamu katika Kiswahili kwani, ufahamu huunga karatasi ya pili ya somo la Kiswahili kwa alama 15 kati ya 80. Sehemu hii isipofanywa vyema, huchangia matokeo duni katika karatasi ya pili. Viwango vya utendaji katika Kiswahili pia vimezidi kudorora katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi kulingana na ushahidi wa matokeo kwenye ripoti za Ofisi za Elimu katika eneo hili. Hali hii ni ya kusikitisha ikizingatiwa kuwa Kiswahili ni lugha muhimu sana nchini Kenya (Ogutu, 2005).

**1.2 Suala la Utafiti**

Lugha ya Kiswahili ina nafasi muhimu kikatiba nchini Kenya (Katiba ya Kenya, 2010). Licha ya kuwa lugha ya taifa, hivi sasa ni lugha rasmi inayotumiwa katika shughuli za kielimu, kibiashara, kisiasa na kiuchumi. Somo la Kiswahili ni la lazima katika shule za msingi na upili nchini Kenya. Mabadiliko katika mtaala wa elimu nchini Kenya yamefanya Kiswahili kuwa mojawapo ya masomo ambayo mwanafunzi anafaa kupata alama ya C+ katika mtihani wa KCSE ndipo ajiunge na masomo ya ngazi za juu. Kwa hivyo, wanafunzi wasioweza kupata alama ya C+ katika Kiswahili huathiri nafasi zao za kujiunga na viwango vya juu kimasomo. Matokeo ya wanafunzi katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi hayajakuwa ya kuridhisha kwa muda wa miaka miwili iliyopita; 2014 hadi 2015. Jedwali 1.1 linaonyesha kuwa wanafunzi wengi katika eneo hili wamepata matokeo yaliyo chini ya wastani.

Maswali ya ufahamu yamekuwapo tangu utahini wa Kiswahili kama somo katika shule za upili nchini Kenya. Licha ya hali hii, matokeo katika sehemu hii yamekuwa dhaifu (KNEC, 2015). Udhaifu huu huathiri alama ya jumla ya mwanafunzi katika mtihani wa KCSE na hivyo kuathiri nafasi yake ya kujiunga na elimu ya kiwango cha

juu.Vile vile ,mtafiti hajakumbana na utafiti wowote ambao ulifanywa katika kaunti ndogo ya Kisumu magharibi ili kuchunguza kuhusu mambo yanayoathiri ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu ambalo limekumbwa na matatizo mengi katika eneo hilo. Hivyo basi, utafiti huu ulinuia kubainisha mambo yanayoathiri utendaji katika ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Kusudi la utafiti huu lilikuwa kuchunguza mambo yanayoathiri walimu na wanafunzi katika ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu katika shule za upili za kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi. Ili kutimiza azma hii, utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo:

a) Kuchunguza mbinu zinazotumiwa katika ufundishaji wa somo la ufahamu katika shule za upili
b) Kutathmini matumizi ya nyenzo za kufundishia somo la ufahamu katika shule za upili
c) Kuchunguza maandalizi ya walimu kuhusu ufundishaji wa somo la ufahamu katika shule za upili
d) Kutathmini maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu somo la ufahamu katika shule za upili.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

e) Je, ni mbinu gani zinazotumiwa na walimu kufundishia somo la ufahamu katika shule za upili?
f) Ni nyenzo gani hutumiwa na walimu kufundishia somo la ufahamu katika shule za upili?

g) Walimu hujiandaa vipi kuhusu ufundishaji wa somo la ufahamu katika shule za upili?

h) Ni nini maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu katika shule za upili.

## 1.5 Misingi ya Uteuzi wa Mada ya Utafiti

Msukumo wa kufanya utafiti huu ulitokana na sababu kadhaa. Kwanza, licha ya matokeo duni katika somo la Kiswahili, tafiti nyingi zilizofanywa katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi ziliegemea sana vipengele vingine vya lugha kama vile fasihi, ushairi, mbinu za kufundishia somo la Kiswahili kwa jumla na isimujamii. Pili, ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu umekumbwa na changamoto kama inavyodhihirika katika ripoti ya KNEC (2015). Sehemu ya ufahamu ndiyo inayochangia matokeo duni katika Kiswahili. Sababu ni kuwa, wanafunzi wana udhaifu katika kujibu maswali ya ufahamu kwani mara nyingi wanafunzi wengine huamua kutoishughulikia sehemu ya ufahamu kwa kuiruka. Ni kutokana na masuala haya ndipo mtafiti alipopata mshawasha wa kuchunguza na kubainisha mambo yanayoathiri ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu katika Kiswahili na kupendekeza njia za utatuzi.

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yatawazindua wapanga mitaala na walimu kutathmini upya mbinu na mikakati katika kusahihisha kuelewa kwa wanafunzi wanapojifunza ufahamu katika Kiswahili.Hali kadhalika,matokeo ya utafiti huu yatakuwa msingi bora kwa kutoa maelekezo kuhusu jinsi ya kuimarisha ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu katika eneo la utafiti. Wanaweza pia kuyatumia matokeo ya utafiti huu katika kupanga na kuratibu mitaala kuhusiana na ufahamu katika somo la Kiswahili.

Maafisa Wadhibiti Ubora wa Elimu na Viwango wanaweza kunufaika na matokeo ya utafiti huu kwani, wanaweza kuyatumia kuandaa semina, warsha na simposia kwa nia ya kushamirisha utendaji kazi wa walimu wa Kiswahili katika ufundishaji wa ufahamu. Utafiti huu vile vile utawaimarisha walimu kuhusu mbinu za kufundishia somo la ufahamu kwani wataweza kuelewa na kutumia mbinu bora za kufundishia somo la ufahamu.Wanafunzi nao watapata msingi bora wa kusoma na kuyajibu maswali ya ufahamu.

Utafiti huu ulichunguza na kufafanua mambo yanayoathiri ufundishaji wa ufahamu katika Kiswahili. Matokeo na mapendekezo yatakayotolewa yakizingatiwa, yatawawezesha walimu na wanafunzi kupenda ufunzaji na ujifunzaji wa ufahamu darasani na hata kulikabili somo la ufahamu kwa njia inayostahili. Mtafiti anataraji kuwa, matokeo ya utafiti huu yatachangia katika elimu ya Kiswahili kwa kuwawezesha walimu na wanafunzi kujua namna ya kulikabili somo la ufahamu, kuwakumbusha walimu kuhusu mikakati muhimu ya kufundisha jinsi ya kusoma na kuyajibu maswali ya ufahamu ipasavyo. Hali kadhalika, utafiti huu utakuwa msingi bora wa kutoa mapendekezo kuhusu jinsi ya kuimarisha hali ya somo la ufahamu katika eneo la utafiti.

## 1.7 Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Utabia iliyoasisiwa na mwanasaikolojia Hull (1943) na kuimarishwa na Skinner (1957). Hull alianzisha nadharia hii akiwa na madhumuni ya kuelekeza ujifunzaji wa lugha. Nadharia ya Hull ilisisitiza sana mambo ya kukariri na kurudiarudia, kwa ufundishaji wa somo la ufahamu. Ilishikilia kwamba wanafunzi humtegemea sana mwalimu kuuenzi ufahamu. Skinner (1957) aliimarisha nadharia hii kwa kuongezea kuwa, upataji na mabadiliko ya uwezo wa

tabia unatokana na michakato ya ujifunzaji na mazoea ya taaluma katika mazingira mahsusi. Mabadiliko haya hutokea kutokana na mazoezi yanayoimarishwa (Kimble, 1961). Kwayo, uwezo na tabia ya kiumbe hudumishwa kwa misingi ya kutosheleza mahitaji yake. Viumbe hujifunza kuwa na tabia ya aina fulani kwa sababu ya kuwa na kitu kinachoridhisha au matokeo ridhishi yanayotarajiwa kutokana na tabia hiyo (Skinner, 1957). Kwake Skinner, matarajio ya kupata matokeo chanya katika somo humtia mwanafunzi hamasa ya kufaulu. Walimu wakichukulia kuwa hawatapata matokeo yatakayowaridhisha baada ya somo, hawafanyi bidii hivyo hufeli kulifikia lengo lao la somo. Mwalimu aliyebobea katika tajriba ya ufundishaji hutumia mbinu na vifaa mbalimbali kuwaelekeza wanafunzi wake somoni ili wajifunze vilivyo (Orodho, 1996). Hata hivyo, nadharia hii humfanya mwanafunzi kukosa ubunifu katika masomo hivyo basi yafaa itumike pamoja na nadharia zingine kuleta mafanikio ya maana.

Nadharia hii imepokea mabadiliko mbali mbali na maoni ya hivi karibuni zaidi ni yale ya Deodutus (2015) ambaye ana maelezo sambamba na yale ya Hull (1943), Skinner (1957) ambayo yanasema kuwa, kujifunza ni tukio la uhusiano wa matukio, mwitiko na kichocheo katika mazingira na uimarisho chanya au uimarisho hasi. Uimarisho chanya huhamasisha mwendelezo wa mwitiko wakati uimarisho hasi hufifisha au kuzuia mwitiko usiendelee. Katika nadharia hii, ujifunzaji wowote wa somo la ufahamu ulionekana kama uamiliaji wa tabia mpya. Nadharia hii inatambua nafasi ya mazingira katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha.Vilevile, Deodutus alizingatia kuwa, mazingira yanatumika kwa maana pana zaidi kwa kuhusisha masuala ya ujifunzaji wa somo darasani.

Hali kadhalika, ujifunzaji wa somo la ufahamu ni sawa na ujifunzaji mwingine wowote kutokana na kufanya mazoezi ya hiyo tabia mpya na kutoa marejesho sahihi. Kulingana na nadharia hii, uimarisho chanya na ingizo sahihi na pakiwa na ukosoaji wa kile ambacho si sahihi, huwezesha mchakato wa ujifunzaji kufanikisha vitu vya msingi kuzingatia katika mchakato wa ujifunzaji wa lugha pamoja na tabia lengwa pamoja na ushiriki wa mwanafunzi. Kwa hivyo basi tutaelekezwa zaidi na mchango wa nadharia ya utabia kulingana na maelezo ya Deodutus katika data yetu, hasa tunapozingatia matumizi ya mhimili wa kwanza wa nadharia ya utabia unaosema kuwa kukariri na kurudiarudia matamshi mazuri ya vipengele vya mazungumzo, miundo ya sentensi na drili za aina mbalimbali. Madhumuni ya kukariri na kurudia yalikuwa ni kujaribu kujenga tabia ya inayofaa kuhusu somo la ufahamu na iliyo sahihi, tabia au lugha isiyo na makosa kwani makosa yalionekana kama kikwazo cha kujenga tabia nzuri. Kulingana na Deodutus, Nadharia hii ina umuhimu ufuatao, Mwalimu ataweza kuwapatia wanafunzi mazoezi mwafaka, na wakati mwingine mazoezi hayo yataweza kurudiwa rudiwa ili mwanafunzi aweze kuimarika katika somo la ufahamu. Mwisho kabisa, mwalimu ataweza kufundisha kwa kuzingatia mazingira bora darasani.

Kulingana na Thorndike (1927), Skinner (1957), Moffet na Wegner (1992) na Musau na Chacha (2001), mihimili muhimu ya nadharia ya ufundishaji ya utabia ni kama ifuatavyo:

1. Mwalimu afaa kuanza kulifundisha suala jipya kwa kukariri na kurudiarudia matamshi ya vipengele muhimu vya ufahamu ili kuwawezesha kuelewa muundo wa msamiati na matumizi maalum ya lugha katika ufahamu.

2. Mwalimu amwelekeze mwanafunzi vyema ili kutorudia makosa. Kutorudia huko kutaathiri ufundishaji na ujifunzaji wao pakubwa. Makosa ni kikwazo cha kujifunza lugha ya pili (jinsi ya kusoma na kujibu maswali ya ufahamu). Makosa yapaswa kukatizwa na kuadhibiwa ili yasirudiwe tena. Makosa haya ni kama athari za lugha mama.
3 Kuandika kuje baada ya kusoma (kukariri na kuzungumza). Sababu ni kuwa wanafunzi watakuwa wameelewa matumizi maalum ya lugha katika somo na kupata uzoefu tosha.
4 Kuwa miundo na sarufi ifundishwe baadaye pamoja na uchanganuzi wa vipengele vya lugha. Hivi watawezeshwa kung'amua kanuni na mielekeo katika ufahamu kwa njia ya kukisia na mazoezi ya mara kwa mara.
5 Kuwa jukumu la mwalimu ni muhimu sana nalo ni kuongoza kila tukio darasani; kuwaelekeza wanafunzi kwa kutayarisha mazingira, kuteua mada inayofaa, kuandaa nyenzo za kufundishia. Jukumu la mwanafunzi ni kufuata maagizo. Hii ni safari ambayo mwalimu ataisafiri pamoja na wanafunzi wake. Nadharia ya utabia ni pana mno. Inawezekana kuwa hatujaeleza vipengele vyake vyote.

Katika somo la kipengele cha ufahamu kwa jumla, wanafunzi wengi wamekiogopa kwa imani kuwa ni mgumu kueleweka, jambo ambalo limetafitiwa katika utafiti huu ili kupata mwanzo na ukweli wake. Utafiti huu unahusu masuala yanayoathiri ufundishaji wa somo la ufahamu katika shule za upili. Watafitiwa katika utafiti huu walikuwa walimu wa Kiswahili ambapo mtafiti alikadiria uwezo na tabia za ufundishaji ufahamu na jinsi wanavyodumisha hamasa zao na za wanafunzi wao katika somo hili. Kwayo, tabia ya walimu huhusishwa na hali ya mazingira ya

ufundishaji kwa mkabala wa matokeo yake. Mazingira mema husababisha ufundishaji bora na mabaya yakisababisha matokeo mabovu kulingana na nadharia hii.

Nadharia ya utabia inalenga kueleza namna tabia inavyojengeka. Hull (1943) na wenzake wanaamini kuwa tabia hutokana na mtagusano wa mara kwa mara wa viumbe na mazingira yao. Mazingira ya wanafunzi katika ufundishaji wa ufahamu wa Kusoma huwa darasa, jamii, nyenzo na hata mwalimu. Nadharia ya utabia inawalenga walimu wa somo la ufahamu kutumia mbinu bora za ufundishaji pamoja na nyenzo wakishirikiana na wanafunzi wao ili kusababisha ukuruba mwema kati yao na hatimaye utendaji bora kwa wote (Rodgers, 1976 na Dewey, 1916).

Kando na walimu wa ufahamu kuwa na umilisi wa somo la Kiswahili, wanahitaji kuchochewa na matokeo mema kwa upande wa wanafunzi katika ufundishafji wao. Anavyosema Schultz na Schultz (1987), haja ya walimu wa ufahamu kutaka wanafunzi wajifunze vyema huibua msukumo unaowapa ufanisi huo. Kwa hivyo, walimu wa ufahamu wa Kiswahili yafaa waweze kubainisha viwango vya wanafunzi ili kuandaa mbinu na kupanga mikakati wanayoitumia kufunza ili kufikia malengo yao katika ufundishaji wa ufahamu wa Kiswahili. Mwalimu ashauriwa kuteua makala ya ufahamu ambayo yanavutia wanafunzi zaidi. (Wanjala & Kavoi, 2013).

Tabia inayoigwa huhitaji kufanyiwa mazoezi ili kuimarika na kudumishwa. Nadharia ya utabia ina azma ya kuwahimiza walimu wa somo la ufahamu kuteua na kutumia mbinu zilizo bora wanapofundisha. Hii ni changamoto itakayofanya walimu wengi kuuthamini ufahamu kwa kutaka kuufundisha na kuhakikisha kuwa wanafunzi wana utendaji bora katika shule za upili. Musau na Chacha (2001) wanasema kuwa tabia isiyorudiwarudiwa kwa njia ya mazoezi hufifia na hata mwishowe hupotea kabisa. Schultz na Schultz (1987) wanakubaliana na kauli hii kwa kusisitiza kuwa ili

tabia fulani idumu yafaa kuigwa, kurudiwarudiwa pamoja na kutuzwa; la sivyo, hufifia na baadaye hupotea kabisa. Nadharia ya utabia yasisitiza mazoezi na utuzaji katika somo lolote hasa ufahamu.

Walimu sawa na wanafunzi, wanatakiwa wafanye mazoezi mengi sana katika somo la ufahamu ili kuboresha utendaji wao kama walimu na wanafunzi mtawalia. Hili lilichukuliwa na mtafiti kuwa jambo ambalo lilifanywa kwa nadra sana shuleni na pengine kuchangia utendaji mbaya. Walimu wa ufahamu wanahimizwa watumie mbinu zinazomhusisha mwanafunzi kama vile, ziara nyanjani kwa njia ya uchunzaji na usaili, kazi mradi, majadiliano na makundi darasani ili kunata hamu na uhusika wa wanafunzi katika somo la ufahamu. Kwa njia hii, wanafunzi hung'amua kuwa hawajifunzi ufahamu kwa ajili ya kupita mtihani tu bali kuwawezesha kukua katika taaluma pamoja na kupata maadili muhimu maishani, sababu ni kuwa ufahamu husheheni masuala muhimu na nyeti yanayoizunguka na kuiathiri jamii.

Usomaji wa ufahamu kwa hivyo utawaanda vyema kuyakabili masuala katika maisha halisi. Hivyo basi, mbinu shirikishi anuai kama kusimulia hadithi, maigizo na makundi zinapotumiwa vyema na mwalimu wa ufahamu, ufundishaji humchochea mwanafunzi kuvutiwa na ufahamu na hivyo kutilia mkazo ili kuimarishja utendaji wake somoni. Nadharia ya utabia inamhimiza mwalimu kuteua mbinu na njia zinazolifanya somo kuwa rahisi kueleweka na liwe la kupendeza.

Matumizi ya nyenzo za ufundishaji katika ufahamu ni shughuli ambayo imependekezwa na wanasaikolojia wengi wa elimu. Nyenzo huwawezesha walimu kudhibiti hali, mihemko na uelewa wa wanafunzi wao (Nsubuga, 2000). Hali hii husababisha mielekeo chanya dhidi ya kipengele cha ufahamu ambapo wanafunzi huendeleza stadi hii kwa kuifanyia mazoezi zaidi kibinafsi na ndivyo nadharia ya

utabia inavyohimiza katika matumizi yake. Nadharia hii inasisitiza kuwa nyenzo hunata katika nadhari ya mwanafunzi na humwezesha kuwa na kumbukumbu ya yale aliyoyashughulikia katika somo la ufahamu kwa muda mrefu.

Nadharia ya utabia inapendekeza walimu wahakikishe kuwa kuna vitabu vya marejeleo na kiada wanapofundisha ufahamu.Vitabu hivi hufaa sana katika shughuli za kufanya mazoezi ili kuimarisha stadi za somo la ufahamu kwa jumla (Thorndike, 1927; Skinner 1957 na Moffet & Wegner, 1992). Mbunda, (1976) analiunga mkono suala hili kuwa, uwepo wa vitabu vya kiada katika vidato vya tatu na nne unawapa wanafunzi muda wa kutosha kujiandaa kwa mitihani. Ili mwalimu wa somo la ufahamu afaulu katika majukumu haya, lazima awe na umilisi wa kutosha na hamu ya kufaulu kuwaongoza wanafunzi wake pia wafaulu. Wamitila (2004) anapendekeza ufundishaji wa ufahamu ufanywe kwa kumruhusu mwanafunzi kusoma ufahamu kwa mara ya kwanza ili kupata picha ya kinachozungumziwa. Baada ya kusoma, mwanafunzi asome maswali kisha kusoma ufahamu kwa mara ya pili akinukuu sehemu muhimu zenye majibu. Baada ya kufanya hivi, mwanafunzi yu tayari kuyajibu maswali. Isitoshe, mwalimu anafaa kuwauliza wanafunzi maswali ya kujibiwa kwa kuzungumza au kuandika (Ndalu, 2008). Majibu ya maswali haya yanafaa kusahihishwa. Ndalu (2008) na Wamitila (2004) wanasema kuwa mafunzo bila mazoezi si mafunzo tena na mazoezi ambayo hayajasahihishwa hayana faida kubwa kwa waliyoyafanya. Utafiti huu ulinuia kuchunguza iwapo hatua hizi huzingatiwa na walimu na wanafunzi wakati wa somo la ufahamu.

Kwa muhtasari, nadharia ya Utabia humwezesha mwalimu kuchunguza ukuaji na uimarikaji wa tabia ya wanafunzi kutokana na mazoezi maridhawa wanayopewa kuishughulikia katika ufahamu kutokana na aina ya mbinu na nyenzo wanazozitumia

kufundishia somo la ufahamu. Walimu huchunguza mabadiliko yanayotokea katika mielekeo, umilisi wa ufahamu na jinsi mbinu na nyenzo zinazotumiwa huondoa utata wa vipengele katika somo la ufahamu.

**1.8 Upeo na Mipaka ya Utafiti**

Utafiti huu ulijikita katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi na matokeo yake yatawakilisha masuala yanayoadhiri ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu katika shule zote za umma nchini Kenya. Watafitiwa walikuwa walimu wa Kiswahili na wanafunzi wa kidato cha tatu na sio madarasa mengine.

Utafiti ulijikita tu katika shule za upili za eneo la kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi. Ingawa kuna vipengee vingi vya kutafitiwa katika somo la Kiswahili, utafiti huu ulijishughulisha tu na ufahamu na haukushughulikia vipengele vingine vya somo la Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yatachukuliwa kama vidokezo na sio kauli ya mwisho. Kwa vile masuala ya lugha hubadilika kila uchao, utafiti zaidi utahitajika baadaye kutathmini ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu. Isitoshe, upeo wa uchunguzi huu ulilenga wanafunzi wa kidato cha tatu tu ambapo si hakika kwamba maoni yaliyotolewa ni sawa katika vidato vingine

**1.9. Hitimisho**

Sursa hii imeshughulikia usuli wa suala la utafiti ,malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, nadharia ya utafiti na hatimaye mipaka ya utafiti. Sura itakayofuata itashughulikia uhakiki wa maandishi.

## 1.10 Maelezo ya Istilahi

**Maudhui** - Haya ni mambo yanayoelezwa au yanayojitokeza katika kazi za fasihi.

Mambo haya hujumuisha dhamira, ujumbe, maadili na falsafa ya mwandishi Msokile (1993).

**Ufahamu** - Ni mojawapo ya kipengele katika silabasi ya somo la Kiswahili

Kinachofunzwa na kutahiniwa katika shule za upili nchini Kenya.

**Ufunzaji** - Hali ya kuandaa mazingira, mada, njia na nyenzo mahsusi ili kuwasilisha maarifa, stadi, mielekeo na maadili kwa namna ambayo itaathiri tabia na hali ya mwanafunzi.

**Ujifunzaji** - Hali ambapo mwanafunzi hukumbana na mazingira na mambo mbalimbali kama vile maarifa kwa njia fulani ambayo huathiri tabia zake.

**Mbinu za kufunza** - Ni utaratibu wa kuwasilisha mada kwa wanafunzi katika somo fulani ulio na sifa teule kama vile mhadhara, makundi, mjadala, maswali na kadhalika.

**Maandalizi ya mwalimu**- Ni mipango na mipangilio yote ambayo mwalimu huweka maanani kabla ya kuwasilisha somo la ufahamu darasani. Inahusu pia maandalizi ya stakabadhi za kitaaluma.

**Nyenzo** - Vifaa vinavyotumiwa kufundishia somo la ufahamu.

**1.11 Maelezo ya Vifupisho**

| | | |
|---|---|---|
| **KCSE** | - | Kenya Certificate of Secondary Education |
| **K.I.E** | - | Kenya Institute of Education |
| **KICD** | - | Kenya Institute of Curriculum Development |
| **KNEC** | - | Kenya National Examination Council |
| **NACOSTI** | - | National Commission for Science and Innovation |
| **WB** | - | Wasichana za Bweni |
| **WVB** | - | Wavulana za Bweni |
| **MK** | - | Mseto kutwa |
| **MB** | - | Mseto Bweni |
| **KK** | - | Kubali kabisa |
| **KU** | - | Kubali |
| **SA** | - | Siwezi amua |
| **SI** | - | Sikubali |
| **SK** | - | Sikubali kabisa |
| **N** | - | North |
| S | - | South |
| **W** | - | West |
| **E** | - | East |
| **NW** | - | North West |
| **NE** | - | North East |
| **SE** | - | South East |
| **SW** | - | South West |

# SURA YA PILI

# UHAKIKI WA MAANDISHI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia uhakiki wa maandishi ambayo yanahusiana na mambo yanayoathiri ufundishaji wa somo la ufahamu. Miongoni mwa maandishi yaliyorejelewa ni yale yanayohusiana na dhana na nafasi ya ufahamu, michakato katika usomaji wa ufahamu, masuala yanayoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu; mbinu na nyenzo za kufundishia ufahamu, maandalizi ya walimu kuhusu ufundishaji wa ufahamu na maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu ufahamu.

## 2.2 Dhana ya Ufahamu

Kwa mujibu wa Wamitila (2004) na Maloba (2008), ufahamu ni tendo au uwezo wa kuelewa kinachosemwa. Pia, ni somo la kumpa msomaji mbinu za uelewaji na kumjaribu kama anaelewa alichokisoma. Ufahamu ni dhana inayorejelea kujua na kulielewa jambo kwa usahihi na kuweza kulieleza upya kwa usahihi bila kupoteza maana yake ya msingi. Ufahamu wa mtu unaweza kupimwa katika kusikiliza jambo au katika kusoma. Mtaala wa elimu nchini Kenya kuhusu ufahamu katika kiwango cha shule za upili hulenga kupima uelewa na uelezaji upya wa alichokisoma mtahiniwa. Huu unaitwa ufahamu wa kusoma. Ufahamu wa kusoma unafafanuliwa na silabasi ya K.I.E. (2006) kama namna ya kuangalia maandishi na kuyasoma, kisha kueleza uliyoyasoma kulingana na mahitaji ya maswali yaliyoulizwa kuhusiana na ufahamu huo.

### 2.3 Masuala Yanayoathiri Ufunzaji na Ujifunzaji wa Somo la Ufahamu

Katika sehemu hii tutashughuikia masuala yanayoathri ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu. Masuala yenyewe ni kama yafutayo; mbinu za kufundishia, matumizi ya nyenzo, maandalizi ya walimu na kutathmini maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu somo la ufahamu.

#### 2.3.1 Mbinu za Kufundishia

Mbinu za kufundishia ni mikakati inayotumika katika shughuli za kielimu kwa madhumuni ya kusaidia katika kutimiza malengo yaliyokusudiwa (Chacha, 2016). Chacha anadai kwamba mbinu za kufundishia ni vigeu muhimu katika ufundishaji wenye kuleta matokeo mema. Ni muhimu kutilia mkazo mbinu za ufundishaji wa ufahamu ndipo usomaji wake uwe na manufaa kwa walengwa. Ufundishaji hudhamiria kuwasaidia watu kujifunza. Sababu kuu ya mwalimu kufunza ni ili mwanafunzi wake apate kuelewa kwa kupata mwelekeo chanya na maarifa yanayofaa kulingana na lengo kuu la somo.

Mbinu zinazotumika katika kufundishia somo la ufahamu sharti ziwe bora na zitakazoleta matokeo mema ili lengo la mwalimu liweze kuafikiwa. Walimu wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali katika shughuli zao za kila siku. Kulingana na Sitanda (1980), Mbuthia (1996) na Chacha (2016), ujifunzaji hutegemea na jinsi mwalimu alivyotayarisha njia za kufundishia. Kuna mambo mengi ambayo sharti azingatie. Miongoni mwayo ni umri wa wanafunzi, yale aliyojifunza mwanafunzi hapo awali, malengo ya somo, mbinu atumiazo zitayakamilisha, na mambo ambayo yatamchochea mwanafunzi ili aweze kutimiza lengo lake. Ili kutimiza haya, mwalimu anahitajika kutumia mbinu zinazomshirikisha mwanafunzi katika ujifunzaji wa ufahamu.

Ndalu (2008) na Miricho (2008) wanasisitiza ya kwamba uteuzi wa njia za kutumia kufundishia darasani ni maandalizi muhimu kwa mwalimu. Wanatoa kauli kuwa, hakuna njia moja ya kufunza iliyo bora kuliko zingine. Mwalimu sharti atumie njia zenye uhitilafiano ndipo aweze kufanikisha shabaha yake. Chacha (2016) naye anapendekeza kuwa, njia mwafaka ya kufundishia ni ile ambayo itavuta hadhira, na itakayowashirikisha wanafunzi na kumfanya aelewe barabara. Njia hizo ni kama vile majadiliano, maigizo, ziara nyanjani, kazi mradi na kadhalika.

Kimani (2015), katika uchunguzi wake wa uhusiano wa mbinu za kufundisha sarufi na umilisi wa mazungumzo ya wanafunzi wa shule za upili, anatupatia miongozo kuhusu umuhimu wa mwalimu kutumia mbinu shirikishi katika kufundisha somo la Kiswahili. Anasema kuwa mwalimu anahitaji kutia juhudi kamili kwa kuzingatia maongezi yake, shughuli zitakazohusisha usikilizaji, usomaji wa maandishi na lugha ambayo wanafunzi wameitumia ndani na nje ya darasa. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wataimarika na hata kupata uwezo wa kutumia lugha kivyao na hata kupata uelewaji bora. Ingawa utafiti wa Kimani ulihusu uchunguzi wa mbinu za ufundishaji, alijikita katika ufundishaji wa sehemu ya sarufi na mazungumzo. Kwa upande mwingine, utafiti huu unahusu uchunguzi wa matumizi ya mbinu za kufundishia katika somo la ufahamu.

Ipara (2006) anasema kuwa mbinu ni ruwaza ya sifa au tabia zinazobainika katika mchakato wa ufunzaji na hutokea kwa mjumuisho au kwa mpangilio fulani. Ni mgawanyo ambao humpa mwanafunzi uwezo wa kujieleza kwani njia hazimhusu mwalimu pekee bali humhusisha mwanafunzi pia. Amefafanua mbinu kuwa njia ambapo walimu huamua namna ambavyo wanafunzi wao watajifunza. Kwa hivyo,

ufunzaji wowote unaomtenga mwanafunzi kwa kutomhusisha katika mchakato wa ujifunzaji si kamili. Huu ni mtazamo wa jumla wa kuendesha somo.

Ufunzaji wa somo la ufahamu lazima ufanywe kwa njia shirikishi zinazompa mwanafunzi ukati katika mchakato wa kujifunza. Aidha haja ya kufundisha ufahamu inabainika. Hii ina maana kuwa njia pia iwe ni ile itakayomchukua mwalimu muda mfupi kuwasilisha dhana anayokusudia na wanafunzi pia waweze kuelewa barabara (Ndalu, 2008; Miricho na wenzake, 2008 na Mirikau, 2008; Kamau, 2015 na Chacha, 2016). Kwa mujibu wa wataalamu hawa, kuna njia nyingi za kufundishia ambazo zinaweza kumshirikisha mwanafunzi. Baadhi ya njia hizo wanazitaja kama majadiliano, uigizaji, makundi, ufaraguzi, na tajriba. Mukwa na Too (2000) wamefafanua njia ya majadiliano kama hali ya utendaji ambapo wanafunzi chini ya usimamizi wa mwalimu hubadilishana mawazo ili kufikia uamuzi na hitimisho kwa pamoja, hata hivyo, njia hii ya kufundishia ina taksiri zake.

Wanasema kuwa si rahisi kutathmini majadiliano kwani yanaweza kuishia kujadili mambo yasiyo na maana ikiwa vikundi vitakuwa na viongozi dhaifu. Mbinu hii pia huchukua muda mrefu kushughulikia mada husika, hali ambayo huwafanya walimu wengi kukimbilia njia ya mhadhara ambayo huchukua muda mfupi kutimiza malengo ya mada. Mbinu ya mhadhara humpa mwalimu umbele badala ya mwanafunzi. Mhadhara humsawiri mwalimu kama mjua yote huku mwanafunzi akibaki kuwa msikilizaji tu badala ya kuwa mtendaji. Musau na Chacha (2001) na Mirikau (2008) wanasema mbinu ya masaili inahusu kuuliza au kuhoji ili kupata ufahamu juu ya jambo mtu au hali. Wametoa umuhimu wa kutumia masaili kwa kufundisha lugha. Wanasema kwamba kuuliza kunaweza kumpa mwanafunzi mrejesho kuhusu wanayoweza na wasioyaweza na kuchangia kwa kiwango kikubwa utendaji wa

mwalimu. Masaili huwafanya wanafunzi wawe makini waanzapo masomo yao kwa vile huwaandaa kujua yaliyomo. Aidha masaili humwezesha mwalimu kujua mambo ambayo wanafunzi wanayafahamu kuhusuiana na ufahamu wa kusoma kabla hujaanza kufunza.

Maswali ya kiwango cha chini humhusisha mwanafunzi wa kiwango cha chini moja kwa moja katika somo. Pia huwapa wanafunzi nafasi ya kuuliza maswali yao wenyewe hali ambayo humwezesha kujiamini. Masaili vile vile humwezesha mwalimu kujitathmini akaweza kutambua ikiwa wanafunzi wamelifahamu somo kutokana na majibu yao. Kuuliza maswali huchangia katika kuzua fikra miongoni mwa wanafunzi na kufanya wafikirie zaidi. Maswali pia humwezesha mwalimu kujua hisia walizonazo wanafunzi kuhusu mada.

Kwa mujibu wa Kamau (2015) na Chacha (2016), mbinu ya makundi ni mbinu ambayo kwayo wanafunzi hugawanywa katika vikundi vidogo vidogo vinavyozingatia shughuli maalum za mafunzo. Kupitia kwa mbinu ya makundi wanafunzi wanaweza kuchangia maarifa, kuzua hoja, kufahamisha tajriba yao na kujenga tabia ya kutegemeana na kuheshimiana. Haya yote huwapa motisha wanafunzi na kuwafanya kufurahia mafunzo ya lugha. Mbinu ya makundi haina urasmi mwingi.

Humshirikisha mwanafunzi na hutumiwa kudhibiti darasa kubwa (Quist, 2000). Vigezo vya kuweka wanafunzi makundini ni kama vile uwezo wao katika stadi fulani, aina ya kazi ya kufanya, mlahaka wao, jinsia moja na umri. Wanafunzi hujifunza kushirikiana kufanya kazi pamoja, kupanga na kutekeleza kazi na kuimarisha uwezo wao wa kuwasiliana. Wanafunzi hukuza uwajibikaji na uongozi. Mwalimu pia

huwezeshwa kugawanya darasa kubwa lisiloweza kufunzwa vizuri kwa madarasa madogo yaliyo na idadi ndogo ya wanafunzi.

Kazi mradi na ziara nyanjani ni mbinu ambazo huwapa wanafunzi fursa ya kujua utaratibu wa kufanya kazi peke yao, kujifunza katika mazingira asili na huleta ukuruba kati ya wanafunzi wafanyapo kazi pamoja (Bennaars na wenzake, 1994; Kimani, 2015 na Chacha, 2016). Ziara nyanjani huwafurahisha wanafunzi kwa kuwatoa katika mazingira ya kila siku ya darasani na kuwapeleka pahali pengine. Taksiri ya mbinu hizi ni kwamba huhitaji muda mwingi na wanafunzi wakiwa nyanjani wakati fulani hupotoshwa na mambo yasiyohusiana na lengo nyanjani.

Mbinu hizi ni muhimu sana kwa ufundishaji wa somo la ufahamu kwa sababu somo huhitaji mbinu shirikishi. Ripoti ya KNEC (2015) inasema kuwa matokeo duni katika karatasi ya pili ya mtihani wa Kiswahili yanawezakuwa yanasababishwa na mbinu zisizo bora za kufundishia. Mawazo haya yanaungwa mkono na Wanyama (2007) anaposema kwamba matumizi ya mwelekeo mseto katika Kiswahili, wepesi wa kueleweka kwa uwasilishaji wa mwalimu na matumizi ya mbinu bora za kufundishia yanahusiana moja kwa moja na matokeo ya wanafunzi katika mtihani. Ripoti ya KNEC (2015) inabainisha kuwa matokeo duni katika sehemu ya ufahamu ni kutokana na ukosefu wa mazoezi ya kutosha katika ufahamu kwa upande wa wanafunzi. Pia walimu hawaangalii makosa ya hijai na sarufi katika majibu ya wanafunzi pamoja na kukosa kusahihisha mazoezi ya wanafunzi. Hivyo basi, inawataka walimu kuwa makini kuhusu mambo haya.

Katika utafiti wa Onyango (2002) kuhusu uchunguzi linganishi wa njia za makundi na uvumbuzi katika kufanikisha ufundishaji wa Kiswahili katika madarasa ya mwanzo katika shule za msingi, ilidhihirika kuwa, utendaji wa wanafunzi katika Kiswahili

uliboreshwa baada ya wanafunzi kufundishwa kwa kutumia njia za makundi na uvumbuzi. Hata hivyo hakukuwa na tofauti kubwa katika utendaji wa wanafunzi wa kikundi dhibiti katika mjarabu wa kwanza na wa pili. Kwa kupitia mawanda ya maarifa, mtafiti alilinganisha athari za kila njia kwa ufundishaji wa Kiswahili na akagundua kuwa njia za uvumbuzi na makundi zinachangiana. Utafiti wa Onyango ulijikita katika ulinganishi wa matumizi ya mbinu mbili pekee katika ufundishaji wa Kiswahili kwa jumla. Utafiti wetu utajikita katika uchunguzi wa mbinu zote zinazotumiwa katika hususan ufundishaji wa somo la ufahamu na sio Kiswahili kwa jumla.

Naye Chacha (2016) alibainisha uhusiano wa mikakati ya ufundishaji wa fasihi ya watoto ya Kiswahili na umilisi wa kusoma katika shule za msingi, Kasarani, kaunti ya Nairobi, Kenya. Alibainisha kuwa umilisi katika stadi ya kusoma uliimarika kulingana na matumizi ya mikakati shirikishi ya kufumdishia. Amebainisha mambo haya kama matumizi ya mbinu na vifaa. Muhimu zaidi, anasema mielekeo ya walimu na wanafunzi pamoja na maandalizi ya walimu kuhusu ufundishaji wa sarufi huathiri ufundishaji na ujifunzaji wa stadi ya kusoma. Utafiti huu unajihusisha na uchunguzi wa mbinu za kufundishia ufahamu tofauti na stadi ya kusoma pamoja na sarufi alizoshughulikia Chacha.

**Jinsi ya Kujibu Maswali ya Ufahamu**

Kusoma na kufahamu ni swali ambalo hupima kiwango cha mwanafunzi cha kuelewa lugha. Katika swali hili, mwanafunzi hupewa makala fulani ayasome na kuonyesha ufahamu wake kwa kujibu maswali. Makala haya yanaweza kuwa ya maandishi ambayo huteuliwa kwa kuzingatia kiwango cha darasa.(Kimani na Nganje 2011).

**Hatua ya Kwanza:** Wanafunzi huhitajika kusoma makala waliyopewa kuanzia mwanzo hadi mwisho kwa makini kwa madhumuniya kupata ujumbe ulioko.

**Hatua ya Pili:** Wanafunzi wasome maswali yote upesi kwa madhumuni ya kutaka kujua ni aina gani ya maswali yaliyoulizwa.

**Hatua ya Tatu:** Wanafunzi huhitajika kulisoma swali kwanza kwa makini.

**Hatua ya Nne:** Wanafunzi huhitajika kuchukua jukumu la kutafuta kwenye makala mahali ambapo swali hilo laweza kuwa limetolewa. Kwa kawaida maswali mazuri ya ufahamu huulizwa kuanzia mwanzo wa makala hayo kuelekea mwisho. Hivyo basi, katika kujibu maswali mwanafunzi atafute jawabu la swali la kwanza kuanzia mwanzo wa habari hiyo.

**Hatua ya Tano:** Mwanafunzi akishapata mahali ambapo swali hilo limetolewa, hutakikana kulisoma swali tena ili afahamu ni nini hasa kilichoulizwa, kisha aangalie tena makala, mahali palipotolewa swali hilo. Kifuatacho ni mwanafunzi kuunda jawabu lake kwa kujiepusha na kunakili maneno moja kwa moja ila kwa kutumia maneno yake mwenyewe.

Mwalimu wa Kiswahili vile vile, itakuwa vyema ikiwa atawaelekeza wanafunzi katika kuyajibu maswali ya ufahamu kulingana na muktadha wa matini yalioandikwa katika ule ufahamu na siyo kulingana na vile mwanafunzi ajuavyo. Kwa mfano kukiwa na msamiati ambao una maana zaidi ya moja, mwanafunzi anatakikana atumie maana ya neno hilo kulingana na jinsi lilivyotumika katika ufahamu aliousoma. (Kimani na Nganje 2008).

### 2.3.2 Nyenzo za Kufundishia Somo la Ufahamu

Nyenzo ni vifaa vinavyotumiwa katika kuendeleza usomaji.K.I.E. (2006) inafafanua nyenzo kama vichokoo vinavyoweza kumsaidia mwalimu kufanikisha ufundishaji wake. Inaelezea ya kwamba nyenzo ni muhimu kwa kumsaidia mwalimu kurahisisha uwasilishaji wa darasani na katika kutia msisitizo kwa yale yanayofundishwa. Eshiwani (1983) anasisitiza ya kwamba matokeo mazuri katika shule za msingi na zile za upili yanaweza kuhusishwa na kuwepo kwa nyenzo na matumizi yake katika somo. Anatoa mfano kuwa, kuwepo kwa vitabu vya kiada vya kutosha huleta matokeo mazuri kwani somo huweza kufundishwa kwa urahisi. Jambo hili liliungwa mkono na uchunguzi wa Heyneman na wenzake (1981) waliofanya uchunguzi wao katika shule sitini ambazo zilichaguliwa kimakusudi nchini Uganda.

Matokeo ya utafiti wake yalionyesha ya kwamba kuna uhusiano wa karibu mno kuhusu matokeo mazuri kuhusu somo la ufahamu na kuwepo na matumizi ya vitabu vya kiada na nyenzo nyingine. Kulingana na matokeo hayo, mwalimu wa lugha anahitaji kuwa na benki ya nyenzo za kufundishia ambazo wanafunzi wake watazitumia wanapojifunza somo la ufahamu.

Ayot (1986) anasema kuwa, nyenzo za ufundishaji ni zana za kufundisha na kujifunza zinazowasaidia walimu katika ufundishaji na huimarisha ujifunzaji. Mawazo haya yanaungwa mkono na Wright (1976) anaposema kuwa, vyombo vya kufunza na kujifunza ni muhimu sana kwa sababu wanafunzi hupata habari zaidi kutokana na vyombo hivi kuliko kutoka kwa mwalimu. Mwalimu anapopanga atakayofunza, mikakati ya ufundishaji lazima aambatishe nyenzo za kufundisha ambazo huhusisha somo atakalofundisha. Gagne (1985) anasisitiza ya kwamba wanafunzi sharti wapate masomo katika mazingira yenye vigezo vya ujifunzaji kwani ujifunzaji wa hali ya juu

hutokea tu ikiwa nyenzo zitatumika katika somo husika. Ni vyema kukumbuka ya kwamba mwalimu anapotumia nyenzo katika kufundishia somo lake, hutumia muda mfupi sana kuwasilisha yale ambayo ameyatayarisha huku wanafunzi pia wakielewa somo na hata kulifurahia. Kwa mujibu wa Saunders (1974), Tajiriba ndio msingi mkuu katika hatua za ujifunzaji. Anataja kuwa mtu hukumbuka asilimia 10 ya anayoyasikia, asilimia 50 ya anayoona na kuyasikia, asilimia 90 ya anayoona, anayosikia na anayoyatenda. Hivyo basi, ufundishaji unaofaa ni ule unaohusisha zaidi matumizi ya vifaa vya ufundishaji ambavyo humuimarisha mwanafunzi kwa kuhuisha na kuamilisha tajriba yake.

Kulingana na K.I.E. (2002), nyenzo zinazopendekezwa kusahilisha uwasilishaji wa ufahamu ni nyenzo za kuona kama vile picha; vitabu vya kiada na ziada; nyenzo zilizorekodiwa kama vile vipindi vya redio, kanda za sauti na video, sidii na filamu, dondoo kutoka magazetini, vitabu, majarida na vipeperushi; maleba; ushairi simulizi na andishi; televisheni na mtandao. Matumizi ya nyenzo hizi yana umuhimu mkubwa katika somo la ufahamu, hutumika kumsaidia mwalimu kurahisisha uwasilishaji wa habari zake na kusititiza jambo linalofundishwa.

Nyenzo zikitumiwa vizuri, humsaidia mwanafunzi kutekeleza jambo kikamilifu na kuelewa dhana vizuri hata kama ni dhahania.Wanafunzi huhitaji kitu watakachosikia, hisi, ona, onja na nusa. Ufundishaji wa mwalimu usiotumia nyenzo utakuwa wa kidhahania kwa wanafunzi na baadhi yao hawatafahamu huku wengine wakichukua muda mrefu kupata mafunzo yaliyokusudiwa. Mwalimu anapokuwa mtawala darasani, wanafunzi watakuwa vizuu wanaotarajiwa kumeza wanayopewa kisha baadaye huyasahau mambo hayo (Saunders 1974).

Kulingana na K.I.E. (2006), mwalimu wa karne hii ya ishirini na moja si mwalimu ambaye anatarajiwa kutegemea kitabu cha kiada pekee kama wenzo wa kufundishia ufahamu. Vitabu vya kiada vilivyoidhinishwa na Wizara ya Elimu huwa ni mwongozo tu na hivyo ni jukumu la mwalimu kujaribu nyenzo nyingine ili kufanikisha mafunzo. Sababu ni kuwa, kufikia sasa hakuna kitabu hata kimoja maalum kilichochapishwa kuhusu mbinu na nyenzo za kufundisha ufahamu (Republic of Kenya, 2009). Kimui (1988) anadai kuwa ukosefu wa nyenzo na zana ni kizingiti kikubwa katika ufundishaji.

Kukosekana kwa nyenzo faafu huathiri pakubwa ufunzaji na ujifunzaji. Walimu wanaoishi katika enzi hizi hawapaswi kutegemea vitabu vichache au vya kiada pekee kama nyenzo ya pekee ya kufundishia ufahamu wa kusoma. Mabadiliko ya hali ya maisha ya kiteknolojia yanashurutisha utendaji wa kazi ya mwalimu kugeuka ili kuoana na hali ya mageuzi yanayomkabili. Hivyo basi mwalimu atalazimika kujiendeleza na kuwa na mtagusano zaidi na vitabu vya kiada, majarida, magazeti, nyenzo zingine nyingi. Githinji (2017) anasema kuwa hivi sasa katika karne ya 21, nyenzo za kielektroniki kama vile redio, televisheni, tarakilishi na mtandao zimeibuka kuwa bora katika ufundishaji na ujifunzaji wowote ule.

Walimu wanastahili kuunda na kutoa nyenzo za kufundishia ili kupata matokeo faafu katika ufunzaji. Vilevile wanapaswa kuhakikisha kuwa nyenzo za kufundishia zinapatikana jinsi inavyostahili (Hergenhahn, 1997). Haya yaweza kutimizwa kupitia ufaraguzi wa nyenzo zinazopatikana karibu. Ihebuzor (1986) anaelezea kwamba kuna mambo mbalimbali yanayotawala uteuzi wa nyenzo. Jambo la kwanza ni mazingira na majira.

Mwalimu anapaswa kuteua nyenzo zilizo katika mazingira ya mwanafunzi na zinazopatikana kwa urahisi katika kipindi fulani cha wakati. Kuna nyenzo nyingi katika mazingira ya mwanafunzi ambazo mwalimu akifanya ufaraguzi anaweza kuzitumia ili kufanikisha somo. Uteuzi wa nyenzo za kufundishia hutawaliwa pakubwa na madhumuni ya somo, yaliyomo na dhana muhimu zinazodhamiriwa kufundishwa katika somo. Nyenzo zinazoteuliwa ni muhimu ziwe zinarahisisha kueleweka kwa maudhui na dhana ya somo. Ndalu (2008) anasema kuwa uwepo na upatikanaji wa nyenzo ni kigezo muhimu mwalimu anapoziteua nyenzo. Ni bora kutafuta nyenzo zinazopatika kwa urahisi bila gharama kubwa.

Uhaba wa fedha na nyenzo zingine huchangia sana katika kutofanikisha utekelezaji wa kufundisha. Nyenzo na vifaa vinastahili kupatikana kwa gharama ya chini ili utekelezaji wa somo la ufahamu wa kusoma uweze kufanikiwa. Elliot na Woodward (1990) wanadahili kwamba walimu hutumia vitabu kuandaa na kutimiza matakwa ya mpangilio wa somo. Hivyo basi ugawaji wa nyenzo kwa ufundi ni muhimu katika kutimiza malengo fulani katika somo. Kwa hivyo, wahusika wote wanastahili kuhakikisha kuwa nyenzo zinapatikana na kutumiwa inavyotakikana ili kufaulisha somo la ufahamu wa kusoma. Walimu wakuu katika shule za Sekondari yafaa wahakikishe kwamba nyenzo na vifaa vya kufundishia vinapatikana ilimradi somo la ufahamu lifundishwe ipasavyo.

Utafiti uliofanywa na KICD (2014) uligundua kuwa uhaba wa nyenzo za kufundishia unapomkumba mwalimu katika ufundishaji wanafunzi wazembe hukosa kupata stadi zinazostahili ilhali wanafunzi werevu wanajifunza kwa kasi sana. Ni muhimu kusaka nyenzo za kutosha kwa wanafunzi wote mwalimu afundishapo. Mwalimu anafaa kuwa mbunifu zaidi katika kutafuta nyenzo za kufundishia maana wanafunzi hupata

stadi zinazohitajika anapotumia nyenzo ifaavyo. Nafasi ya vifaa na vitabu katika utekelezaji wa silabasi ni jambo linalofahamika (Tuntufye na Mwakyembe, 1986). Ukosefu wa nyenzo za kufundishia na kujifunzia ni jambo ambalo limekithiri ulimwengu mzima. Upungufu wake unaathiri moja kwa moja utendaji kazi wa walimu. Odeo (2007) na Wambui (2015) wanasema kuwa walimu wengi wanalalamikia ukosefu wa nyenzo faafu na vitabu rejea juu ya mbinu na vifaa vya kufundishia vipengee vya somo Kiswahili kikiwemo cha ufahamu.

Vile vile wanalalamikia kuwepo kwa anwani nyingi tofauti za vitabu vya kiada vinavyowakanganya. Isitoshe, vitabu hivi vina uhitilafiano kuhusu jinsi dhana na mambo fulani yanavyoshughulikiwa na waandishi tofauti tofauti wa vitabu hivi zaidi ya kuwa na lugha ngumu; mambo ambayo huwatatiza wanafunzi zaidi. Ingawa kuna maandishi mengi ambayo yanashughulikia ufahamu, hakuna kazi yoyote ambayo imezingatia mikakati na mbinu za kufundishia somo la ufahamu. Fauka ya wakuza mitaala kupuuza ufunzaji na ujifunzaji wa ufahamu kwa muda mrefu, waandishi na watafiti hawajashughulikia ufundishaji wake kwa kina. Asemavyo Wambui (2015), ni muhali kutekeleza mtaala wa masomo iwapo nafasi ya nyenzo haitatiliwa maanani. Utafiti huu unanuia kuchunguza uwepo na matumizi ya nyenzo katika ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu.

Onyango (2010) alichunguza pia uwepo na matumizi ya nyenzo katika ufundishaji wa Kiswahili. Matokeo ya utafiti wake yalidhihirisha ya kwamba kulikuwa na uhaba wa nyenzo za kufunzia na kujifunzia somo la Kiswahili katika madarasa ya mwanzo katika manispaa ya Kakamega. Nyenzo zingine hazikutumika isipokuwa ubao. Nyenzo zingine hazikutumika kutokana na ukosefu wa mwongozo wa matumizi, walimu kukosa uwezo wa kutumia nyenzo, matatizo ya nguvu za umeme. Walimu

wengi walitegemea picha na michoro kwenye vitabu vya kiada vya wanafunzi, hali hii ilitokana na ukosefu wa fedha na ukosefu wa maarifa ya kisanaa ya kuandaa nyenzo. Utafiti wetu utaangazia mambo yanayoathiri shughuli za kufunza na kujifunza somo la ufahamu ila si Kiswahili kwa jumla katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi.

Mukwa (2014) alifanya utafiti kuhusu umuhimu wa vifaa vya kufundishia somo la Kiswahili kwa jumla. Utafiti wake ulibainisha ya kwamba vifaa vilivyopewa kipaumbele katika ufunzaji wa somo la Kiswahili vilikuwa ni vile vilivyopigwa chapa, picha, redio na televisheni na ambavyo viliimarisha ufunzaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Utafiti wetu utazingatia sana kuhusu vifaa vya kufundishia kama kipengee kimojawapo kinachoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu wa kusoma. Fauka ya hayo utafiti huu unaazimia kuimarisha matokeo ya mitihani ya kitaifa ya Kiswahili ya KCSE. Utafiti wa Mukwa uliangazia shule zote zilizoko katika nchi nzima, lakini utafiti wetu utadhamiria kuchunguza matumizi ya nyenzo zinazotumika katika kufundishia ufahamu katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi ili kuchunguza uhusiano wake na matokeo ya somo la ufahamu katika mitihani ya kitaifa ya KCSE.

### 2.3.3 Maandalizi ya Mwalimu Nyanjani na Darasani

Maandalizi ambayo mwalimu anahitaji ni yale ya kibinafsi kabla ya kuingia darasani. Kwa mujibu wa Bennaars na wenzake (2004) mwalimu lazima awe anajua malengo ya elimu na silabasi na atayarishe maazimio ya kazi na mpangilio wa somo. Hoja hii inaonyesha muumano wa mambo yaani mwalimu akiyafahamu malengo ya elimu, huweza kuwaelekeza wanafunzi wake vizuri kutimiza malengo hayo akitumia silabasi. Maazimio ya kazi hutengenezwa kutokana na silabasi ilhali mpangilio wa somo hutokana na maazimio ya kazi. Quist (2000) anaeleza kuwa maazimio ya kazi humpa mwalimu mwongozo ambao utamwonyesha mada ambazo zitashughulikiwa katika muhula. Hivyo basi mwalimu ataweza kufanya mabadiliko katika mihula ijayo.

Naye Pollard (2002), anadokeza kuwa mwalimu anapotayarisha maazimio ya kazi anatakiwa ajiulize ni nini kinachotakikana kufunzwa? Kifunzwe vipi? Kifunzwe lini? Atajuaje ya kwamba kimefunzwa? Maswali haya humpa mwalimu mwongozo wa kutayarisha maazimio ya kazi ambayo yanahitaji kutekelezwa. Akichangia kuhusu maandalizi ya mwalimu, Moseti (2003) anasisitiza umuhimu wa mpangilio wa somo kwa mwalimu. Kwake mpangilio wa somo kwa mwalimu humsaidia mwalimu kuwasilisha somo kimantiki bila kuchanganya mambo. Mwalimu vilevile hatasahau dhana fulani, atakumbuka aina ya nyenzo za kufundishia zinazohitajika na atakuwa na ukadiriaji bora wa muda anapofundisha kwa hatua.

Linderman (2001) anadokeza kuwa kufaulisha utekelezaji wa silabasi kunategemea mwalimu kuweka malengo bayana na shabaha za kufundisha. Mawazo haya ya Linderman vilevile yameangaziwa na K.I.E. (2006). Uandalizi wa walimu nyanjani pia hauwezi kuepukika kwani asemavyo Peters (1980) ni kuwa maarifa hubadilika na wakati hivyo basi, huenda yanayoibuka hayakuwepo awali wakati wa maandalizi. Maandalizi nyanjani husaidia sio tu kuelezea ufundishaji wa mambo mapya bali pia kuvuta kumbukumbu ya yale ambayo huenda yakasahaulika.

Taaluma ya elimu lazima isisitize kozi za nyanjani kwa sababu inakumbwa na mabadiliko mengi sana. Brian (1975) na Oluoch (2002) wana hoja kwamba mafunzo ya nyanjani huhitajika ili kupata maarifa mapya. Kwa mujibu wa Goble na Porter (1977) na Muruguru (2000) kozi za kupiga msasa huwa njia nzuri ya kujaliza pengo mahali ambapo walimu wamegundua upungufu au wanahitajika kujiamini katika ujuzi mahsusi. Stima (1988) wakati fulani akiwa mkaguzi wa shule katika wizara ya elimu alisisitiza kuwa mafundisho ya walimu nyanjani ni muhimu sana.

Shiundu na Omulando (1992) wanakubaliana na haya kwa kusema kwamba mafunzo ya nyanjani yanasaidia kumfahamisha na kumzoesha mwalimu kuhusu mambo mapya ya hivi karibuni katika somo lake. Walimu pia huhitaji fursa ya kujifunza maarifa mapya yanayotokana na maendeleo katika uwanja wao na kubadilishana mawazo. Maarifa haya yanawezekana kupitia semina, warsha na kozi zingine za kupiga msasa (Fullan, 1990; Shiundu na Omulando 1992). Omulando (1992) anasema kuwa mfumo wa 8-4-4 ulipoanzishwa palizuka haja ya kuwapiga msasa walimu ili kuelewa usetaji uliokuwa katika somo la Kiingereza.

Usetaji huo ulikuwa mwelekeo mpya katika Kiingereza wakati huo kama ilivyo katika somo la Kiswahili kwa sasa, kwani tunaona somo hili likiwa na vipengele vipya kama vile ufahamu. Kwa mujibu wa Sifuna (1996), walimu wanapaswa kuhudhuria warsha, makongamano na mikutano ili kupigwa msasa. Msaada huu utamfanya mwalimu kujenga uhusiano na kupata ufafanuzi kutoka kwa walimu wengine na wataalmu ambao atashirikiana nao. Jambo hili litaimarisha mitazamo ya mwalimu juu ya maudhui na mbinu zake za ufundishaji.

Utafiti wa Mwaura (2013) unabainisha kuwa walimu wengi huona muhali kujifunza mikakati mipya ya kufundishia palipo na uzoefu wa mbinu nzee wanazozifahamu vyema. Kwa hivyo, kuna haja ya mafunzo nyanjani kuhusu mbinu na nyenzo za kufundishia. Anasema kwamba walimu wengi hawasomi baada ya kufuzu vyuoni licha ya mafunzo ya ziada kuwa muhimu kwa ufanisi wa shughuli za kufundisha na kujifunza shuleni. Hii ndiyo sababu Kiragu (1986) na Githinji (2017) wanasema kuwa mbali na kiwango cha kufuzu cha walimu, uwepo na ubora wa vitabu na usahihishaji

wa vitabu, mafunzo ya walimu nyanjani ni kiungo muhimu katika kufanikisha uelewaji wa ufahamu. Kutokana na ufichuzi huu, inadhihirika wazi kuwa maandalizi ya walimu ni muhimu lakini inasikitisha wanafunzi wanaofunzwa na walimu waliohitimu kuanguka mtihani wa ufahamu. Utafiti huu ulikusudia kuchunguza ikiwa maandalizi ya walimu kuhusu somo la ufahamu yanaathiri ufundishaji na ujifunzaji wake.

### 2.3.4 Maoni ya Wanafunzi Kuhusu Somo la Ufahamu wa Kusoma

Baker (1992) ameonyesha kuwa kuna sababu zinazochangia kuwepo kwa mielekeo. Katika utafiti kuhusu wanafunzi na lugha ya Kiwelsh, Baker ameelezea kwamba tofauti za kijinsia, umri, usuli wa lugha ya kwanza, aina ya shule na "utamaduni wa vijana" huathiri viwango vya mielekeo ya wanafunzi. Aligundua kuwa wanafunzi waliokuwa na asili ya Kiwelsh walipenda lugha hiyo kuliko wale wenye asili tofauti.

Kwa mujibu wa Ryan na wenzake (1982), mielekeo ya lugha kwa upana wake ni ukadiriaji wa kihisia, kiufahamu na kitabia na mwitiko wetu kwa lugha tofauti au wazungumzaji wake. Hali hii kwa jumla huathiri matumizi ya lugha katika jamii. Manufaa ya kujifunza kwa lugha kwa mujibu wa Baker (1992), yanaweza kuwekwa katika makundi mawili. Kundi la kwanza linahusisha motisha ya mtu kujifunza lugha kwa kuwa ana imani kuwa ujuzi na umilisi katika lugha husika utamwezesha kupata ajira. Hii ndiyo sababu inayowafanya wanafunzi kwa mfano, mbali na kuwa na umilisi katika Kiingereza, pia wanajifunza lugha nyingine za kigeni kama vile Kifaransa na Kijerumani. Kundi la pili linahusu kuwepo kwa haja ya utambulisho na kundi la watu.

Krashen (1992) anasema kwamba mielekeo ni ya muhimu sana katika ujifunzaji wa lugha. Wanafunzi wakiwa na mielekeo chanya hupata ari ya kutia bidii katika

ujifunzaji wao wa lugha na kwa kufanya hivyo wao hupokea maarifa husika kwa wingi. Anafafanua mielekeo kuwa ni jinsi ambavyo mtu hufikiria kuhusu mtu au kitu. Mielekeo hii hujitokeza na kuonekana kwenye tabia za mtu kuhusu mtu watu au kitu. Hivyo basi, mwanafunzi huenda akachukulia somo la ufahamu kuwa gumu au rahisi na aonyeshe ile hali ya kupata ufahamu kuwa mgumu au rahisi. Kwa mfano mwanafunzi anaweza kukosa kusoma ufahamu na akose kufanya mazoezi; tabia inayojitokeza hapo ni mwelekeo hasi au mwelekeo chanya.

Utafiti wa Mwangi (1985) nao ulikuwa na matokeo kuwa kulikuwa na uhusiano mkubwa kati ya mielekeo na matokeo. Katika mazingira ya shuleni Mwangi ameonyesha kuwa kuna uhusiano chanya baina ya mielekeo ya wanafunzi na utendaji wao. Utafiti huo uliofanywa katika tarafa ya Maseno wilayani Kisumu pia ulionyesha kuwa vipengele mbalimbali vya kijamii viliathiri mielekeo ya wanafunzi. Vipengele hivyo ni pamoja na jinsia, sehemu ya makazi, umri wa kujifunza lugha na usuli wa lugha ya kwanza. Mwangi alipata kuwa, katika sampuli ya wazungumzaji wa lugha ya Dholuo, ambao sio Wabantu, kulikuwa na mielekeo hasi kwani walichukulia lugha ya Kiswahili kuwa lugha ngeni jambo ambalo limekuwa likiathiri matokeo yao ya somo la Kiswahili.

Pia wanaona Kiswahili kama lugha ambayo inaweza tu kuwasaidia kutangamana na watu wa kawaida katika jamii na haina uwezo wa kuwakweza katika hadhi ya kiuchumi na kijamii. Kwa hivyo, si muhimu sana katika maisha yao. Utafiti wa Mwangi ulihusisha uchunguzi wa athari ya mielekeo ya wanafunzi kwa ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili ilhali utafiti huu unahusu uchunguzi wa athari za mielekeo kuhusu ujifunzaji wa kipengee cha ufahamu katika Kiswahili. Fauka ya hayo, utafiti huo ulifanywa katika shule za Sekondari ambapo suala la mielekeo

limekithiri. Wanafunzi wengi hawapendi somo la ufahamu wakiwa na madai kuwa somo hilo ni tata mno. Wengi wao hupuuza kulijibu swali hilo la ufahamu jambo ambalo limechangia pakubwa katika kuyarudisha nyuma matokeo ya somo la Kiswahili.

Utafiti uliofanywa kuhusu mielekeo ya wanafunzi kuhusu somo la Hesabu na Hunsen (1977) ulikuwa na matokeo kuwa, wanafunzi waliokuwa na mielekeo chanya waliweza kupata alama za juu kuliko wale waliokuwa na mielekeo hasi. Vile vile, wanafunzi waliokuwa na mielekeo chanya kuhusu somo hilo, walitumia muda wao mwingi sana kufanya mazoezi katika somo hilo. Utafiti wa Hunsen unahusu uhusiano kati ya mielekeo ya wanafunzi na matokeo katika somo la Hesabu ilhali utafiti huu unahusu athari za milelekeo ya wanafunzi kwa ujifunzaji wa somo la ufahamu katika Kiswahili.

Utafiti uliofanywa na Githinji (2017) kuhusu athari za mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu kipengee cha sarufi ulitambua ya kwamba, walimu walikosa ilhamu za kufundisha somo la sarufi huku wanafunzi pia wakikosa motisha ya kujifunza somo hilo; jambo ambalo limechangia pakubwa katika matokeo ya somo hili kudorora. Ingawa utafiti wetu ulichunguza mielekeo ya walimu na wanafunzi, ulihusu athari zake kwa ufunzaji na ujifunzaji wa ufahamu tofauti na wa Githinji uliohusu sarufi.

Kutokana na uhakiki wa maandishi, mapengo yafuatayo yamedhihirika. Kwanza, mbinu na nyenzo huathiri ufunzaji wa ufahamu lakini utafiti zaidi unahitajika kufanywa ili kubainisha matumizi yake katika shule za upili kufundishia somo la ufahamu. Pili ni wazi kuwa mielekeo huathiri ufundishaji wa Kiswahili. Hata hivyo,

hakuna uchunguzi wa kina uliofanywa kuelewa jinsi mielekeo ya walimu huathiri ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu wa kusoma katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi. Isitoshe, ni dhahiri pia kuwa ingawa mielekeo ya wanafunzi huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili, hakuna utafiti uliofanywa kubainisha jinsi mielekeo hii huathiri ujifunzaji wa Kiswahili hususan somo la ufahamu katika kiwango cha shule za upili, kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi.

Utafiti huu basi, unanuia kujaza mapengo haya kwa kubainisha mambo yanayoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu wa kusoma katika Kiswahili, katika shule za upili katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi. Lengo lake ni kusaidia kuimarisha matokeo ya Kiswahili katika eneo hili ambayo yamedorora.

## 2.4 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia uhakiki wa maandishi yanayohusiana na mada ya utafiti. Mambo hayo ni kama vile ufafanuzi wa dhana na nafasi ya ufahamu, michakato katika usomaji wa ufahamu, na mambo yanayoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu kama vile, maandalizi ya mwalimu kabla ya kuingia darasani kufundisha somo la ufahamu, mbinu na nyenzo za kufundishia na kujifunzia somo la ufahamu wa kusoma darasani na maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu somo la ufahamu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sehemu hii imeshughulikia muundo wa utafiti, eneo la utafiti, watafitiwa, taratibu za uteuzi wa sampuli, sampuli ya watafitiwa na vyombo vilivyotumika kukusanya data za utafiti huu. Aidha, sura hii ilifafanua michakato iliyotumiwa kuchanganua na kufasiri data ya utafiti.

## 3.2 Muundo wa Utafiti

Muundo wa usoroveya elezi umetumiwa. Kulingana na Kombo na Tromp (2006) ni kwamba, muundo huo hutumiwa kupata data kuhusu mielekeo, maoni, mazoea na pia mambo muhimu yanayohusu elimu na masuala ya jamii. Katika utafiti huu muundo wa usoroveya elezi ulisaidia katika kuchunguza ili kupata habari zaidi kuhusu maoni ya wanafunzi na walimu kuhusu somo la ufahamu, maandalizi ya walimu, mbinu na nyenzo ambazo wanatumia kwa kufundishia ufahamu na jinsi vigezo hivi vinaathiri ufundishaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu. Good (1972), ameeleza kuwa kwa kutumia muundo huu wa usoroveya elezi, mtafiti anaweza kupata data ya kutathmini njia mbalimbali zinazotumiwa ili uamuzi mwafaka kuweza kufikiwa.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika Kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi, Kaunti ya Kisumu, Kenya. Eneo hili linapakana na Kaunti ya Vihiga upande wa Kaskazini, Kericho upande wa Kusini, Nandi upande wa Mashariki. (tazama kiambatisho E). Sababu za kuchagua eneo hili ni kuwa, matokeo ya mtihani wa KCSE, mitihani ya miigo pamoja na ya mwisho wa mihula yamekuwa chini ya wastani katika lugha ya Kiswahili kuanzia mwaka wa 2012 hadi 2016 (tazama jedwali 1.2). Matokeo hayo

yanahusishwa na utendaji wa chini katika somo la ufahamu inavyodhihirishwa katika ripoti ya, mitihani ya miigo, mwisho wa mihula pamoja na KNEC (2015). Sababu nyingine ni kwamba mtafiti hajawahi kukumbana na utafiti wa aina hii ambao ulifanywa katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi.

Mtafiti vilevile alichagua eneo hili kwa sababu alilielewa vyema. Tuckman (1988) anasema kuwa wakati mwingine uzoefu wa eneo la utafiti humpa mtafiti kibali miongoni mwa wakazi wa eneo husika. Anatilia mkazo kuwa eneo linalofaa kwa utafiti ni lile linalofikiwa kwa urahisi na mtafiti na watafitiwa. Mtafiti alitarajia kwamba matokeo ya utafiti wake yangeibua data halisi ambayo ingeweza kubainisha kinachotendeka katika sehemu zingine nchini zenye sifa sawa na eneo la kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi.

### 3.4 Idadi Lengwa

Kwa mujibu wa Peil (2002) si rahisi kuchunguza idadi nzima ya watu inavyostahili kwani wakati na gharama ni vizingiti vikubwa. Idadi lengwa katika utafiti ni kikundi kikubwa cha watu wenye sifa moja au zaidi za kimsingi zinazozingatiwa katika utafiti. Molusa (1992) anadai kuwa ni kutokana na idadi lengwa ambapo mtafiti hupata watafitiwa kamili. Kwa mujibu wa rekodi za Wizara ya Elimu (2015), kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi, ina shule thelathini na saba za upili (tazama kiambatisho D), walimu sitini wa Kiswahili na wanafunzi mia sita. Katika utafiti huu idadi lengwa ilijumuisha wanafunzi wote wa kidato cha tatu pamoja na walimu wa somo la Kiswahili waliokuwa wakifundisha fundisha kidato cha tatu katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi.

### 3.5 Uteuzi wa Sampuli

Kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi ina shule 37 za upili zenye sifa zifuatazo: za Wasichana za Bweni (WB), za Wavulana za Bweni (WVB), za Mseto za Kutwa (MK), za Mseto za Bweni (MB). Utafiti umehusisha wanafunzi wa kidato cha tatu kutoka shule zilizoteuliwa kutoka kwenye eneo la utafiti. Sababu za kuteuliwa kwa kidato cha tatu ni kuwa wanafunzi hawa wamekuwa na miaka mitatu ya ujifunzaji wa ufahamu katika kiwango cha shule za upili na hivyo, wana tajriba kuhusu somo la ufahamu na jinsi somo hili linavyofunzwa. Wanafunzi wa kidato cha kwanza walikuwa wageni, wa kidato cha pili walikuwa wangali wanajizoesha kukabiliana na maisha ya shule za upili na wa kidato cha nne walikuwa na kazi nyingi ikizingatiwa kuwa wanajiandaa kwa mtihani wa KCSE.

Ili kupata sampuli wakilishi ya utafiti, mtafiti aliweka shule katika matabaka tofauti tofauti: WB, WVB, MK, na MB. Sababu ya kufanya hivi ni kuwa kila aina ya shule huwa na mazingira yake bainifu na tofauti na zingine ambayo huathiri ufundishaji na ujifunzaji. Utabakishaji ulitumiwa ili kupata sampuli yenye uwakilishi tosha na yenye kutupatia data inayoweza kutegemewa na matokeo ya kuaminika na kuthibitika (Kilemi & Wamahiu, 1995; Kerlinger, 2004; Kothari, 2004). Sampuli ya wanafunzi walioshiriki katika utafiti iliteuliwa kwa mbinu ya bahati nasibu.

Mbinu hii ilihakikisha kuwa wanafunzi wote kutoka shule za matabaka yote; WB, WVB, MK, na MB walipewa nafasi sawa ya kushiriki katika utafiti. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999) ni vigumu sana kuchunguza idadi nzima ya watu inavyotakiwa kwa sababu ya wakati na gharama na hivyo watafiti huchagua na kuzingatia idadi fulani ambayo huitwa sampuli. Tuckman (1988) anasema kwamba sampuli ya asilimia 30 ya wahojiwa ni wakilishi na ya kutosha kukusanya data ya

kutegemewa na isiyo na upendeleo wowote mradi imeteuliwa kwa misingi ya sifa bainifu za sampuli. Hivyo basi utafiti huu uliwalenga wanafunzi 180 (asilimia 30 ya wanafunzi 600) wa kidato cha tatu katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi. Miongoni mwa idadi ya wanafunzi 180, 110 walikuwa wasichana na 80 wavulana. Haingewezekana kuhusisha wanafunzi wote 600 kwa sababu ya ukubwa wa idadi.

Shule zilizoteuliwa kwa misingi ya matabaka manne ilikuwa ifuatavyo: WB -2, WVB-2, MK-5, na MB-2 Jumla ni shule 11 ambazo ni asilimia 30 ya shule zote za upili katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi. Kwa upande mwingine, mbinu ya uteuzi wa kimakusudi ilitumika pia kuchagua sampuli wakilishi ya walimu 18 ambao ni 30% ya walimu walioshiriki katika utafiti huu. Idadi hii ilichukuliwa kutoka kwa idadi yote ya walimu 60 (100%) wa Kiswahili wanaopatikana katika shule za upili katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi.Mtafiti aliwachagua walimu 11 kutoka kila shule.Mtafiti aliwaongeza walimu wengine 7 ambao walikuwa watahini wa mitihani ya Kiswahili ya kitaifa karatasi ya pili sehemu ya ufahamu na ambao wangempatia majibu bora zaidi kuhusu utendaji wa wanafunzi.

### 3.6 Vifaa vya Utafiti

Ili matokeo ya utafiti wowote (yapatikane na) yawe na uthabiti, mtafiti hana budi kushirikisha vifaa mbalimbali (Peil, 2002). Peil anaeleza kwamba, matumizi ya vifaa zaidi ya kimoja huweza kuziba pengo lililoachwa na kingine hasa ikiwa kimetumiwa kuibua data sawa. Matumizi ya vifaa anuwai huimarisha uaminifu na uthabiti wa data. Katika utafiti huu, mtafiti ametumia vifaa vifuatavyo: hojaji, na mwongozo wa usaili. Vifaa hivi vimejadiliwa hapa chini kimoja baada ya kingine. Vifaa hivi viliandaliwa kulingana na madhumuni ya utafiti.

### 3.6.1 Hojaji

Mtafiti ametumia hojaji kati ya vifaa vingine kukusanya data kuhusu mbinu za kufunzia na kujifunzia somo la ufahamu,matumizi ya nyenzo,maandalizi ya walimu na maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu. Hojaji ilijitokeza kuwa ya muhimu katika utafiti huu kwa sababu ilikuwa mwafaka sana katika kuchunguza mambo yanayoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu. Newman (1994) anataja kwamba hojaji fupi ni mwafaka katika utafiti wowote. Hojaji iliyotumiwa ilikuwa na maswali funge na wazi kama inavyopendekezwa na Wamitila (2004). Sehemu funge ilikuwa na maswali na majibu ambapo mhojiwa alihitajika kuteua majibu kisha kulikuwa na maswali wazi ambayo yalihitaji maoni, maelezo na mitazamo ya wasailiwa. Mtafiti anakubaliana na mawazo haya na aliyazingatia katika maandalizi ya hojaji.

#### 3.6.1.1 Hojaji ya Walimu.

Hojaji ya walimu imegawika katika sehemu nne. Kwenye sehemu ya kwanza, vipengee kadha wa kadha kuhusu walimu vilibainishwa kupitia kifaa hiki. Katika sehemu ya kwanza, yaliyoshughulikiwa ni habari za kimsingi kumhusu mwalimu. Habari hizi zilihusu jinsia, kiwango cha kuhitimu na tajriba. Kati ya yale yaliyoshughulikiwa katika sehemu ya pili ni mbinu za ufundishaji na makadirio ya ufaafu wake katika kufundishia ufahamu na athari za mbinu zisizo bora kwa ufundishaji wa ufahamu. Sehemu ya tatu ilihusu uwepo wa nyenzo za kufundishia ufahamu, utoshelezo wake, ufaafu na matumizi ya nyenzo hizo darasani. Sehemu ya tatu ilihusu maoni ya jumla kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu. Mambo yaliyolengwa kubainishwa katika sehemu hii ni manufaa ya kujifunza ufahamu, matumizi ya nyaraka za maandalizi ya kufunza, changamoto zinazokumba ufundishaji wa ufahamu na suluhisho kwa changamoto hizo. (tazama kiambatisho A).

### 3.6.1.2 Hojaji ya Wanafunzi

Hojaji ya wanafunzi imetokeza kuwa mwafaka katika kuchunguza maoni au mielekeo ya wanafunzi kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu. Hojaji hii iligawika katika sehemu tatu. Sehemu ya kwanza ililenga kubainisha jinsia ya mtafitiwa. Sehemu ya pili ilinuia kubainisha mielekeo ya mtafitiwa kuhusu ufahamu wa Kiswahili. Katika sehemu ya tatu, mtafitiwa alihitajika kubainisha manufaa ya ufahamu, changamoto zinazokabili ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu, athari za mielekeo ya wanafunzi kuhusu ufundishaji na ujifunzaji ufahamu, mbinu zinazotumika kufundishia ufahamu na mapendekezo ya jinsi ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu. (tazama kiambatisho b)

## 3.7 Mwongozo wa Maswali ya Usaili

Mbinu ya mahojiano pia ilitumiwa katika utafiti huu. Masaili yalitumika kwa sababu, hulenga suala la utafiti moja kwa moja na hivyo huibua data halisi. Ili kuhakikisha kuwa usaili ulikwepa upendeleo, sampuli ilihojiwa kwa kufuata mpangilio sawa wa maswali yaliyosomwa jinsi yalivyokuwa yameandikwa na maswali hayo yaliulizwa bila kuonyesha kuwa yalimlenga mhojiwa binafsi. Maswali hayo vilevile yalirudiwa kila ilipohitajika (Grey 2004). Majibu yaliandikwa jinsi yalivyotolewa na wahojiwa bila kuongezea hisia za mtafiti. Mwongozo huu ulinuia kuthibitisha kile ambacho walimu walisema hukifanya kupitia kwa hojaji. Data iliyolengwa ilihusu matumizi ya mbinu na vifaa pamoja na maoni au mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu wa Kiswahili (Tazama kiambatisho C).

### 3.8 Uaminifu wa Vifaa vya Utafiti

Katika harakati za kupima iwapo vifaa vya hojaji na mwongozo wa masaili vinaaminika na kutegemewa, mtafiti alivifanyia majaribio kwa walimu watatu katika shule mbili zilizo katika eneo tofauti na lile la utafiti kabla ya utafiti wenyewe. Kufanya hivi, kulimsaidia mtafiti kugundua maswali ya utafiti ambayo hayakulengwa vizuri katika nyenzo hizo na kuzirekebisha mapema. Isitoshe, ili kupima uaminifu wa vifaa, mtafiti alitumia mbinu ya uradidi. Aliwapa walimu watatu hojaji mara ya kwanza na kisha kuwapa tena baada ya siku chache baadaye. Mtafiti alichanganua vifaa na kulinganisha tuzo za kila mtafitiwa.

### 3.9 Uthabiti wa Vifaa vya Utafiti

Kulingana na Nkapa (1997) uthabiti wa vifaa ni ukamilifu wa vifaa mintarafu vipengele vilivyoainishwa kwenye vifaa hivyo. Ili kuhakikisha uthabiti wa vifaa vya utafiti, mtafiti alitunga maswali yanayohusiana moja kwa moja na mambo yanayoathiri ufundishaji wa ufahamu wa Kiswahili katika shule za upili. Maswali katika vifaa hivi yaliambatana na vipengele katika madhumuni ya utafiti, nadharia na vigeu vya utafiti. Mtafiti vilevile alichanganua majibu katika majaribio ya vifaa vya utafiti. Uchanganuzi huu ulimwezesha mtafiti kulainisha baadhi ya maswali na kuyafanya yawe faafu katika utafiti huu. Kulingana na Orodho (1996), vifaa vya utafiti vinaweza kuthibitishwa na waataalamu mbalimbali. Uthabiti wa vifaa ulizingatiwa kwa kurejelea uelekezi wa baadhi ya wataalamu ambao wametoa uelekezi kuhusu ufundishaji wa ufahamu wa kusoma. Hatimaye, wasimamizi wawili wa utafiti walipitia vifaa hivi kisha kuviidhinisha kuwa vina uthabiti.

### 3.10 Majaribio ya Vifaa vya Kukusanyia Data

Kwa mujibu wa Mutai (2000), majaribio ya awali ya vifaa humwezesha mtafiti kutambua udhaifu na ubora wa vifaa vyake. Matatizo huweza yakawa ya utunzi mbaya wa maswali au msamiati usio mwafaka. Matatizo haya lazima yalainishwe kabla ya utafiti kamili kuanza. Majaribio yalifanywa baada ya mtafiti kupata kibali kutoka kwa Wizara ya Elimu ili kufanya utafiti. Siku nne kabla ya utafiti kufanywa, mwongozo wa usaili na hojaji zilitolewa kwa walimu watatu wakati wa kufunza, katika shule mbili tofauti katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi. Shule hizi ambazo hazikuhusishwa wakati wa utafiti wenyewe ni shule ya upili ya A na shule ya upili ya B. Kusudi la majaribio huwa ni kubainisha iwapo kuna tatizo lolote katika kuandaa maswali ya hojaji na mwongozo wa usaili (Mugenda na Mugenda, 1999). Baada ya majaribio, maswali ya hojaji yalirekebishwa pale ambapo yalionekana kutolingana na madhumuni ya utafiti. Vifaa hivi viliimarishwa na kuandikwa upya ili maswali ya hojaji na mwongozo wa

### 3.11 Mchakato wa Ukusanyaji Data

Shughuli hii ilitekelezwa baada ya mtafiti kupata kibali kutoka kwa Baraza la usaili yalingane na madhumuni na maswali ya utafiti.Kitaifa la Sayansi na Teknolojia. Ukusanyaji wa data ulichukua muda wa mwezi mmoja. Mtafiti alizitembelea shule zilizoteuliwa mwenyewe ili kuwapa walimu hojaji pasipo kuathiri shughuli zao za kila siku. Baada ya mwisho wa wakati uliotolewa, mtafiti mwenyewe alizikusanya hojaji kutoka kwa walimu. Hojaji hizi zilikusanywa siku ambayo mtafiti alifanya usaili. Mtafiti alibuni mpangilio wa kuzuru shule ambapo kila shule ilitengewa siku yake. Wasailiwa walifahamishwa kuwa habari zilizokusanywa zitaboresha na kuimarisha ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu wa kusoma.

### 3.12 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Data iliyokusanywa kupitia kwa hojaji na mwongozo wa usaili ilichanganuliwa baada ya kuandaliwa. Katika hojaji, kila sehemu ya swali iliwekwa katika mpango ulio wazi na kisha kuchanganuliwa kwa misingi ya dafaa (mara idadi) na kuwasilishwa kwa asilimia. Data iliyokusanywa wakati wa usaili ilidhamiriwa kuthibitisha kile ambacho walimu walisema hukifanya kupitia kwa hojaji (Tazama Kiambatisho C). Mbinu, vifaa na mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu ilichunguzwa wakati wa usaili. Mtafiti alilinganisha matokeo ya hojaji na mwongozo wa usaili ili kutambua mambo yanayoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu wa Kiswahili. Uchanganuzi huu ulilenga kudhihirisha uhalali wa matokeo ya utafiti. Hatua hii ilichangia katika mahitimisho na kutoa majibu kwa maswali ya utafiti. Hitimisho la jumla lilifanywa kwa misingi ya data yote iliyokusanywa kupitia kwa vifaa vyote vya utafiti.

### 3.13 Changamoto Nyanjani

Mtafiti alikumbana na changamoto kadha wa kadha katika harakati za kukusanya data. Mojawapo ni kwamba baadhi ya walimu hawakuwa na ari ya kushiriki katika utafiti. Ilimchukua mtafiti muda kuwashawishi watafitiwa licha ya kuwahakikishia kwamba matokeo ya utafiti hayatakuwa na athari yoyote kwa kazi yao. Watafitiwa walioogopa kutafitiwa walielezwa kuwa kiini cha utafiti kilikuwa kupata utatuzi wa changamoto zinazowakumba kuhusu ufunzaji wa ufahamu wa kusoma na wala si kutathmini utekelezaji wao. Mtafiti hakukusanya hojaji kwa muda aliokuwa amepanga kwa vile hazikuwa zimejazwa na baadhi ya walimu. Ilimbidi mtafiti afanye ziara kadhaa na hivyo kumgharimu zaidi kiwakati na kifedha; hali iliyoathiri mpangilio wake wa kazi. Isitoshe, baadhi ya walimu kutaka kulipwa pesa ili kujaza

hojaji au kushiriki katika kujibu maswali ya usaili. Hali ilipotokea hivyo, mwalimu aliwasihi kushiriki bila kulipwa kwani hata wao wangehitaji kusaidiwa katika siku zijazo za usoni, ikiwa watafanya utafiti.

Tatizo jingine ni kuwa katika shule kadhaa wanafunzi walikuwa wametumwa nyumbani ili waende kuleta karo. Hivyo basi ilimbidi mtafiti kufanya ziara nyingine katika eneo hilo la utafiti akingojea kupata idadi ya wanafunzi iliyofaa kwa utafiti. Hata hivyo, matatizo haya hayakukwamisha shughuli za utafiti kwani mtafiti alifaulu kupata data ya kutosha kutumia.

### 3.14 Hitimisho

Katika sura hii, mtafiti ameeleza muundo wa utafiti. Ameeleza eneo la utafiti, njia za utafiti, idadi lengwa, vifaa vya kukusanyia data, uaminifu wa vifaa vya utafiti na uthabiti wa vifaa hivi. Aidha, ameeleza majaribio ya vifaa vya kukusanya data, mchakato wa ukusanyaji wa data na changamoto nyanjani. Sura ifuatayo itashughulikia matokeo ya maoni kuhusu matumizi ya mbinu na nyenzo za kufundishia somo la ufahamu ufahamu, maoni au mielekeo ya walimu na wanafunzi pamoja na maandalizi ya walimu nyanjani na kabla ya kuingia darasani kufundisha.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inahusu uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo yaliyokusanywa kutoka nyanjani kwa kutumia hojaji na mwongozo wa usaili. Data imechanganuliwa kwa mtindo wa maelezo kwa kutumia majedwali, chati, grafu na asilimia kwa madhumuni ya kuifanya ieleweke kwa urahisi. Utafiti huu ulidhamiria kushughulikia malengo yafuatayo na ambayo yalitumika kuwasilisha matokeo ya utafiti.

## 4.1 Mbinu za Kufundishia Ufahamu

Katika sehemu hii, tumeshughulikia lengo letu la kwanza ambalo ni kubainisha mbinu zinazotumiwa na walimu wa Kiswahili kufundishia ufahamu. Mara-idadi ya matumizi yake na makadirio ya ufaafu wa mbinu hizo katika kufundishia somo la ufahamu.

### 4.1.1 Matumizi ya Mbinu za Kufundishia

Dhima ya mbinu mwafaka katika ufundishaji wa Kiswahili inaungwa mkono na wataalamu wengi (Ellis, 1997; Lighbown na Spada, 1990 na Gathumbi na Masembe, 2005). Ingawa mbinu nyingi zilijadiliwa na baadhi ya hizo kupendekezwa katika ufundishaji wa ufahamu katika sura ya pili utafiti ulibainisha kuwa nyingi ya mbinu hizi hazitumiki katika ufundishaji wa ufahamu. Data kuhusu mbinu zitumikazo kufundisha ufahamu ilikusanywa kutoka kwa hojaji za walimu, wanafunzi na mwongozo wa usaili kwa walimu.

**Jedwali 4.1: Matumizi ya Mbinu za Kufundishia (mwitiko wa walimu)**

| **Mbinu** | **Inatumika** | **Haitumiki** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Makundi | 10(56%) | 8(44%) | 18(100%) |
| Masaili | 10(56%) | 8(44%) | 18(100%) |
| Kusoma kwa sauti | 18(100%) | 0(0%) | 18(100%) |
| Kusoma kibinafsi | 7(39%) | 11(61%) | 18(100%) |
| Mhadhara | 16(89%) | 2(11%) | 18(100%) |
| Kusimulia hadithi | 5(28%) | 13(72%) | 18(100%) |
| Mbinu ya kidrama | 4(22%) | 14(78%) | 18(100%) |
| Mjadala | 6(33%) | 12(67%) | 18(100%) |

**Chanzo: Data kutokana na maswali ya hojaji**

Jedwali 4.1 linaonyesha kuwa walimu 10(56%) ndio waliotumia makundi huku 8(44%) wakisema kuwa hawakuitumia mbinu hii. Vilevile, walimu 10(56%) walikiri kutumia mbinu ya maswali na majibu ikilinganishwa na 8(44%) waliosema hawaitumii. Walimu wote 18(100%) waliwahusisha wanafunzi katika usomaji kwa sauti. Walimu 7(39%) walipendelea kutumia mbinu ya wanafunzi kujisomea kibinafsi ikilinganishwa na walimu 11(61%) waliosema hawapendelei mbinu hii. Njia ya mhadhara ilipendelewa na walimu 16(89%) ikilinganishwa na 2(11%) waliosema hawaitumii. Huenda kutotumiwa sana ni kwa vile mbinu hii haimshirikishi mwanafunzi kikamilifu. Mbinu ya kusimulia hadithi ilitumiwa na walimu 5 (28%) huku 13(72%) wakisema hawaitumii. Mbinu ya kidrama ilitumiwa na walimu 4(22%) tu ikilinganishwa na 14(78%) ambao hawakuitumia. Mijadala ilipendelewa kwa

asilimia ndogo ya 6(33%) huku 12(67%) wakisema hawaipendelei. Matokeo haya yanaonyesha kuwa mbinu za kusoma kwa sauti, makundi, maswali na majibu na mhadhara ndizo zinazopendelewa na walimu wengi kwa zaidi ya 50% kuliko zile zinazomweka mwanafunzi katika nafasi ya kuendesha ujifunzaji wake. Hali hii huenda ndiyo inayoathiri ujifunzaji wa ufahamu na kusababisha matokeo duni katika sehemu hii. Kwa mujibu wa Mukwa na Too (2014), mbinu zisizomhusisha mwanafunzi si bora kwa kuwa wanafunzi huachwa nje ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo ambapo mwalimu ndiye huchukua usukani.

### 4.1.2 Mara-idadi ya Matumizi ya Mbinu za Kufundishia

Mtafiti alitaka kujua mara-idadi ya kutumia mbinu za ufundishaji darasani. Matokeo yameonyesha kuwa mbinu ambazo hutumiwa mara kwa mara ni masaili 14(78%), kusoma kwa sauti 10(56%), na mhadhara 10(56%). Mbinu ambazo hazitumiwi sana ni kusoma kibinafsi 3(17%), makundi 6(33%), kusimulia hadithi 1(6%), mbinu ya kidrama 3(17%) na mjadala 6(33%). Matokeo yanaonyesha kuwa mbinu ambazo humpa mwalimu umbele na kumpunguzia kazi mathalani kusoma kibinafsi, kusoma mhadhara na masaili ndizo hutumiwa zaidi kuliko zile ambazo humshirikisha mwanafunzi kama vile kusimulia hadithi, drama, mjadala na makundi hazitumiwi sana. Matokeo haya yanashadidia ukweli kwamba huenda matokeo duni katika ufahamu yanachangiwa na matumizi ya mbinu ambazo si bora.( tazama jedwali 4.2)

**Jedwali 4.2: Mara-idadi ya Matumizi ya Mbinu za Kufundishia (mwitiko wa walimu)**

| Mbinu | Mara kwa mara | Wakati mwingine | Haitumiwi kamwe | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Makundi | 6(33%) | 10(56%) | 2(11%) | 18(100%) |
| Masaili | 14(78%) | 4(22%) | 0(0%) | 18(100%) |
| Kusoma kwa sauti | 10(56%) | 3(17%) | 5(28%) | 18(100%) |
| Kusoma kibinafsi | 3(17%) | 14(78%) | 1(6%) | 18(100%) |
| Mhadhara | 10(56%) | 4(22%) | 4(22%) | 18(100%) |
| Kusimulia hadithi | 1(6%) | 6(33%) | 11(61%) | 18(100%) |
| Mbinu ya kidrama | 3(17%) | 5(28%) | 10(56%) | 18(100%) |
| Mjadala | 6(33%) | 4(22%) | 8(44%) | 18(100%) |

**Chanzo: Data kutokana na maswali ya hojaji**

Utafiti pia umelenga kukadiria mara-idadi ya matumizi ya mbinu za kufundishia ili kulinganisha na kuthibitisha miitiko ya walimu. Utafiti ulibainisha kuwa mbinu zinazotumiwa sana na walimu ni kusoma kwa sauti 110(61%), mhadhara 115(64%) na masaili 80(44%). Mbinu zisizopendelewa ni kusoma kibinafsi 22(12%), makundi 40 (22%), kusimulia hadithi 31 (17%), mbinu ya kidrama 35(19%) na mjadala 40(22%). Matokeo haya yanathibitisha madai ya walimu kuhusu mbinu zinazotumiwa mara kwa mara ambazo ni masaili, kusoma kwa sauti, kusoma kibinafsi na mhadhara huku mbinu ya kidrama, kusimulia hadithi na makundi kuonekana kutopendelewa jambo ambalo huenda limechangia hali ya wanafunzi kutoweza kuwa na utendaji bora katika kazi za somo la ufahamu**. (**tazama jedwali 4.3).

**Jedwali 4.3: Mara-idadi ya Matumizi ya Mbinu za Kufundishia (mwitiko wa wanafunzi)**

| Mbinu | Mara kwa mara | Wakati mwingine | Haitumiwi kamwe | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Makundi | 40 (22%) | 30(17%) | 110(61%) | 180(100%) |
| Masaili | 80(44%) | 48(27%) | 52(29%) | 180(100%) |
| Kusoma kwa sauti | 110(61%) | 25(14%) | 45(25%) | 180(100%) |
| Kusoma kibinafsi | 22(12%) | 145(81%) | 13(7%) | 180(100%) |
| Mhadhara | 115(64%) | 27(15%) | 38(21%) | 180(100%) |
| Kusimulia hadithi | 31 (17%) | 16(9%) | 133(74%) | 180(100%) |
| Mbinu ya kidrama | 35(19%) | 20(11%) | 125(69%) | 18(100%) |
| Mjadala | 40(22%) | 24(13%) | 116(64%) | 18(100%) |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

### 4.1.3 Stahabu za Wanafunzi Kuhusu Njia za Ufundishaji wa Ufahamu

Walimu na wanafunzi waliulizwa kukadiria kiwango cha kustahabu (kuvutiwa, kupendelea) mintarafu ya mbinu za kufundishia. Matokeo yalikuwa kama inavyoonyeshwa katika kielelezo 4.1 ilivyoripotiwa na walimu na wanafunzi.




**Kielelezo 4.1: Stahabu za wanafunzi kuhusu njia za ufundishaji wa ufahamu**

**Chanzo: Data kutokana na hojaji**

Kutoka na maoni ya watafitiwa, idadi kubwa ya walimu walioshiriki katika utafiti walieleza kuwa wanafunzi hupendelea kusoma kwa kibinafsi, kusoma kwa sauti, mhadhara na masaili. Kwa upande mwingine, wanafunzi hupendelea mbinu ambazo walimu hawatumii kila wakati wanaposoma ufahamu mathalani njia ya kidrama, kusimulia hadithi na mjadala. Kwa hivyo, kuna haja ya kujumuishwa kwa mbinu hizi ili kufundisha ufahamu licha ya kutopendwa na walimu wengi. Mukwa na Too (2014) wanasema kuwa walimu wanafaa kutumia mbinu ambazo zinawavutia wanafunzi kwa sababu ujifunzaji hutokea hasa palipo na kiwango cha juu cha ilhamu ya wanafunzi.

Ni muhimu kutilia mkazo mbinu za ufundishaji wa ufahamu ndipo usomaji wake uwe na manufaa kwa walengwa.Wasomi wengi wameangazia kuhusu mbinu tofauti tofauti

zinazoweza kutumiwa katika ufundishaji wa masomo ya lugha. Kwa mfano Quist (2000) na Savignon (2005), wamependekeza mikakati ifuatayo mahususi inayopaswa kuzingatiwa: kusoma kwa sauti ambapo walimu anaweza kuwasomea wanafunzi au mwanafunzi mmoja anaweza kusoma wengine wakisikiliza. Kusoma kwa sauti huwasaidia katika kujenga hali ya utulivu na usikivu. Aidha, huwasaidia wanafunzi katika kupenda lugha na kuhadithia hadithi inayosomwa.

Kusoma kwa sauti kukitumiwa pamoja na kusimulia hadithi, husaidia wanafunzi kuwa na hamu na kuibua ile hamu ya kusoma. Hadithi inaweza kusimuliwa na mwalimu kwa wanafunzi au mwanafunzi anaweza kusimulia wanafunzi wenzake wakisikiliza. Isitoshe, mbinu ya mjadala katika makundi hupanua ujifunzaji kwani wanafunzi hujadiliana kuhusu matini tofauti mbali na kila mmoja katika kikundi kugeuka wanapobadilishana majukumu. Majukumu haya ni kama msimamizi wa majadiliano, anayeandika muhtasari na atakayetoa ripoti ya waliyojadiliana. Inaonekana kuwa mbinu hizi hazitumiwi kwa upana na hali hii huenda inaathiri ufundishaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu, na kuchangia katika upataji wa matokeo duni katika eneo la utafiti.

### 4.1.4 Vigezo Vinavyotinga Uteuzi na Matumizi ya Mbinu

Walimu waliulizwa maswali kuhusu vigezo vinavyothibiti au kuathiri uteuzi na matumizi ya mbinu katika ufundishaji wa ufahamu darasani. Kielelezo 4.2 inaonyesha matokeo haya.

**Kielelezo 4.2: Vigezo vinavyotinga uteuzi na matumizi ya mbinu darasani**




**Chanzo: ukokotozi wa mtafiti**

Kulingana na matokeo, kazi nyingi ya mwalimu 18(100%) ndicho kigezo kikuu zaidi kinachozuia walimu kuteua na kutumia mbinu mwafaka katika ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu. Katika nafasi ya pili, kuna idadi kubwa ya wanafunzi 16(88%) ikifuatiwa na vipindi vichache vya kusoma 13(72%). Ushiriki mdogo wa wanafunzi na mielekeo ya wanafunzi pia ilionekana kuathiri uteuzi na matumizi ya Ufahamu mbinu za kufundishia kwa asilimia 67% na 50% mtawalia.

### 4.1.5 Athari za Matumizi ya Mbinu Zisizo Mwafaka Kufundishia

Walimu walipoulizwa kukadiria matokeo ya kutumia mbinu zisizo mwafaka kufundishia ufahamu darasani, matokeo duni ndiyo athari ya juu zaidi 14(78%) ikifuatiwa na ujenzi wa mielekeo hasi kwa upande wa wanafunzi 12(67%). Vilevile, ukosefu wa motisha upande wa wanafunzi pamoja na ushiriki uliodidimia wa walimu na wanafunzi katika somo zilitajwa kama athari kwa asilimia 10(56%) na 8(44%)

mtawalia. Hii inathibitisha maoni ya Ruddell (2002) kuwa ingawa walimu wengi wa lugha wamefuzu vyema na kuwa na uwezo wa kufundisha inavyostahili, wengi hawajizatiti kuweka mikakati bora ya kufundishia jambo ambalo linasababisha matokeo duni. Hii ni licha ya wao kufahamu kuwa mbinu wanazozotumia si bora**.** Tazama kielelezo Kielelezo 4.3

**Kielelezo 4.3: Athari za matumizi ya mbinu zisizo mwafaka**




**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

## 4.2 Nyenzo za Kufundishia

Dhamira kuu ya sehemu hii lilikuwa kutafuta majibu kwa lengo letu pili ambalo lilikuwa; kuchunguza uwepo na matumizi ya walimu ya vifaa vya kufundishia ufahamu wa Kiswahili na kubainisha iwapo vinaathiri ufundishaji na ujifunzaji wake. Vifaa katika ufundishaji wa ufahamu ni muhimu. Vifaa hivi vinapotumiwa vilivyo huwafanya wanafunzi kuelewa wanachofunzwa na kufurahia somo la ufahamu.

### 4.2.1 Uwepo wa Nyenzo za Kufundishia

Nyenzo za kufundishia huunda msingi mkuu wa somo lolote lile. Uwepo na matumizi ya nyenzo hufanikisha ufundishaji na hurahisisha kazi ya mwalimu. Mtafiti aligundua kwamba shule nyingi zilizoshiriki katika utafiti zilikosa nyenzo muhimu na za kutosha kufundishia ufahamu kama ilivyoonyeshwa katika. Jedwali 4.4.

Utafiti ulifichua kwamba shule nyingi zilikosa nyenzo za kimsingi za kufundishia ufahamu kwa viwango tofauti tofauti. Utafiti ulibainisha kuwa baadhi ya nyenzo muhimu sana zinazoweza kufaulisha ufundishaji wa ufahamu hazikupatikana kamwe katika shule zilizotafitiwa. Miongoni mwa nyenzo hizo ni pamoja na: maleba, mapiku, michongo, sanamu na mabango. Mtafiti aligundua kwamba licha ya nyenzo nyingine kupatikana, zilikuwepo kwa asilimia ndogo sana katika shule zilizohusishwa katika utafiti. Asilimia 11 walionyesha kuwa shule zao hurejelea mtandao huku asilimia 89 wakieleza kuwa hawatumii nyenzo hii.

Waalikwa na mafanani wanaweza kuwa wa manufaa sana katika ufundishaji wa ufahamu lakini utafiti huu ulifichua kwamba asilimia 28 pekee ya walimu huwaalika wataalamu muhimu huku asilimia 72 ya walimu wakionyesha kwamba hawawaaliki wataalamu hawa muhimu. Utafiti huu pia ulifichua kwamba asilimia 22 ya shule tafitiwa zina picha kama nyenzo za kufundishia ufahamu ikilinganishwa na asilimia 78 ya walimu katika shule zingine waliosema kuwa picha hazipatikana kama nyenzo za kufundishia ufahamu. Hali hii ilionyesha kuwa shule nyingi zilikosa picha na hivyo ni bayana kuwa hazitumiwi katika kufundishia ufahamu. Nyenzo nyingine iliyochunguzwa katika utafiti huu ilikuwa ni ya kanda za sauti. Matokeo yalibainisha

kwamba asilimia 22 ya shule zilikuwa na kanda za sauti ikilinganishwa na asilimia 78 ya shule zilizoikosa wakati wa ufundishaji wa ufahamu wa Kiswahili.

Isitoshe, utafiti ulifichua kwamba baadhi ya nyenzo zilipatikana kwa kiasi katika shule zilizotafitiwa. Nyenzo hizi ni pamoja na chati zilizopatikana kwa asilimia 39, michoro kwa asilimia 22, magazeti kwa asilimia 44, redio kwa asilimia 28, na vitabu vya marejeleo kwa asilimia 44. Asilimia zilizoonyeshwa za upatikanaji ziko chini ya wastani. Ni bayana kutokana na utafiti huu kwamba shule nyingi zilikosa nyenzo za kimsingi zinazoweza kutumiwa katika ufundishaji wa ufahamu wa Kiswahili.

Ufundishaji bora wa ufahamu unahitaji matumizi ya nyenzo nyingi zilizotajwa zinazokosekana katika shule nyingi ambazo mtafiti alitembelea. Ingawa baadhi ya nyenzo zinazoundwa viwandani kama runinga, tarakilishi na mtandao ni ghali, walimu wanapaswa kuunda na kukuza baadhi ya nyenzo zinazoweza kutengenezwa kama picha, michoro, maleba na kadhalika.

**Jedwali 4.4: Uwepo wa nyenzo za kufundishia.**

| **Nyenzo** | **Uwepo** | **Ukosefu** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Vitabu vya kiada | 12(67%) | 6(33%) | 18 (100%) |
| Vitabu vya ziada/marejeleo | 8(44%) | 10(56%) | 18 (100%) |
| Miongozo ya walimu | 13(72%) | 5(28%) | 18 (100%) |
| Silabasi | 16(89%) | 2(11%) | 18 (100%) |
| Kamusi | 15(83%) | 3(17%) | 18 (100%) |
| Runinga | 6(33%) | 12(67%) | 18 (100%) |
| Kinasa sauti | 4(22%) | 14(78%) | 18 (100%) |
| Redio | 5(28%) | 13(72%) | 18 (100%) |
| Filamu | 3(17%) | 15(83%) | 18 (100%) |
| Magazeti | 8(44%) | 10(56%) | 18 (100%) |
| Majarida | 9(50%) | 9(50%) | 18 (100%) |
| Tarakilishi | 8(44%) | 10(56%) | 18 (100%) |
| Maktaba | 9(50%) | 9(50%) | 18 (100%) |
| Chumba cha Kiswahili | 2(11%) | 16(89%) | 18 (100%) |
| Mtandao | 2(11%) | 16(89%) | 18 (100%) |
| Picha | 4(22%) | 14(78%) | 18 (100%) |
| Michoro | 4(22%) | 14(78%) | 18 (100%) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ubao | 18(100%) | 00 | 18 (100%) |
| Chati | 7(39%) | 11(61%) | 18 (100%) |
| Maleba na mapiku | 00 | 18(100%) | 18 (100%) |
| Michongo na sanamu | 00 | 18(100%) | 18 (100%) |
| Mabango | 00 | 18(100%) | 18 (100%) |
| Waalikwa na mafanani | 5(28%) | 13(72%) | 18 (100%) |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

### 4.2.2 Idadi ya Vitabu vya Kiada Shuleni Ikilinganishwa na Idadi ya Wanafunzi

Vitabu vya kiada hutekeleza jukumu kubwa katika kufanikisha ujifunzaji na ujifunzaji wa masomo ya lugha (Savignon, 2005). Uwepo wake, utoshelevu na matumizi yake ni vigezo ambavyo huathiri ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya lugha na hatimaye matokeo katika mtihani. Jedwali 4.7 linaonyesha kuwa shule nyingi zilizohusika katika utafiti zilikuwa na kiwango cha 1:2 cha idadi ya vitabu kwa idadi ya wanafunzi. Shule 12(67%) zilikuwa na kiwango hiki cha 1:2. Inawezekana kuwa hali hii inatokana na ruzuku ya karo ya serikali kwa shule za upili nchini Kenya. Hakuna shule hata moja iliyojitokeza kuwa na kiwango cha 1:5 kuendelea.

**Jedwali 4.5: Idadi ya vitabu kwa idadi ya wanafunzi**

| **Kiwango** | **Mara-idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| 1:1 | 3 | 17 |
| 1:2 | 12 | 67 |
| 1:3 | 2 | 11 |
| 1:4 | 1 | 6 |
| 1:5 | 00 | 00 |
| Jumla | 18 | 100 |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

### 4.2.3 Utoshelevu wa Vitabu vya Kiada

Walimu walipoulizwa kuhusu utoshelevu wa vitabu vya kiada kwa idadi ya wanafunzi wakati wa kufundisha ufahamu, walimu 16(89%) walisema kuwa kuna vitabu vya kiada vya kutosha kufundishia ufahamu huku 2(11%) wakisema hawana vya kutosha. Matokeo haya yanadhihirisha wazi kuwa kigezo cha utoshelevu wa vitabu hakiathiri ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu shuleni.

**Jedwali 4.6: Utoshelevu wa vitabu vya kiada**

| Utoshelevu | Mara-idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| Vinatosha | 16 | 89 |
| Havitoshi | 2 | 11 |
| Jumla | 18 | 100.0 |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

Kwa mujibu wa Muruguru (2000), kuna uhusiano mkubwa kati ya uwepo wa vitabu ambavyo ni nyenzo muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji na utendaji katika somo la lugha. Shule zenye vitabu vya kiada na ziada vya kutosha hupata matokeo mazuri kuliko zile zisizo na vya kutosha. Hata hivyo, kulingana na matokeo ya utafiti, suala la uwepo wa vitabu si changamoto katika somo la Kiswahili na hivyo haliathiri ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu.

### 4.2.4 Matumizi ya Nyenzo

Fauka ya kuwepo kwa nyenzo za kufundisha, mtafiti pia alitaka kujua namna ambavyo nyenzo hizi hutumiwa katika ufundishaji wa ufahamu wa Kiswahili. Katika utafiti, iligunduliwa kuwa walimu wengi hawakutumia nyenzo za kufundishia licha ya hali kwamba wengi wao wanafahamu umuhimu wake kutokana na mafunzo waliyopata vyuoni. Tarakimu zinaonyesha kuwa asilimia 100 ya walimu hutumia ubao na chaki kama nyenzo ya kufundishia. Vilevile, asilimia 94 hutumia zaidi vitabu vya kiada kama nyenzo za kufundishia. Aidha asilimia 6 ya walimu walionyesha kwamba hawatumii sana nyenzo hii.

Nyenzo nyingine ambayo ilitumiwa sana na walimu katika ufundishaji wa ufahamu ni kamusi. Utafiti huu ulionyesha kuwa asilimia 89 ya walimu walitumia nyenzo hii mara kwa mara ikilinganishwa na asilimia 6 waliosema huitumia wakati mwingine na kutoitumia kamwe mtawalia. Miongozo ya walimu ilitumiwa zaidi na asilimia 72 huku asilimia 17 wakisema kwamba hawakuitumia sana. Asilimia 11 ya walimu walionyesha kuwa hawaitumii kamwe nyenzo hii. Nyenzo nyingine iliyoonekana kutumiwa kwa kiwango kikubwa ni vitabu vya ziada/marejeleo kwa asilimia 67.

Licha ya ukosefu wa nyenzo nyingi za kufundishia, utafiti huu ulifichua kwamba hata chache zilizopatikana katika baadhi ya shule hazikutumiwa vizuri au hazikutumiwa kamwe na walimu wakati wa kufundishia ufahamu. Ukweli unaojitokeza ni kuwa walimu wengi hawatumii kamwe nyenzo mwafaka wakati wa ufundishaji ufahamu. Somo la ufahamu linahitaji nyenzo bora ndipo lieleweke vyema na hata kuwasisimua. Kulingana na matokeo ya utafiti, walimu wengi walikubali kuwa vitabu vya kiada, ziada, miongozo, silabasi, kamusi na ubao ndizo nyenzo zilizotumiwa sana nyakati za mafunzo ya ufahamu. Hata hivyo, vifaa vya teknolojia ya kisasa kama vile redio, runinga, filamu na vinasa sauti havikutumiwa kamwe. Kwa hivyo, ni thibitisho tosha kuwa walimu wengi wana dhana ya uasilia kuwa ubao, vitabu vya kiada na ziada ndivyo vinaweza kuwa na uwasilishaji murua wa ufahamu. Tazama jedwali 4.7

**Jedwali 4.7: Mara-idadi ya matumizi ya nyenzo**

| **Nyenzo** | **Mara kwa mara** | **Wakati mwingine** | **Haitumiwi kamwe** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| Vitabu vya kiada | 17(94%) | 1(6%) | 00 | 18 (100%) |
| Vitabu vya ziada/marejeleo | 12(67%) | 4(22%) | 2(11%) | 18 (100%) |
| Miongozo ya walimu | 13(72%) | 3(17%) | 2(11%) | 18 (100%) |
| Silabasi | 11(61%) | 2(11%) | 5(28%) | 18 (100%) |
| Kamusi | 16(89%) | 1(6%) | 1(6%) | 18 (100%) |
| Runinga | 4(22%) | 3(17%) | 11(11%) | 18 (100%) |
| Kinasa sauti | 2(11%) | 4(22%) | 12(67%) | 18 (100%) |
| Redio | 5(28%) | 5(28%) | 8(44%) | 18 (100%) |
| Filamu | 3(17%) | 4(22%) | 11(11%) | 18 (100%) |
| Magazeti | 9(50%) | 4(22%) | 5(28%) | 18 (100%) |
| Majarida | 8(44%) | 5(28%) | 4(22%) | 18 (100%) |
| Tarakilishi | 3(17%) | 3(17%) | 12(67%) | 18 (100%) |
| Maktaba | 5(28%) | 6(33%) | 7(39%) | 18 (100%) |
| Chumba cha Kiswahili | 2(11%) | 1(6%) | 15(83%) | 18 (100%) |
| Mtandao | 4(22%) | 4(22%) | 10(56%) | 18 (100%) |
| Picha | 9(50%) | 5(28%) | 4(22%) | 18 (100%) |
| Michoro | 8(44%) | 4(22%) | 6(33%) | 18 (100%) |
| Ubao | 18(100%) | 00 | 00 | 18 (100%) |
| Chati | 6(33%) | 2(11%) | 10(56%) | 18 (100%) |
| Maleba na mapiku | 1(6%) | 8(44%) | 9(50%) | 18 (100%) |
| Michongo na sanamu | 2(11%) | 5(28%) | 11(11%) | 18 (100%) |
| Mabango | 3(17%) | 4(22%) | 12(67%) | 18 (100%) |
| Waalikwa na mafanani | 4(22%) | 5(28%) | 9(50%) | 18 (100%) |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

Walimu katika shule zilizoshirikishwa katika utafiti hutumia vifaa tofauti kama inavyoonyesha katika jedwali 4.5. Walimu waliulizwa maswali kuhusu changamoto au vigezo vinavyothibiti (kuathiri) uteuzi na matumizi ya mbinu katika ufundishaji wa

ufahamu darasani. Kielelezo 4.5 kinaonyesha matokeo haya. Kwa mujibu wa Kamau (2015), matumizi ya nyenzo ni kigezo muhimu kinachoathiri matokeo katika mtihani wa Kiswahili. Hii ni kutokana na sababu kuwa nyenzo huwezesha mwanafunzi kubwia mafunzo kwa wepesi kutokana na hali kuwa nyenzo huhuisha dhana ambazo hukaa dhahania kwa wanafunzi.

### 4.2.5 Changamoto Zinazotinga Matumizi ya Nyenzo

Matokeo ya kielelezo 4.6 yanaonyesha kuwa bei ghali ya vifaa vya kusomesha ufahamu ilikuwa changamoto katika ufundishaji ilivyoripotiwa na idadi kubwa ambayo ni asilimia 94 ya walimu. Haya yaonyesha kuwa shule zinahitaji mikakati mwafaka katika bajeti ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia ili kujumuishwa kwa matokeo kabambe ya Kiswahili. Changamoto zingine zilizoripotiwa ni ukosefu wa rasilmali kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi kwa asilimia 89, vipindi vichache na kazi nyingi ya mwalimu.

**Kielelezo 4.2.Vigezo vinavyotinga uteuzi na matumizi ya mbinu darasani**




**elezo 4.4: Vigezo vinavyotinga uteuzi na matumizi ya nyenzo darasani**

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

Walimu walitaja changamoto nyingine kwamba kulikuwa na uzembe wa kutafuta nyenzo, muda wa kujitayarisha na kutafuta nyenzo haukuwepo kwani muda ni mfupi. Wengine walidai kuwa wanafanya kazi nyingi sana ambazo hazikuwaruhusu kutafuta nyenzo kwani walipewa vipindi vingi vya Kiswahili na masomo mengine kama vile Historia, Jiografia, Hisabati na Dini. Isitoshe, wengine walitaja hali ya kupuuza majukumu ambapo walisema kuwa hawakuona haja ya kuteua nyenzo za kufunzia na kujifunzia somo la ufahamu wa kusoma.

Ni dhahiri kwamba matumizi ya nyenzo huchangia katika ufanisi wa kufundisha Kiswahili. Wambui na Nyacomba (2002) wanatoa kauli kwamba ni vyema kutumia nyenzo na kuzielewa kadri unavyozirejelea. Mwalimu anaweza kueleza dhana fulani katika lugha kwa urahisi atumiapo nyenzo na uelewekaji wa dhana ukafaulu. Nyenzo halisi huibua motisha na husaidia katika uelewekaji wa msamiati kwa urahisi mno. Wanafunzi hushika na huona na kuweza kurudiarudia utendaji huo, hapo basi uelewekaji ukawa rahisi na kuweza kukumbukwa vyema. Nyenzo halisi zikilinganishwa na dhana husika huwa rahisi kueleweka kuliko kubuni jambo katika ubongo (Kamau, 2015). Mwalimu huzungumza kwa uchache na mwanafunzi ndiye mtenda kazi. Utendaji kazi unahimizwa katika mfumo mpya wa elimu. Wanafunzi

ya Walimu Kuhusu wawe wavumbuzi wanapoingiliana na nyenzo katika somo.

### 4.3 Maandalizi Ufundishaji wa Ufahamu wa Kiswahili

Sehemu hii inashughulikia lengo letu la tatu ambalo ni maandalizi ya walimu. Imegawika katika sehemu mbili: maandalizi nyanjani na darasani.

### 4.3.1 Maandalizi ya Walimu Nyanjani

Kufanikiwa au kufaulu kwa mpango au mradi wowote kunahitaji maandalizi bora ya mapema. Shughuli hizi hupanua uwezo wa mwalimu wa kuifasiri silabasi na hata utendaji halisi darasani (Moseti 2003). Ilikuwa muhimu katika kazi hii kujua maandalizi ambayo walimu walifanyiwa nyanjani kuhusu ufundishaji wa ufahamu. Maandalizi ya nyanjani aliyotaka kujua mtafiti yalihusu mahudhurio ya kazi mbalimbali baada ya mwalimu kufuzu masomo ya chuo kikuu au chuo kingine. Kozi walizoulizwa walimu zilikuwa ni kozi za kupiga msasa, semina warsha na simposia. Mtafiti alitaka kupata taarifa kuhusu mafunzo haya mintarafu ya changamoto za ufunzaji na ujifunzaji wa ufahamu wa kusoma.

Tarakimu za matokeo zilifichua kuwa, walimu 7(39%) walikuwa wamehudhuria warsha mbili au tatu. Walimu 11(61%) walikataa kwamba hawakupata matayarisho yoyote nyanjani. Wengi wa walimu waliohojiwa walisema kwamba hawakuwahi kupata mawasiliano yoyote kuhusu shughuli za kitaaluma kama vile semina, warsha na simposia kuhusu ufundishaji wa masuala ibuka.

Hali hii inaonyesha udhaifu katika maandalizi ya walimu nyanjani kumaanisha kuwa kuna changamoto. Matokeo haya ni kinyume cha ushauri wa Goble na Porter (1977) na Muruguru (2000) kuwa kozi za kupiga msasa huwa nzuri kwa kujaza pengo walimu wanapogundua upungufu wowote. Ujifunzaji wa maarifa mapya yanayotokana na maendeleo katika uwanja fulani, huwezekana kupitia semina, warsha na kozi mbalimbali za kupiga msasa.

Kwa wale waliokuwa wamehudhuria warsha au semina mtafiti alitaka kujua aliyegharamia mafunzo hayo na wasimamizi walikuwa akina nani. Ilibainika wazi kuwa walimu 10(56%) waligharamia mafunzo hayo kisha walimu 8(44%) walilipiwa na shule, wizara ya elimu haikuhusika katika kugharamia mafunzo yoyote ya somo la Kiswahili.

Jambo hili lilionyesha udhaifu kwani, wizara ya elimu ndiyo ilitakikana kuwajibika katika kuyashughulikia mafunzo ya walimu ya kupiga msasa. Hali kadhalika, ilibainika kuwa, wasimamizi wa warsha na semina za walimu wa Kiswahili, baadhi yao hawakuwa wataalamu wa Kiswahili, wengi wao walikuwa wachapishaji wa vitabu. Kulingana na maoni ya baadhi ya walimu, warsha hizo zilishughulikia tu vitengo vichache vya somo la Kiswahili zaidi ya vingine.

Miitiko ya walimu wote 18(100%) ilifichua kuwa sehemu ya somo la Kiswahili iliyopewa kipaumbele ilikuwa inahusu uchambuzi wa vitabu viteule vya fasihi. Somo la ufahamu halikupewa uzingativu katika mafunzo ya nyanjani. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa kuna changamoto kuhusu jinsi somo la ufahamu lilishughulikiwa katika warsha. Utafiti wa Peters (1980) ulionyesha kuwa, maarifa hubadilika kulingana na wakati au kuibuka kwa mambo mapya. Maandilizi ya nyanjani basi husaidia kutekeleza ufundishaji wa mambo mapya na kuvuta kumbukumbu ya yale yaliyosahaulika. Hivyo basi mapendekezo ni kuwa, walimu wote wawe wakihudhuria warsha, semina ama kozi za kupiga msasa ili waweze kujifunza maarifa mapya ama kuvuta kumbukumbu ya yaliyosahaulika.

**Kielelezo 4.5: Mahudhurio ya warsha na semina**




**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

### 4.3.2 Mchango wa Maafisa Wadhibiti Ubora na Viwango wa Elimu.

Maafisa wadhibiti ubora wa elimu wana jukumu la kushauri na kuelekeza walimu kuboresha ufundishaji wao. Mtafiti katika kazi hii alitaka kujua iwapo walimu walitembelewa na maafisa hawa ili kutoa ushauri kuhusu ufundishaji wa ufahamu wa Kiswahili. Mtafiti aligundua kwamba ni walimu 5 (asilimia 28 ya walimu) waliosema wamewahi kutembelewa na maafisa hao huku 13 (asilimia 72) wakidai kwamba hawajawahi kutembelewa na maafisa hao.

Walimu wote 30 walipoulizwa kukadiria mchango wa maafisa hawa kuhusu namna ya ufundishaji wa masuala ibuka, walimu 4 (asilimia 22) walisema kuwa mchango wao ni wa kuridhisha, walimu 3 (asilimia 17) walisema ni wa wastani ilhali walimu 11 (asilimia 61) walisema si wa kuridhisha. Miitiko hii imewasilishwa katika Jedwali 4.7 hapa chini.

**Jedwali 4.8: Makadirio ya Ushauri wa Maafisa Wadhibiti Ubora na Viwango wa Elimu.**

| **Makadirio** | | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| A | Wa kuridhisha | 4 | 22 |
| B | Wastani | 3 | 17 |
| C | Usioridhisha | 11 | 61 |
| | Jumla | 18 | 100 |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

Matokeo haya yanaonyesha kwamba maafisa hao hawajatekeleza wajibu wao inavyopasa hasa ikikumbukwa kwamba silabasi mpya inayosisitiza ufundishaji kwa mwelekeo mseto inahitaji maelekezo na ushauri mwingi. Hali ya kukosekana kwa maafisa hawa huenda imechangiwa na ukosefu wa maafisa wa kutosha ikifahamika kwamba idadi ya walimu inazidi kuongezeka. Aidha, huenda kukawa na maafisa ambao wanazembea kazi.

### 4.3.3 Maandalizi ya Walimu Darasani

Maandalizi ya mwalimu katika sehemu hii ni yale ambayo mwalimu anafanya akiwa shuleni. Matayarisho haya humwezesha mwalimu kuwa na utaratibu bora anapotekeleza wajibu wake darasani.

**Jedwali 4.9: Matumizi ya stakabadhi za kujifunza na kufundishia**

| Stakabadhi | Mara kwa mara | Wakati mwingine | Haitumiwi | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| Maazimio ya kazi | 5(28%) | 3(17%) | 10(56%) | 18(100%) |
| Andalio la somo | 1(6%) | 1(6%) | 16(89%) | 18(100%) |
| Rekodi ya kazi | 5(28%) | 3(17%) | 10(56%) | 18(100%) |
| Matini ya somo | 6(33%) | 2(11%) | 10(56%) | 18(100%) |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

Pollard (2002) anaeleza kuwa maazimio ya kazi humjumlishia mwalimu kile ambacho anatakiwa kufunza kwa wakati gani na namna gani ya kutathimini yaliyofunzwa. Maazimio ya kazi ni mojawapo ya hatua za mwanzo za mwalimu kujiandaa kufundisha darasa fulani. Maazimio yakiwa na upungufu wowote katika sehemu fulani, upungufu utamwandama mwalimu hadi darasani na hivyo hatafundisha vyema. Matokeo ya utafiti katika jedwali 4.9 yanaonyesha kuwa ni asilimia 28 tu ya walimu ndiyo iliyokiri kutumia maazimio ya kazi huku asilimia 56 ikisema kuwa haikuitumia stakabadhi hii kamwe. Rekodi ya kazi ni stakabadhi nyingine muhimu ambayo mwalimu anatakiwa awe nayo. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, rekodi za kazi zilijazwa na walimu 5(28%) huku walimu 10(56%) wakisema kuwa hawakujaza rekodi hizi.

Andalio la somo ndilo linalomuongoza mwalimu katika hatua zinazofuatana. Katika andalio la somo mwalimu huongozwa kuhusu njia za kufundishia, hatua za kufundishia somo, vitabu vya kutumia, muda wa kutumia kwa somo zima na hata

tathmini ya somo. Hivyo basi andalizi la somo ni dira ambayo humuongoza mwalimu anapokuwa akifundisha somo. Utafiti ulifichua kwamba, idadi kubwa ya walimu wa Kiswahili waliokuwa wakifunza somo la ufahamu 16(89%) hawakuona umuhimu wa stakabadhi hii na hivyo hawakuandaa andalio la somo. Walipohojiwa walijitetea kwamba somo la ufahamu wa kusoma halikuhitaji andalio la somo kwani lilihusisha kusoma tu na kujibu maswali.

## 4.4 Maoni ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Somo la Ufahamu

Utafiti huu pia ulichunguza maoni ya wanafunzi na walimu kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu kama lengo la nne la utafiti huu kwa sababu hii inaweza kuathiri matokeo katika mtihani (Babusa, 2010).Mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu ufunzaji wa ufahamu wa kusoma ilikadiriwa katika sehemu hii. Mtafiti alilenga kupata jibu kwa swali hili: Ni nini mielekeo ya walimu na wanafunzi wa shule za upili kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu? Sehemu hii imegawika katika vitengo vidogo vidogo vinavyokadiria mielekeo ifuatavyo.

### 4.4.1 Manufaa ya Somo la Ufahamu

Ni bayana kwamba, watekelezaji na wavumbuzi wanaweza kuathiri ufanisi wa jambo fulani. Hawes (1979). Utekelezaji wa mtaala hushirikisha hatua nyingi ikiwemo hatua ya kubadili mitazamo na mielekeo ya walimu. Hali hii imechangiwa pia na Gross na wenzake (1971) wanaosema kuwa walimu wanahitaji kuwa na mtazamo chanya kuhusu uvumbuzi ili kuweza kujitolea wakati wao na bidii katika hatua zao za utekelezaji

Kulingana na matokeo kwenye jedwali 4.10, walimu wote 18(100%) walikubali kuwa ufahamu huelimisha na kuhamasisha wanafunzi na vilevile kukuza stadi za lugha huku 17(94%) wakikiri kuwa ujumbe uliomo katika ufahamu hutekeleza udhibiti wa

kijamii kwani huhusu masuala ibuka yanayoathiri jamii kama vile magonjwa sugu, ugaidi, jinsia na mazingira. Walimu 15(83%) walikubali kuwa ufahamu huburudisha wanafunzi na kupitia kusoma kwa burudani, wanafunzi hatimaye hupata na kuelewa ujumbe.

**Jedwali 4.10: Maoni ya Walimu**

| **Manufaa** | **Ndio** | **La** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Jukumu la burudani | 15(83%) | 3(17%) | 18(100%) |
| Jukumu la kuelimisha na kuhamasisha | 18(100%) | 0(0%) | 18(100%) |
| Kukuza stadi za lugha | 18(100%) | 0(0%) | 18(100%) |
| Udhibiti kijami | 17(94%) | 1(6%) | 18(100%) |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

Wanafunzi wengi 172 (96%) na 168 (93%) wanatambua kuwa ufahamu una jukumu muhimu la kukuza stadi zao za lugha pamoja na kuwaelimisha na kuwahamasisha kuhusu masuala ya kijamii mtawalia. Hata hivyo, asilimia 50 wanasema ujumbe uliomo kuhusu masuala ibuka katika jamii ya kisasa unaweza kuwadhibiti kijamii huku asilimia nyingine 50 ikisema ujumbe huu hauwezi kutekeleza jukumu hilo. Wanafunzi 85 (47%) wanaonelea kuwa ufahamu huwapa burudani mbali na kuwaelimisha.

**Jedwali 4.11: Maoni ya Wanafunzi**

| **Manufaa** | **Ndio** | **La** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Jukumu la burudani | 85(47%) | 95(53%) | 180(100%) |
| Jukumu la kuelimisha na kuhamasisha | 168(93%) | 22(7%) | 180(100%) |
| Kukuza stadi za lugha | 172(96%) | 18(4%) | 180(100%) |
| Udhibiti kijamii | 90(50%) | 90(50%) | 180(100%) |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

### 4.4.2 Kupenda Somo la Ufahamu

Hata hivyo, licha ya walimu kutambua umuhimu wa ufahamu kwa wanafunzi, utafiti katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi uliashiria kwamba, walimu wa Kiswahili wana mtazamo hasi kuhusu ufunzaji wa ufahamu wa kusoma. Walimu waliulizwa ikiwa walifurahia kufundisha somo la ufahamu wa kusoma. Walipewa vibadala viwili (i) Ndiyo (ii) La ili kila mmoja achague.

**Jedwali 4.12: Maoni ya Walimu**

| **Mielekeo ya walimu** | **Idadi** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| La | 10 | 56% |
| Ndiyo | 8 | 44% |
| Jumla | 18 | 100% |

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Walimu 10 (56%) walichagua (la) ilhali 8 (44%) walichagua (ndiyo). Swali liliendelezwa kwa kuwauliza watoe sababu za kufurahia au kutofurahia somo la

ufahamu wa kusoma. Walimu waliosema kuwa walifurahia kufundisha ufahamu walitoa sababu za kufurahia ambazo ni kwamba, somo hili lilihusu ukuzaji wa stadi za lugha, liliwashirikisha wanafunzi zaidi kuliko masomo mengine ya Kiswahili, walipokuwa wakisoma mada za ufahamu zenye mnato.

Walimu waliosema kuwa hawakufurahia kufunza ufahamu walitoa sababu zifutazo: mada za ufahamu hazikuvutia na mara nyingi walipatia wanafunzi wang’ang’ane nazo kivyao, wanafunzi hawawapatii motisha kwani huwa hawamalizi kazi na pia hawayajibu maswali ya ufahamu vyema, somo la ufahamu wa kusoma lilikuwa na alama 15 pekee na kutokana na hali kwamba wana kazi nyingi za kutekeleza ili kukamilisha silabasi, hawangepoteza muda sana kushughulikia ufahamu. Sababu hizo zinadhihirisha kuwepo kwa changamoto ya mielekeo kwa vile tunaona kuwa idadi kubwa ya walimu 10(56%) walisema kuwa hawakufurahia kufundisha somo la ufahamu wa kusoma.

Urevbu (1999) anatambua mielekeo ya walimu kuwa muhimu kuliko maudhui katika ufunzaji wa vipengele vya lugha. Maoni yake Urevbu ni mwafaka kwa sababu mwalimu ni kiungo maalum katika ufundishaji, kwa hivyo mwelekeo wake ni muhimu. Mwalimu anapaswa awe na mwelekeo chanya kwani ndio huchangia ubora wa utendaji. Aidha ushupavu wake mara nyingi hutokana na yaliyomo katika fikra zake (Collins& Nind 2002)

**Jedwali 4.13: Maoni ya Wanafunzi**

| Mielekeo ya wanafunzi | Idadi | Asilimia |
|---|---|---|
| La | 130 | 72% |
| Ndiyo | 50 | 28% |
| Jumla | 180 | 100% |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

Swali jingine lilihusu mielekeo ya wanafunzi kuhusu somo la ufahamu wa kusoma. Wanafunzi waliulizwa ikiwa walifurahia somo la ufahamu wa kusoma wakapewa vibadala viwili ili mmoja achague. Vibadala hivi vilikuwa: Ndiyo na La. Wanafunzi wengi 130(72%) walionyesha kuwa na mwelekeo chanya kuhusu somo la ufahanu kwa kuitikia kuwa wao hufurahia kusoma ufahamu. Ni matarajio ya mtafiti kuwa mwelekeo huu unafaa kudhihirika kupitia matokeo bora katika mtihani wa ufahamu.

Wanafunzi waliodai kutofurahia somo la ufahamu waliwalaumu walimu kwa kusema kuwa, hawakusahihisha kazi zao mara kwa mara, hawakuwapatia maelezo na tena, walimu mara nyingi walitumia muda wa somo la ufahamu kufunzia vipengele vingine vya lugha kama vile sarufi na fasihi. Wanafunzi waliokiri kufurahia somo la ufahamu walitoa sababu kuwa somo hilo lilihusika na masuala ibuka tofauti tofauti yanayowahamasisha pamoja na kuwa vifungu vya ufahamu huwa chanzo cha burudani kwao.

Mtafiti vilevile aliwataka wanafunzi kukadiria mielekeo yao kuhusu kauli mbalimbali zinazohusiana sehemu ya ufahamu katika somo la Kiswahili kwa jumla. Kauli saba

zilitolewa na wanafunzi wakaulizwa kuchagua mojawapo. Majibu hayo yalifuata mpangilio ufauatao: kubali kabisa (KK), kubali (KU) siwezi kuamua (SA), sikubali (SI) na sikubali kabisa (SK). Mtafiti aliwataka wanafunzi waonyeshe maoni kuhusu kauli mballimbali. Jedwali 4.12 linaonyesha kauli hizi na matokeo ya makadirio ya wanafunzi.

**Jedwali 4.14: Maoni Kuhusu Ufahamu kwa Jumla**

| Kauli | KK | KU | SA | SI | SK | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Sehemu ya ufahamu ni fupi na huchukua muda mfupi kusoma | 24(13%) | 42(23%) | 8(4%) | 56(31%) | 50(28%) | 180(100%) |
| Sehemu ya ufahamu husisimua | 78(43%) | 80(44%) | 0(0%) | 15(8%) | 7(4%) | 180(100%) |
| Ufahamu ni sehemu ninayofurahia zaidi kusoma | 70(39%) | 97(54%) | 0(0%) | 13(7%) | 10(6%) | 180(100%) |
| Vifungu vya ufahamu huakisi maisha ya kisasa | 67(37%) | 74(41%) | 3(2%) | 34(19%) | 12(11%) | 180(100%) |
| Sifurahii kukosa vipindi vya somo la ufahamu | 66(37%) | 78(43%) | 0(0%) | 19(11%) | 17(9%) | 180(100%) |
| Sehemu ya ufahamu inafaa kuondolewa kwa Kiswahili | 24(13%) | 13(7%) | 6(3%) | 100(56%) | 37(21%) | 180(100%) |
| Ufahamu ni mgumu kuelewa | 39(22%) | 23(13%) | 15(8%) | 53(29%) | 50(28%) | 180(100%) |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

Wanafunzi wengi 56 (31%) walisema kuwa hawapendi ufahamu kwa sababu vifungu huwa virefu na hivyo huchukua muda kusoma. Hata hivyo, wanafunzi 100 (56%) hawangependa sehemu ya ufahamu kuondolewa kwenye mtihani wa Kiswahili. Hii inatokana na wengi wao 80 (44%) kusema kuwa wanapenda sehemu ya ufahamu kwa vile huwa na makala yanayoyosisimua na hivyo 97 (54%) yao hufurahia zaidi kusoma hii sehemu kuliko sehemu nyingine katika somo la Kiswahili. Wanafunzi 74 (41%) walisema yaliyomo katika ufahamu huakisi masuala ibuka katika maisha ya kisasa huku 78 (43%) wakisema kuwa hawangefurahia kukosa vipindi vya somo la ufahamu.

Matokeo yanadhihirisha kuwa wanafunzi wana mwelekeo chanya kuhusu ufahamu wa Kiswahili na wanaipenda sana sehemu hii katika somo la Kiswahili. Hivyo basi, kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya utabia, ni jukumu la mwalimu kuongoza kila tukio darasani; kuwaelekeza wanafunzi kwa kutayarisha mazingira, kuteua mada inayofaa, kuandaa nyenzo na kufundishia. Jukumu la mwanafunzi ni kufuata maagizo. Hii ni safari ambayo mwalimu ataisafiri pamoja na wanafunzi wake ili kupata matokeo mema katika mtihani wa ufahamu. Hii ni kutokana na hali kwamba kuna uhusiano kati ya mielekeo ya wanafunzi na utendaji wao katika somo husika. Hunsen (1977) anasema kuwa, wanafunzi wenye mielekeo chanya kuhusu somo hupata alama za juu kuliko wale wenye mielekeo hasi. Vile vile, wanafunzi wenye mielekeo chanya kuhusu somo hilo, hutumia muda wao mwingi sana kufanya mazoezi katika somo hilo.

### 4.4.3 Changamoto Zinazokabili Ufunzaji na Ujifunzaji wa Ufahamu

Watafitiwa walipewa kauli na kuulizwa kubainisha iwapo kauli hizo ni changamoto zinazokabili ufunzaji na ujifunzaji wa ufahamu wa Kiswahili katika shule za upili na kupendekeza jinsi zinavyoweza kutatuliwa.

Jedwali 4.13 linaonyesha maoni ya walimu. Matokeo haya yanaonyesha kuwa mbinu mbovu za kufundishia ni changamoto kubwa inayokabili ufunzaji na ujifunzaji wa ufahamu. Walimu 14 (78%) waliunga mkono kauli hii. Kwa upande mwingine, upungufu na ukosefu wa nyenzo za kufundishia ilidhihirishwa na walimu 16 (89%) huku maandalizi mabovu yakionekana kuwa changamoto kutokana na walimu 10 (56%) waliounga mkono kauli hii. Hii inaonyesha kuwa walimu wengi waliingia darasani kufunza ufahamu bila maandalizi kabambe wakichukulia kuwa ufahamu ni kusoma tu. Kazi nyingi ya mwalimu ni changamoto iliyoitikiwa na walimu 16 (89%) nao walimu 15 (83%) wakisema ukosefu wa muda wa kutosha uliwafanya wapuuze kufundisha ufahamu na kuegemea sehemu nyingine mathalani fasihi, insha na sarufi ambazo ni sehemu wanazoona zinabeba alama nyingi kuliko ufahamu ambao unabeba alama 15 tu. Walidai kuwa wanafanya kazi nyingi sana ambazo hazikuwaruhusu kujiandaa kwa kutafuta nyenzo na kutumia mbinu bora za ufundishaji kwani walipewa vipindi vingi vya Kiswahili na masomo mengine kama vile Historia, Jiografia, Hisabati na hata somo la Dini. Hatimaye, mielekeo hasi ya walimu ilidhihirika kuwa changamoto kubwa kulingana na walimu 14 (78%) waliokiri kuwa ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu huathiriwa pakubwa na changamoto hii.

**Jedwali 4.15: Maoni ya Walimu**

| Kauli | Ni changamoto | Si changamoto | Jumla |
|---|---|---|---|
| Mbinu mbovu za kufundishia | 14(78%) | 4(22%) | 18(100%) |
| Upungufu na ukosefu wa nyenzo za kufundishia | 16(89%) | 2(11%) | 18(100%) |
| Maandalizi mabovu ya walimu | 10(56%) | 8(44%) | 18(100%) |
| Kazi nyingi ya mwalimu | 16(89%) | 2(11%) | 18(100%) |
| Ukosefu wa muda wa kutosha | 15(83%) | 3(17%) | 18(100%) |
| Mielekeo hasi ya walimu | 14(78%) | 4(22%) | 18(100%) |

**Chanzo: Ukokotozi wa Mtafiti**

Wanafunzi 89 (49%) walisema kuwa mbinu za ufundishaji si changamoto huku 124 (69%) wakikiri kuwa upungufu na ukosefu wa matumizi ya nyenzo ndiyo changamoto kubwa. Wanafunzi wengi 167 (93%) walisema kuwa upungufu na ukosefu wa vitabu vya kiada si changamoto huku wanafunzi 99 (55%) wakitaja mielekeo hasi ya wanafunzi kuhusu ufahamu kuwa changamoto. Tazama jedwali 4.14

**Jedwali 4.16: Maoni ya Wanafunzi**

| **Kauli** | **Ni changamoto** | **Si changamoto** | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| Mbinu mbovu za kufundishia | 89(49%) | 91(51%) | 180(100%) |
| Upungufu na ukosefu wa matumizi ya nyenzo za kufundishia | 124(69%) | 56(31%) | 180(100%) |
| Upungufu na ukosefu wa vitabu vya kiada | 13(7%) | 167(93%) | 180(100%) |
| Ushiriki mdogo wa wanafunzi katika somo | 78(57%) | 102(43%) | 180(100%) |
| Mielekeo hasi ya walimu | 99(55%) | 81(45%) | 180(100%) |

**Chanzo: Ukokotozi wa mtafiti**

### 4.4.4 Mapendekezo ya Suluhisho

Watafitiwa waliulizwa kupendekeza suluhisho kwa changamoto zilizobainishwa. Walimu 16 (89%) walipendekeza kuwa kuboresha matumizi ya mbinu na nyenzo wanazotumia kufundishia ufahamu kutasaidia kutatua baadhi ya changamoto zinazokabili somo hili huku walimu 18 (100%) wakisema kuwa kuwapunguzia walimu kazi pamoja na kuimarisha mafunzo nyanjani ya kuwapiga msasa kutasaidia pakubwa kusuluhisha changamoto zinazokabili somo hili.

**Kielelezo 4.6 Mapendekezo ya Walimu**




**Chanzo: Matokeo ya Utafiti.**

Swali liliulizwa wanafunzi pia kutoa mapendekezo yao kuhusu jinsi wangependa somo la ufahamu wa kusoma lifunzwe ili waweze kulifurahia. Wanafunzi walitoa mapendekezo yafuatayo: Wanafunzi 30 (15%) walisema walimu watumie nyenzo wanapofundisha somo la ufahamu wa kusoma. Wanafunzi 70 (35%) walipendelea shule ziweze kununua vitabu vya kutosha. Wanafunzi 40 (20%) walipendekeza kwamba walimu wawe wakitoa maelezo kabla ya somo na pia wawe wakisahihisha kazi za wanafunzi. Wanafunzi 60 (30%) walipendekeza kuwa walimu waweze kubadilishabadilisha mbinu za kufunzia.

**Kielelezo 4.7: Mapendekezo ya Wanafunzi**




**Chanzo: Matokeo ya utafiti**

### 4.5 Hitimisho

Sura hii imeeleza mambo yaliyozingatiwa katika uchanganuzi na uwasilishaji wa data. Yaliyoshughulikiwa ni matumizi ya mbinu za kufundishia ufahamu, uwepo na matumizi ya nyenzo za kufundishia ufahamu, maandalizi ya walimu nyanjani na kabla ya kuingia darasani, mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu ufunzaji na ujifunzaji wa ufahamu pamoja na changamoto zinazokabili ufunzaji na ujifunzaji wa somo hili na mapendekezo ya suluhisho kwa hizo changamoto.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Utafiti huu umekusudia kuchunguza masuala yanayoathiri ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi nchini Kenya. Tasnifu hii imekamilishwa kwa sura tano. Katika sura ya kwanza, utafiti umezingatia usuli wa suala la utafiti, suala la utafiti, madhumuni na maswali ya utafiti, misingi ya uteuzi wa mada, umuhimu wa utafiti, misingi ya kinadharia na upeo wa utafiti.

Sura ya pili imetalii maana na umuhimu wa ufundishaji wa ufahamu, michakato katika usomaji wa ufahamu, mambo yanayoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu wa kusoma katika Kiswahili mintarafu ya mbinu za kufundishia, nyenzo za kufundishia ufahamu, maandalizi ya mwalimu na maoni ya walimu na wanafunzi kuhusu ufahamu.Katika sura ya tatu, muundo na mbinu za utafiti zimejadiliwa. Sura ya nne nayo imewasilisha na kuchanganua data kuhusu matumizi ya mbinu za kufundishia, uwepo na matumizi ya nyenzo za kufundishia ufahamu, maandalizi ya mwalimu nyanjani na kabla ya kuingia darasani pamoja na maoni au mielekeo ya walimu na wanafunzi kuhusu ufunzaji na ujifunzaji wa ufahamu. Sura ya tano inahusu muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo

Utafiti huu ulidhamiria kutimiza malengo manne ya utafiti. Malengo hayo yameshughulikiwa ifuatavyo:

### 5.2.1 Mbinu za Kufundishia Ufahamu

Katika hojaji za walimu, wengi wao wamedai kuwa walitumia mbinu mbalimbali katika ufundishaji wa sarufi. Miongoni mwa mbinu walizotaja zilikuwa mbinu ya makundi, kusoma kwa sauti, maswali na majibu na mhadhara. Wengi walitumia mbinu ya kusoma kwa sauti na kupuuza mbinu nyingine zinazohusisha tajriba ya mwanafunzi kama vile kusimulia hadithi, mjadala na mbinu ya kidrama. Claessen (1994) anasema mbinu ya usomaji kwa sauti si bora kwa ufunzaji wa ufahamu kwa vile hupunguza kasi ya usomaji na kupunguza uelewaji wa ujumbe.

Anasema mbinu hii yafaa zaidi katika kufunza stadi za kusikiliza na kuzungumza. Claessen anapendekeza matumizi ya mbinu mbalimbali za kufundishia lakini anasisitiza zaidi matumizi ya kusoma kibinafsi. Kwa mujibu wa Muya (2012), kuna haja ya walimu kuchanganya matumizi ya mbinu za ufundishaji kwani hakuna mbinu moja iliyo bora kuliko nyingine. Isitoshe, kwa vile kila darasa huwa na wanafunzi wenye sifa tofauti tofauti, matumizi ya mbinu tofauti tofauti huwawezesha wanafunzi wenye sifa tofauti tofauti kuelewa mafunzo.

Hata hivyo, anasisitiza matumizi ya mbinu ziazowashirikisha wanafunzi kama vile uigizaji, makundi, mjadala, masaili na masimulizi. Kulingana na matokeo ya utafiti, wanafunzi wengi wanastahabu matumizi ya hizi mbinu ambazo ni shirikishi kuliko zile zinazopendelewa na walimu jambo ambalo huenda lilichangia pakubwa hali duni ya matokeo ya somo la Kiswahili katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi kwani wanafunzi hawawezi kufanikiwa katika somo la ufahamu ikiwa hawatashirikishwa katika somo.

Kama wanavyoshadidia Allwright na Bailey (1991) mtagusano kati ya msikilizaji na mzungumzaji huimarisha ujifunzaji lugha. Ellis (1994) pia anasema kuwa mtagusano

wa mwalimu na mwanafunzi huathiri ujifunzaji wa vipengee vya lugha na huwapa msamiati wa kutumia wakati wa mazungumzo. Hali hii itawezekana tu kwa matumizi ya mbinu shirikishi.

Baadhi ya walimu wamedai kuwa hawakuweza kushirikisha mbinu tofauti kwa sababu walikumbwa na changamoto kama vile: vipindi vichache vilivyotengewa somo la Kiswahili, silibasi pana inayompa mwalimu wa Kiswahili kazi nyingi, na idadi kubwa ya wanafunzi madarasani mwao. Miongoni mwa walimu walioshirikisha mbinu tofauti katika ufundishaji walidai kukumbwa na matatizo ya ukosefu wa motisha au mielekeo hasi miongoni mwa wanafunzi kuhusu ufahamu.Wanafunzi walidhihirisha hali ya kuwa na mielekeo hasi kuhusu somo la ufahamu hasa kwa kutoyajibu maswali ya ufahamu wakati wa mitihani ya mwisho wa mihula kwa kuiruka sehemu hiyo na hata walipopewa mazoezi ya kila mara ambayo walistahili kufanya darasani.

Hali hii ilitokana na udhaifu wa walimu katika kuyatekeleza majukumu yao walipokuwa wakifundisha somo la ufahamu kwa kutotumia mbinu mwafaka za kufundisha somo hilo, kwa kuyapuuza matumizi ya vifaa vya kufundishia, na hata kwa kutojiandaa kikamilifu kama vile kwa kutengeneza stakabadhi maalum ambazo ni ratiba za kazi pamoja na maandalio ya somo. Kulingana na matokeo ya utafiti huu, ni dhahiri kuwa masuala hayo yote ndiyo yaliochangia katika kudorora kwa ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu katika shule za upili za kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi.

Licha ya changamoto hizi imebainika wazi kuwa ni muhimu kushirikisha mbinu tofauti zitakazowapa wanafunzi nafasi ya kuelewa somo la ufahamu kwa urahisi ili kuimarisha utendaji katika mitihani ya Kiswahili mbali na kujenga umilisi ufahamu

wao wa mazingira halisi ya maisha na jamii kwa jumla. Mbinu za kufundishia kama mbinu ya mhadhara na zile zisizomshirikisha mwanafunzi katika somo la ufahamu zisihusishwe kamwe katika ufunzaji wa somo hilo ili kuzuia kuwakinahisha wanafunzi wa somo la Kiswahili.

### 5.2.2 Nyenzo za Kufundishia Ufahamu

Matumizi mwafaka ya vifaa katika kufundishia lugha hasa ufahamu huimarisha kuelewa kwa sheria za kisarufi, msamiati, maudhui na mwishowe kuimarisha umilisi wa lugha na utendaji katika mitihani (Gathumbi na Masembe, 2005; Johnson 1995).

Kwa mujibu wa Saunders (1974), tajriba ndio msingi mkuu katika hatua za ujifunzaji. Anataja kuwa mtu hukumbuka asilimia 10 ya yale anayoyasikia, asilimia 50 ya yale anayosikia na kuona na asilimia 90 ya yale anayoyasikia, kuona na kutenda. Saunders (1974) anahitimisha kwa kusema:

> Nikisikiacho, hukisahau
> Nikionacho, hukikumbuka
> Na nikitendacho, hukibwia milele (Tafsiri yangu).

Kwa hivyo, ufundishaji unaofaa unastahili kuyahusisha zaidi matumizi ya vifaa vya ufundishaji ambavyo humshirikisha mwanafunzi. Kuwepo kwa vifaa vya ufundishaji huruhusu matumizi ya mbinu nyingi za ufundishaji ambazo huleta matokeo bora.

Licha ya ukweli huu, matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa kulikuwa na uhaba wa vifaa vya kufundishia ufahamu na hivyo, wengi wa walimu waliegemea matumizi ya vitabu vya kiada. Fauka ya utafiti kubainisha kuwa shule nyingi zilikuwa na utoshelevu wa vitabu vya kiada, ilibainika pia kuwa shule nyingi hazikuwapa wanafunzi fursa ya kusoma matini yaliyomo maktabani ili kuimarisha usomaji, sheria za sarufi, msamiati na ufahamu wa maudhui au masuala ya jamii utakaowawezesha kuboresha utendaji wao katika somo la ufahamu na hatimaye Kiswahili kwa ujumla.

Umuhimu wa usomaji wa mapana kwa kuimarisha utendaji katika masomo ya lugha unaungwa mkono na Bright na McGregory (1970).

Halikadhalika, imebainika kuwa wengi wa walimu walitumia sana ubao na chaki kufundishia somo la ufahamu. Gathumbi na Masembe (2005) wanasema kuwa hizi ni mbinu zilizozoeleka katika ufunzaji na ujifunzaji wa lugha na inabidi walimu wawe wabunifu na wafaraguzi ili kuteua na kutumia nyenzo. Wanasema kuwa walimu wanafaa kutumia nyenzo zinazorahisisha ufunzaji na ujifunzaji, zinazomshirikisha mwalimu na mwanafunzi katika mchakato mzima wa ufunzaji na ujifunzaji, zinazoamsha ilhamu ya mwanafunzi katika somo pamoja na kuuchochea ubunifu wa mwanafunzi wa soma la lugha.

Muya (2012) anasema walimu wanafaa pia kuhusisha nyenzo za kisasa za kielektroniki katika ufunzaji wao. Nyenzo hizi ni kama vile runinga, redio, filamu, tarakilishi na mtandao. Ufunzaji bora wa ufahamu unahitaji matumizi ya nyenzo nyingi zilizotajwa zinazokosekana katika shule nyingi ambazo mtafiti alizitembelea. Halikadhalika, walimu walibainisha kuwa kulikuwa na uzembe wa kutafuta nyenzo, kukosa muda wa kujitayarisha na kutafuta nyenzo kwani muda ni mfupi. Pia, walidai kuwa wanafanya kazi nyingi sana ambazo hazikuwaruhusu kutafuta nyenzo kwani walipewa vipindi vingi vya Kiswahili na masomo mengine. Changamoto nyingine ni ya kupuuza majukumu ambapo walimu wengi hawakuona haja ya kuteua nyenzo za kufunzia na kujifunzia somo la ufahamu wa kusoma.

Japo walimu na wanafunzi walisema kuwa redio na tarakilishi ni nyenzo mwafaka katika ufundishaji, ilibainika kwamba nyenzo hizi zilitumika kwa nadra sana. Wote walisema kuwa zilikuwa ghali mno na pia wanafunzi wengi walizihusisha na burudani. Walisema pia kuwa redio haikuruhusu mtagusano wa moja kwa moja huku wakidai tarakilishi ilikuwa na ugumu wa kutumia. Ingawa baadhi ya nyenzo

zinazoundwa viwandani kama runinga, tarakilishi na mtandao ni ghali, walimu wanapaswa kuwa wafaraguzi katika kuunda na kukuza baadhi ya nyenzo zinazoweza kutengenezwa kama picha, michoro, maleba na kadhalika kwani ufunzji na ujifunzaji hauwezi kufanikiwa kamwe bila walimu kutumia nyenzo zinazofaa.Matokeo ya utafiti huu yanatuonyesha kuwa hali duni katika utendaji wa walimu na wanafunzi wa somo la Kiswahili katika kaunti Ndogo ya Kisumu Magharibi ilitokana na hali ile ya walimu kutotumia nyenzo walipokuwa wakiendeleza ufundishaji wao wa somo la ufahamu hali ambayo huenda ilichangia katika wanafunzi kutekeleza mielekeo hasi kuhusu somo hilo.

### 5.2.3 Maandalizi ya Walimu Kuhusu Ufundishaji wa Ufahamu

Ili kupanua uwezo wa mwalimu wa kuifasiri silabasi na hata kuimarisha utendaji halisi darasani, shughuli za kitaaluma kama vile warsha, semina, simposia ni muhimu (Muruguru, 2000; Moseti, 2003). Ufichuzi unaotokana na utafiti huu ni kwamba shughuli za kitaaluma za kuwapiga msasa walimu kuhusu ufundishaji wa ufahamu licha ya ripoti ya KNEC kuonyesha kuwa ufundishaji katika sehemu hii ni wa kutilia shaka hazikuandaliwa vyema na Wizara ya Elimu. Matokeo yalionyesha kuwa asilimia kubwa ya walimu walioshiriki katika utafiti hawakupata matayarisho yoyote wakiwa nyanjani kuhusu ufundishaji wa masuala ibuka katika Kiswahili,kama vile ugaidi, magonjwa na hata mashambulizi jambo ambalo limechangia kwa kina hali ya somo la ufahamu katika Kaunti hii kudorora.

Baadhi ya walimu waliohojiwa walisema kwamba hawakupata mwaliko wala mawasiliano yoyote yale kuhusu shughuli za kitaaluma. Hali hii ni ya kusikitisha ikifahamika kwamba, aidha, kwa wale waliohudhuria walibainisha kuwa, baadhi ya

wasimamizi wa warsha, semina na simposia za walimu wa Kiswahili hawakuwa wataalamu wa Kiswahili. Wengi wao walikuwa wachapishaji wa vitabu waliolenga mauzo kuliko kufaa walimu. Kulingana na maoni ya baadhi ya walimu, warsha hizo zilishughulikia tu vitengo vichache vya somo la Kiswahili hasa uchambuzi wa vitabu vya fasihi kuliko vitengo vingine kama vile sarufi, isimu jamii, ufupisho na ufahamu.

Ili kutekeleza mtaala kwa njia iliyo bora, maelekezo bora na ushauri wa Maafisa wadhibiti wa Ubora wa Elimu na Viwango unahitajika. Ni ajabu sana katika uchunguzi huu kwamba ni asilimia ndogo sana ya walimu waliotembelewa na maafisa hao. Ni dhahiri kutokana na data hii kwamba walimu wengi hawakupata ushauri au mwongozo wowote kutoka kwa maafisa Wadhibiti Ubora wa Elimu na Viwango. Aidha utafiti ulibainisha kuwa walimu wengi hawakuridhika na ushauri ambao maafisa hawa hutoa kuhusu ufahamu na ufundishaji wake.

Inabainika wazi hapa kuwa Wizara ya Elimu imelegea katika utekelezaji wa majukumu yake. Ni hatari kwamba huenda ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu usipate mwongozo inavyostahiki iwapo Maafisa Wadhibiti Ubora wa Elimu na Viwango hawatatekeleza jukumu lao kikamilifu. Matokeo haya yote kwa ujumla yanazidi kubainisha kwamba wengi wa washika dau ambao ni walimu hawakuandaliwa vyema kuhusu utekelezaji wa mafunzo ya ufahamu. Iwapo walimu hawana msingi thabiti wa jinsi ya kuushughulikia ufahamu wa Kiswahili, ni vigumu sana ujifunzaji na ufunzaji kufanyika kikamilifu.

Fauka ya hayo, utafiti pia ulilenga kubainisha maandalizi na matumizi ya stakabadhi zinazotumika kuelekeza ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu. Matokeo yamebainisha kwamba, ingawa walimu walionyesha kutumia maazimio ya kazi,

rekodi ya kazi na matini ya somo kuliko andalio la somo, kiwango cha matumizi bado hakikuridhisha kwani yote yalikuwa chini ya asilimia 30. Matumizi ya stakabadhi hizi huwa na uhusiano wa moja kwa moja na ufanisi katika ufundishaji kwani huimarisha ufunzaji na ujifunzaji kisha husababisha matokeo bora katika somo hili. Maandalizi na matumizi yake hudhihirika kwani utafiti wetu umebainisha kuwa, shule zinazofanya vyema katika mitihani ya kitaifa hudhihirisha ushahidi wa matokeo mema. Hali ni kinyume kwa shule ambazo walimu wake hawaandai stakabadhi hizi (Moseti, 2003) kwani matokeo huwa duni.

Kiwango cha chini cha matumizi ya stakabadhi hizi ni kinyume na mafundisho wanayopokea walimu vyuoni ambapo umuhimu wa stakabadhi hizi husisitizwa. Matumizi mabovu ya stakabadhi katika eneo la utafiti yalichangia matumizi mabovu ya mbinu na nyenzo katika ufunzaji wa somo la ufahamu na hivyo, ufundishaji na ujifunzaji duni wa ufahamu. Hivyo basi, ni muhimu kwa walimu wa Kiswahili kuandaa na kutumia stakabadhi hizi ili kuboresha na kufanikisha ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu.

### 5.2.4 Maoni ya Walimu na Wanafunzi Kuhusu Somo la Ufahamu

Mwalimu anapaswa awe na mwelekeo chanya kwani ndio huchangia ubora wa utendaji. Aidha ushupavu wake mara nyingi hutokana na yaliyomo katika fikra zake (Collins & Nind 2002). Maoni yake Urevbu (1999) ni kuwa mwalimu ni kiungo maalum katika ufundishaji na hivyo mwelekeo wake ni muhimu. Licha ya walimu wengi kutambua umuhimu wa kufunza na kujifunza ufahamu, utafiti ulibainisha kuwa walimu wengi wana mwelekeo hasi kuhusu utekelezaji wa somo hili darasani. Wengi wanatoa sababu kama vile somo la ufahamu wa kusoma lilikuwa na alama 15 pekee ikilinganishwa na vipengee vingine katika Kiswahili mathalani sarufi na fasihi. Kwa

hivyo wanasema kuwa kutokana na hali kwamba wana kazi nyingi za kutekeleza ili kukamilisha silabasi, hawangepoteza muda sana kushughulikia ufahamu.

Sababu hizo zinadhihirisha kuwepo kwa changamoto ya mielekeo kwa upande wa walimu na hii huathiri utendaji wao kwa njia hasi katika somo la ufahamu na mwishowe kuathiri ujifunzaji na utendaji wa wanafunzi. Matokeo haya ni ya kuhofisha kwani ufundishaji wa ufahamu hauwezi kufanikiwa ikiwa wadau wakuu hawawezi kuifurahia kazi yao. Mwelekeo huu si wa kutia moyo kwa sababu mwelekeo hasi wa walimu huathiri ufunzaji wao darasani. Mwelekeo huathiri sana utekelezaji wa jambo lolote lile na hivyo basi ugunduzi huu ulionyesha kuwa ufundishaji wa ufahamu ni wa kutilia shaka na huenda malengo ya kufundisha ufahamu yasitimizwe.

Kwa upande mwingine kutokana na maoni ya wanafunzi, mielekeo hasi imedhihirika. Mielekeo ya wanafunzi ni muhimu katika kufaulu kwa malengo yoyote katika elimu (Wambui & Nyacomba, 2002). Wataalamu hawa wanasema kuwa motisha ya wanafunzi huwa muhimu sana katika mradi wowote wa elimu au mafunzo kwani wanafunzi walio na mielekeo chanya kuhusu suala lolote la kielimu huwa tayari na wenye hamu kubwa ya kujifunza suala hilo. Hivyo basi, mwalimu anafaa kuhakikisha kuwa mwanafunzi ameshirikishwa na kuelekezwa vyema katika mchakato wa somo la ufahamu ili kufanikisha ujifunzaji. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa wanafunzi wengi wana mielekeo chanya kuhusu ufahamu na hivyo wanapenda somo hili. Licha ya haya, wenye mwelekeo hasi wanapaswa kushughulikiwa ili wasiathiri utendaji katika somo la Kiswahili kwa jumla. Hii inatokana na hali kwamba kuna wale wanafunzi wanaochukulia kwamba ufahamu ni mgumu na hivyo unapaswa kuondolewa kwenye silabasi.Wanapopewa zoezi la ufahamu wengi wao huliruka

swali hilo na kushughulikia maswali mengine yasiyohusika na ufahamu kwani wao hushindwa kuyajibu maswali.

**5.3 Hitimisho**

Baada ya kuchanganua data ya utafiti, mambo mbalimbali yalifichuka.Utafiti ulibainisha kwamba, walimu hawakutumia njia mwafaka za kufundisha somo la ufahamu wa kusoma ila walifunza somo hilo kiholela na kusahau kuwa, ufunzaji na ujifunzanji bora wa ufahamu wa kusoma ulihitaji njia mwafaka za kufunzia. Pia, ilibainika kwamba walimu hawakutumia nyenzo zozote isipokuwa kitabu cha kiada ambacho walikitumia kufundishia somo la ufahamu wa kusoma jambo ambalo linachangia katika kuathiri ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu wa kusoma. Wanafunzi hawakufunzwa vizuri somo la ufahamu, walibwagiwa kazi bila kupewa maelezo, mara nyingine hawakufunzwa somo la ufahamu wa kusoma kwani vipindi vyake vilitumika kufunzia vipengele tofauti vya Kiswahili mbali na wanafunzi kutopewa mazoezi ya ufahamu ya kutosha na kazi zao kutosahihiswa.

Vilevile, ilibainika kuwa walimu wa Kiswahili katika shule za Sekondari hawakuhudhuria kozi za nyanjani za kuwapiga msasa, na pia kozi zilizoandaliwa ziliegemea tu upande wa fasihi na vitengo vingine tofauti na ufahamu. Utafiti pia ulifichua kwamba walimu wengi wa shule za Sekondari hawakujitayarisha kikamilifu walipokuwa nyanjani na hata walipokuwa darasani wakifundisha,baadhi yao walienda kufundisha somo la ufahamu bila kutumia stakabadhi mwafaka zilizohitajika. Mwisho kabisa, kutokana na maoni ya walimu  utafiti ulifichua kuwa mielekeo yao kuhusu utekelezaji wa somo la ufahamu darasani ilikuwa hasi, hali ambayo huathiri ufundishaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu. Hata hivyo, maoni ya wanafunzi yamedhihirisha mielekeo yao kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu

wa kusoma ambayo ilikuwa chanya, hali ambayo inafaa kuimarishwa na walimu kwani itaboresha utendaji wa wanafunzi katika mitihani.

### 5.4 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tunapendekeza kuwa, walimu waimarishe mbinu wanazotumia. Mbinu hizi ziwe ni zile zinawashirikisha wanafunzi zaidi. Miongoni mwa mbinu hizi ni mbinu ya makundi, mijadala, uigizaji na masimulizi ambazo huimarisha umilisi wa sheria za lugha, msamiati, maudhui na utendaji katika lugha. Katika mbinu zote mwalimu awe mwelekezi huku wanafunzi wakiwa ndio kiini cha ufundishaji na ujifunzaji.

Matumizi ya nyenzo hufanikisha ufundishaji wa ufahamu na hivyo kuimarisha umilisi wa lugha na utendaji katika somo hilo. Kwa hivyo, inapendekezwa kuwepo na matumizi ya nyenzo tofauti na za kutosha ili kufanikisha ufundishaji wa ufahamu. Walimu wahakikishe kuwa nyenzo hizi zimetumika kwa njia ifaayo. Isitoshe, inapendekezwa pia kuwepo na kipindi cha matumizi ya maktaba katika ratiba ya ufundishaji ili kuwahimiza wanafunzi kusoma matini yatakayowaongezea umilisi wa sarufi, msamiati na maudhui ambao utaimarisha utendaji wao katika somo la ufahamu. Matumizi ya mtandao, runinga, tarakilishi na redio yanapendekezwa katika shule nyingi ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa ufahamu wa Kiswahili.

Kuna tafiti ambazo zimeonyesha kuwa mielekeo chanya kuhusu ujifunzaji wa vipengee vya lugha huimarisha umilisi na utendaji katika lugha hiyo ilhali mielekeo hasi hudidimiza umilisi na utendaji huo (Babusa, 2010; Njuguna, 2002). Kwa hivyo ni muhimu walimu wa Kiswahili wawasaidie wanafunzi kujenga mielekeo chanya kuhusu somo la ufahamu na Kiswahili kwa jumla ambayo ni lugha ya kitaifa, rasmi

na ya kimataifa. Hii itaboresha utendaji wa wanafunzi katika mitihani hasa watakapokuwa wakijibu swali la ufahamu.

Wizara ya elimu iweze kufuatilia na kuchunguza namna walimu wanavyofunza shuleni kwa kuhakikisha kwamba walimu wanatayarisha stakabadhi zote zinazohitajika, wanatumia njia mwafaka wanapofundisha, wanatumia nyenzo mwafaka ili utekelezaji wa kufundisha somo la Kiswahili ambalo somo la ufahamu wa kusoma ni kipengele kimojawapo ukamilike kwa minajili ya matokeo bora ya mitihani ya kitaifa. Aidha warsha, semina na symposia ziandaliwe na KICD kwa ushirikiano na wataalam wa lugha ili kuimarisha ufundishaji wa somo la Kiswahili na vipengele vyake.

Kwa kufanya hivi walimu watapata maarifa ambayo yataondoa kuchanganyikiwa na kuchangia katika uelekezi bora kwa wanafunzi mbali na kujenga mielekeo chanya ya walimu kuhusu somo la ufahamu. Maafisa Wadhibiti Ubora wa Elimu na Viwango washirikiane na KICD kuelekeza na kuamsha ari ya walimu ya kutumia nyenzo kufunza, kutumia mbinu mwafaka na kujiandaa vyema kabla ya kuingia darasani kufundisha somo la Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yatakuwa ya manufaa mno katika kuimarisha ufunzaji na ujifunzaji wa somo la Ufahamu.

### 5.5 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi

Mtafiti hawezi kudai kuwa ameshughulikia mambo yote kuhusu masuala yote yanayoathiri ufundishaji na ujifunzaji wa somo la. Itakuwa bora zaidi ikiwa utafiti wa aina hii utafanywa katika maeneo mengine nchini. Utafiti huo unaweza kuwa wa mlinganisho ambapo matokeo katika maeneo mengine yanaweza kulinganishwa ili kubainisha hali halisi ya mambo yanayoathiri ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufaham.

Utafiti kama huu vile vile unaweza kufanywa katika shule za msingi nchini Kenya ili kubaini hali halisi kuhusu mambo yanayoathiri ufunzaji na ujifunzaji wa somo la ufahamu wa kusoma katika Kiswahili. Utafiti ufanywe kubainisha sababu zinazofanya walimu kuandaa stakabadhi za kufundishia ufahamu wa Kiswahili kama vile andalio la somo, maazimio ya kazi na rekodi ya kazi huku wengine wakikosa kuandaa stakabadhi hizi.

Mwisho, kwa vile utafiti huu ulifanywa kwa wanafunzi wa kidato cha tatu pekee katika kaunti ndogo ya Kisumu Magharibi, ipo haja ya utafiti mwingine kufanywa katika vidato vingine katika maeneo mengine nchini ili kuyalinganisha na matokeo haya na kubaini hali halisi kuhusu ufahamu na mambo yanayoathiri ufundishaji na ijufunzaji wake.

# MAREJELEO


Allwright, D. & Bailey, K. (1991). *Focus on the Language Classroom: An Introduction for Language Teachers*. New York: Cambridge University Press.

Ayot H.O. (1986). *Economics of education*. Nairobi: Education Research and Publication.

Babusa, H. (2010). *Uchanganuzi Linganuzi wa Mielekeo na Umilisi wa Lugha ya Kiswahili wa Wanafunzi katika Mikoa ya Pwani na Nairobi Nchini Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu *ya* Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Baker, C. (1992). *Attitudes and Language*. Philadelphia: Multilingual Matters Ltd.

Brian, A. (1975). *Social Research Methods.* New York: Oxford University Press Publishers Ltd.

Benaars, G. A., Otende, J. E., & Boisevert, B. R. (1994). *Theory and Practice of Education.* Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Brown, H. D. (2007). *Principles of Language Learning and Teaching* (5$^{th}$ Ed.) White Plains: New York: Pearson Education.

Bindra, S. (2007). *Why Kenyans are not Reading.* Sunday Nation, August 26, 2007. Nairobi.

Bright, J.A. & Mc Gregory, P. (1970). *Teaching English as a Second Language*. Essex: Longman Group Limited.

Chacha, S. (2016). *Uhusiano wa Mikakati ya Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili na Umilisi wa Kusoma Katika Shule za Msingi, Kasarani, Kaunti ya Nairobi, Kenya*: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Claessen, A. (1994). *How Important is Where You Start? Early Mathematics Knowledge and Later School Success.* Teacher College Record, 115(6), 1-29.

Collie, J. & Slater, S. (1987) *Literature in Language Classroom. Cambridge:* Cambridge University Press.

Collins, J. & Nind, M. (2002). *Manifesto for Learning: Fundamental Principles*. London : Continuum.

Davis, P.M. (1990). *An Evaluation of Journal-published Research on Attitudes in Reading, 1900- 1977*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Tennesse, Knoxvile. (Haijachapishwa).

Dewey, J. (1916). *Democracy and Education: An Introduction to the Philosophy of Education*. New York:The Macmillan Company.

Deodutus,R. (2015).Nadharia za Awali katika uamiliaji wa Lugha ya pili kutoka www.ac.edu.Toleo la 6/11/2018.

Ellis, R. (1994). *Current Issues in the Teaching of Grammar: An SLA Perspective*. Tesol Quarter. Oxford : Oxford University Press.

Ellis, R. (I997). *Instructed Second Language Acquisition*. Oxford: Basil Blackwell Ltd.

Elliot, D. & Woodward, A. (1990). *Textbook and Schooling in the United States*.(90TH ed). Chicago: Chicago University Press.

Eshiwani, G.S. (1993). *Education in Kenya Since Independence*. Nairobi: East African Educational Publishers Limited.

Fullan, M. (1990). *The Meaning of Educational Change*. London: Casselle Educational Company.

Gagne, R.M. (1985). *The Conditions of Learning.* New York: Holt: Holt Rinehart and Winston.

Gathumbi, A. na Masembe, S. (2005). *Principles and Techniques in Language Teaching*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Gekombe, C. (2015). *Factors affecting teaching. of Kiswahili Comprehension in Secondary Schools*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi Edoret. (Haijachapishwa).

Githinji, D. G. (2017). *School Factors Influencing Instruction of Kiswahili Grammar in Public Secondary Schools in Baringo Central Sub-County Kenya*. Eldoret: Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Moi Eldoret. (Haijachapishwa).

Goble, N. M & Porter, F. (1977). *The Changing Role of the Teacher: International Perspective*. London: UNESCO.

Good, C. (1972). *Essentials of Education: Research Methodology and Design*. New York: Meredith Corporation.

Gross, D. & Clark, F. (1971). *Organizational Climate for Change in Schools.* Towards Innovativeness. From https://www.tandfonline.com. Retrieved, Thursday, 21st June 2018.

Halliday, M.A. (1973). *Explorations in the Functions of Language*. London: Edward Arnold.

Hegenhann, B. R. (1997). *An Introduction Media* (AIMS): An issue in Educational Technology.17, No. 2.

Hawes, H. (1979). *Curriculum and Reality in African Primary Schools.* Harlow: Longman Press.

Heyneman, S. (1981). *Textbooks and Achievement in Developing Countries*: Journal of Curriculum Studies. Juzuu. 13, No. 3. Pg. 227-246

Hunsen, J. (1977). *International Study of Achievent in Mathematics. A Comparison of twelve Countries.* Juzuu 1. Johan Wiley and Sons.

Hurst, C. & Johns O. (2004). *Carol Hurst's Children Literature Site.* Retrieved from: http//www//carolhurst.com 13.6.2018.

Ihebuzor, N. A. (1986*). Appropriate Instructional Media (AIMS): An Issue in Educational Technology in the Nigerian School System*. British Journal of Educational Technology - 17 ( 2). Mei 1986.

Ipara, O. I. (2006).*Matatizo ya Kufundishia Fasihi Simulizi katika Shule za Upili Katika Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza Communication na CHAKITA.

Johnson, D. (1995*). Investing in Teacher Effectiveness to Improve Educational Quality in Developing Countries: Does In-service Education for Primary Mathematics Teachers in Sri Lanka Make a Difference to Teaching and Learning*? Research in Comparative and International Education Journal. 1 (1) 73 (87.

Kamau, H. (2015). *Tathmini ya Matumizi ya Vifaa vya Kufundishia Msamiati wa Kiswahili Katika Shule za msingi za Umma, Kaunti ya Kisumu Mashariki, Kenya.* Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kerlinger, F.N. (2004). *Research Foundations of Behavioural*. New Delhi: Holt Rinehalt and Winston.

KICD, (2014). *Summative Evaluation of the Secondary School Curriculum*. Nairobi: Kenya Institute of Education.

K.I.E, (2002*). Kiswahili Sekondari. Mwongozo wa Walimu*. Nairobi: Taasisi ya Elimu.Kenya.

K.I.E, (2006). *Kiswahili Sekondari Mwongozo wa Walimu.* Nairobi: Taasisi ya Elimu. Kenya.

Kilemi, M. na Wamahiu, S.P. (1995). *Issues in Educational Research in Africa.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Kimani, J. N. (2015). *Uhusiano wa Mbinu za Kufundisha Sarufi na Umilisi wa Mazungumzo ya Wanafunzi wa Sekondari, Kaunti Ndogo ya Thika Magharibi, Kenya.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kimble, G.A. (1961). *Hilgard and Marquis Conditioning and Learning* (2nd Edition). New York: Appleton-Century-Crofts.

Kimui, V.W. (1988). *A Study of Availability and Use of the Learning and Teaching Resources in Primary Teacher's Colleges in Kenya.* Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Kiragu, F.W. (1986). *A Study of Factors that Affect Achievement for Mathematics at Secondary School Level in Kenya.* Kenyatta University, Seminar Paper No. 201:79.

K.N.E.C. (2016). *Examination Report*, Nairobi: Government Printers.

Kothari, K.H. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi: Vishwa

Krashen, S.D. (1982). *Principles and Practice in Second Language Acquisition*. Oxford: Perganon

Lighbown, P. na Spada. (1990). *Focus on Form and Corrective Feedback in Communicative Language Teaching: Effects on Second Language Learning*. Cambridge: Cambridge University Press.

Linderman, R. H. (2001). *Educational Measurements*. Illinois. Scott. Foremanand Company.

Littlewood, W.T. (1981). *Foreign and second language learning*. Cambridge, United Kingdom: Cambridge University Press.

Mackay, W.F. (1986). *Language Teaching Analysis*. Edinburgh: T and A. Constable. LTD.

Maloba, M. M. (2008). *A Study of Influence of Students' Attitude Towards Learning Kiswahili on Their Performance Among Secondary Schools in Rachuonyo Sub-County, Kenya*. M. Phil. Thesis, Moi University.(Unpublished).

Mbuthia, F.K. (1996). *A comparative study of effect of two Instructional Approaches on Students Performance in Kiswahili Poetry in Selected Secondary Schools in Eldoret Municipality.* Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).

.

Miricho, M. (2008). *Distinction Kiswahili for Primary Teacher Education.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mirikau, S. (2008). *Msururu wa PTE: Kiswahili kwa Vyuo vya Ualimu*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Momanyi, C. (2007). *Nafasi ya Lugha ya Kiswahili katika Elimu ya Vyuo Vikuu Nchini Kenya.* katika Njogu K.(Mh.). Nairobi: Twaweza Communications.

Molusa, T. (1992*). Innovation in Education*.New York: Teachers College Press.

Mpesha, N. (1995). *Children's Literature in Tanzania: A Literary Appreciation of its Growth and Development.* Tasnifu ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Mugenda, M., & Mugenda, G. (1999). *Research methods.* Nairobi: African Centre for Technology Studies (ACTS).

Mugenda, O .M & Mugenda, A.G. (2003). *Qualitative and Quantitative Approaches.* Nairobi: Acts Press

Mukwa, C.W. & Too, J. (2014). *General Instructional Methods.* Moi University Press. Eldoret.

Mukwa, J. (2014). *Education Communication and Technology*. Nairobi*:* UON.

Muruguru, S. K. (2000). *Students' Performance in Kiswahili: A Study of Selected Schools in Nakuru Sub-County*. Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).

Musau, P.M. & Chacha, L. (2001). *Mbinu za Kisasa za kufundishia Kiswahili*. Nairobi: K.L.B.

Mutai, B.K. (2000). *How to Write Quality Research Proposal: A Complete and Simplified Recipe*. New York: Thelley Publication.

Muya, D. (2012). *Mbinu na Mikakati ya Kufundishia Kiswahili.* Taifa Leo, Nairobi: Nation Media Group. Toleo la 02.03.2012.

Moffet, J. na Wegner (1992). *Active Voice: A writing Programme Across the Curriculum*. (2nd Ed). Bynton Cook, Portsmouth.

Moseti, O. (2003). *Walimu Wachunguzwe*. Taifa Leo. Nairobi: Nation Media Group. Toleo la 27/7/2003.

Mwangi, P. K. (1985). *Uhusiano Uliopo Kati ya Mitazamo ya Lugha ya Wanafunzi wa Kidato cha Nnena Utendaji wao Katika Tarafa ya Maseno*. Tasnifu ya M.Phil. Moi University. (Haijachapishwa).

Mwaura, T. (2013). *Fasihi na Lugha.* Taifa Leo. Nairobi: Nation Media Group. Toleo la 29.08.2013.

Ndalu, A. (2008). *Mwangaza wa Kiswahili*. Nairobi: East African Educational Publishers

Newman, L. (1994). *Social Research Methods: Qualitative and Quantitaive Approaches*.London: Library of Cataloging-in-Publication Data.

Njogu, K. (2011). *Kiswahili kwa Vyuo vya Walimu*. The Jomo Kenyata Foundations. Kenya.

Njuguna, N. (2002). Verbal *Classroom Interaction Patterns of Selected Secondary School Homescience Teachers with their students in Nairobi Province, Kenya*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).

Nkapa, N. (1997). *Educational Research for Modern Schools*. Unugu: Forth Dimension Publishing Companies.

Nsubuga, E.H. (2000). *Fundamentals of Educational Research*. Kampala: M. K. Publishers Ltd.

Odeo, I. (2007). *Matatizo ya Kufundisha Fasihi Simulizi katika Shule za Upili: Mtazamo wa Walimu.* Kiswahili na Elimu Nchini Kenya. Nairobi. Twaweza Communications.

Oluoch, G.R. (2002). *Essentials of Curriculum Development for Schools*. Nairobi: Elimu Bookshop.

Onyango, R. (2002). *"Matumizi ya Nyenzo katika Ufunzaji na Ufundishaji* wa *Kiswahili katika Madarasa ya Mwanzo ya Shule za Msingi za Manispaa ya Kakamega, Kenya.* Tasnifu ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. (Haijachapishwa).

Orodho, I. (1996). *Social Sciences Research for Environmental Improvement in Kenya.* Addis Ababa: Bureau of Education Research.

Orodho, J.A. (2003). *Elements of Education & Social Science Research Methods*. Nairobi: Masola Publishers.

Peil, M. (2002). *Social Reseacrch Methods:* A. Handbook. Nairobi: E.A.E.P

Peters, V. J. (1980). *Teaching-Learning Strategies*.From https://Journals.sagepub.com Retrieved, Thursday, June 21st 2018

Pollard, M. (2002*). Effective Teaching*. New York: Continuum.

Quist, D. (2000). *Primary Teaching Methods:* Malaysia: Macmillan Education Limited.

Republic of Kenya (2009). *Elimu News: A Newsletter of the Ministry of Education*. Nairobi: Ministry of Education.

Rodgers, S. (1976). *Approaches and Methods in Language Teaching. A Description and Analysis:* Cambridge University Press; Cambridge.

Ryan, F.B. & Giles, H. (1982). *Towards Language Attitudes Variation: Social and Applied Contexts*. London: Edwards Arnold.

Saunders, D. J. (1974). *Visual Communication Handbook: Teaching and Learning Using Simple Visual Materials.* London: Lutterworth Press.

Savignon, S. (2005). *Communicative Competence: An experiment in Foreign Language Teaching*. Montreal, Quebec: Marcel Didier.

Schultz, A. & Schultz, F. (1987). *A Neural Substrate of Predication and Reward*. Science.275:1593-1598.

Shiundu, J. & Omulando, S. (1992). *Curriculum Theory and Practice in Kenya.* Nairobi: Oxford University Press.

Shitemi, N. & Mwanakombo, M. N. (2001). *Kiswahili: A Tool for Multidisciplinary Approach*. Nairobi: Downtown Printing Works.

Sifuna, D. (1996). *Short Essays on Education in Kenya.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Skinner B. F. (1938). *Educational Psychology*. (4th ed). New York: Prentice Hall India Private Limited.

Skinner, B.F. (1957). *Verbal Behaviour*. New York: Appleton.

Stranda, E. M. (1980). *Educational Technology: It's Relevance to Teaching*. Seminar Paper No. 2049.

Stima, T. (1988). *Issuesof Implementing 8-4-4 Program and Inspection of Schools. Report of Educational Administration Conference*, Nairobi. Jomo Kenyatta Foundation.

Suad, A. (2009). *Problems in Reading Comprehension Skills Among Secondary School Students In Yemen*. ISSN-1930-2940

Thorndike, E. L. (1927). *Reading as Reasoning: A study of Mistakes in Paragraph Reading.* Journal of Educational Psychology, 8(6), 323-332. doi:10.1037/h0075325

Tuckman, B.W. (1988). *Conducting Education Research.* New York: Harcourt Brace, Janoritch Inc.

Tuntufye, N. & Mwakyembe, G. (1986). *Msingi wa Ualimu.* Dar es Salaam: General Publications Limited.

Urevbu, A. (1999). *Curricullum Studies*. Lagos: Longman Nigeria Ltd

Wambui, N. & Nyacomba, W. (2002). *SMASSE Impact Assessment Report*.

Wambui, M. (2015). *Ufundishaji wa Kusoma kwa Sauti Katika Madarasa ya Chini Katika Shule za Msingi Tarafa ya Gatanga.* Tasnifu ya Uzamili. Kenyatta University. (Haijachapishwa).

Wamitila, K. W. (2004). *Chemchemi za Kiswahili, Kidato cha Tatu: Mwongozo wa Mwalimu*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Wanjala F.S. na Kavoi, J.M. (2013). *Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili.*

Wanyama, P.O. (2007*). Silabasi Mpya: I Wapi Tofauti?* Education Insight, Issue No. 4 Pg. 2

Wasike, M. (2015). *Tathmini ya Matumizi ya Nyimbo za Kizazi Kipya Kama Mbinu ya Kufundishia Masuala Ibuka Kiswahili Katika Shule za Upili Nchini Kenya.* Tasnifu ya M.Ed. Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. (Haijachapishwa).

Wright, A. (1976). *Visual Materials for Language Teachers*. London: Longman Publishers.

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO A: HOJAJI YA MWALIMU

Hojaji hii inaniua kuhusu masuala yanayoadhiri ufunzaji na ujifunzaji wa ufahamu wa kusoma katika shule za Sekondari kaunti ndogo ya Kisumu Magharib. Tafadhali jaza nafasi katika hojaji uliyopewa. Hakuna haja ya kuandika jina lako. Maelezo utakayotoa yatatumiwa tu kwa kusudi la uchanganuzi huu na yatahifadhiwa sana wakati wa utafiti na baada ya utafiti

**SEHEMU YA B: Mbinu za Kufundishia Ufahamu**

(1) Je, ni mbinu gani unazotumia kufundishia ufahamu? Weka tiki panapofaa.

| **Mbinu** | **Inatumika** | **Haitumiki** |
|---|---|---|
| Makundi | | |
| Masaili | | |
| Kusoma kwa sauti | | |
| Kusoma kibinafsi | | |
| Mhadhara | | |
| Kusimulia hadithi | | |
| Mbinu ya kidrama | | |
| Mjadala | | |

(2) Kadiria matumizi yako ya mbinu za kufundishia kwa kuonyesha mara-idadi ya matumizi yako.

| Mbinu | Mara kwa mara | Wakati mwingine | Haitumiwi kamwe |
|---|---|---|---|
| Makundi | | | |
| Masaili | | | |
| Kusoma kwa sauti | | | |
| Kusoma kibinafsi | | | |
| Mhadhara | | | |
| Kusimulia hadithi | | | |
| Mbinu ya kidrama | | | |
| Mjadala | | | |

(3) Kadiria kiwango cha wanafunzi kuvutiwa, kupendelea au kustahabu mbinu zifuatazo za kufundishia. Weka tiki panapofaa.

Makundi Ndio [ ] La [ ]

Masaili Ndio [ ] La [ ]

Kusoma kwa sauti Ndio [ ] La [ ]

Kusoma kwa sauti Ndio [ ] La [ ]

Mhadhara Ndio [ ] La [ ]

Kusimulia hadithi Ndio [ ] La [ ]

Mbinu ya kidrama Ndio [ ] La [ ]

Mjadala Ndio [ ] La [ ]

**(4).** Je, ni sababu au vigezo gani vinavyothibiti au kuathiri uteuzi na matumizi yako ya mbinu katika ufundishaji wa ufahamu darasani? Weka tiki kwenye ‘ndio’ au ‘la’

Wingi wa wanafunzi Ndio [ ] La [ ]

Vipindi vichache vya kusoma Ndio [ ] La [ ]

Mielekeo ya wanafunzi Ndio [ ] la [ ]

Kazi nyingi ya mwalimu Ndio [ ] La [ ]

Nyinginezo (eleza)………………………………………………………………

**(5** Je, ni nini matokeo ya kutumia mbinu zisizo mwafaka kufundishia ufahamu darasani?

Mielekeo hasi upande wa wanafunzi Ndio [ ]La [ ]

Matokeo duni Ndio [ ]La [ ]

Motisha ya wanafunzi kudididimia Ndio [ ]La [ ]

Ushiriki wa walimu na wanafunzi katika somo uliodidimia Ndio [ ] La [ ]

**SEHEMU YA C: Matumizi ya Nyenzo**

**(6)** Je, ni nyenzo gani za kufundishia zinazopatikana shuleni mwako?

| **Nyenzo** | **Ipo** | **Haipo** |
|---|---|---|
| Vitabu vya kiada | | |
| Vitabu vya ziada/marejeleo | | |
| Miongozo ya walimu | | |
| Silabasi | | |
| Kamusi | | |
| Runinga | | |
| Kinasa sauti | | |
| Redio | | |
| Filamu | | |
| Magazeti | | |
| Majarida | | |
| Tarakilishi | | |
| Maktaba | | |
| Chumba cha Kiswahili | | |
| Mtandao | | |
| Picha | | |
| Michoro | | |
| Ubao | | |

| | | |
|---|---|---|
| Chati | | |
| Maleba na mapiku | | |

(7) (i) Onyesha idadi ya vitabu vya kiada kwa idadi ya wanafunzi darasani mwako………….. …………………………................................................

(ii)Je, kwa maoni yako, vitabu hivi vya kiada vinatosha wanafunzi katika darasa Lako ? Ndio [ ] La [ ]

(8) Ni mara ngapi wewe hutumia nyenzo zifuatazo katika kufundishia ufahamu? Weka tiki panapofaa.

| **Nyenzo** | **Mara kwa mara** | **Wakati mwingine** | **Haitumiwi kamwe** |
|---|---|---|---|
| Vitabu vya kiada | | | |
| Vitabu vya ziada/marejeleo | | | |
| Miongozo ya walimu | | | |
| Silabasi | | | |
| Kamusi | | | |
| Runinga | | | |
| Kinasa sauti | | | |
| Redio | | | |

| | | | |
|---|---|---|---|
